ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.

13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.

25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

Mhe. Spika, *(Pandu Ameir Kificho)* alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naomba kuweka mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko kw mwaka 2025/2016.

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo: Mhe. Spika, naomba kuweka mezani hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko kwa mwaka 2015/2016. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

(*Majadiliano yanaendelea)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii nikawa mchangiaji wa mwanzo katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri, pamoja na wetendaji wake wote kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya, lakini pia niwapongeze watendaji. Lakini vile vile nataka niwape pole watendaji wa Wizara hii. Katika Wizara ambayo ilipata misuko suko mikubwa sana katika bajeti zake ni Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Lakini tulikuwa tunafanya vile kwa nia njema ya kuboresha mambo yetu, ili yaende vizuri. Kwa hivyo kwa sasa hivi mimi nataka niseme *Alhamdulillahi* tunashukuru kwamba ingawa wenzetu walikuwa wanatuona wakorofi, wabaya, lakini matunda yake tumeanza kuyaona. Wizara sasa hivi inaanza kwenda vizuri na tunawaombea kila la kheri katika shughuli zao za huko baadae.

Mhe. Spika, nataka nimpe pole sana rafiki yangu mpenzi ndugu yangu Said Ndibugeni, kwa matatizo aliyoyapata kiafya na tunamuomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema, ili aendelee kulitumikia taifa letu. Kwa hiyo vile vile nataka niwape pole na wengine ambao sikuwataja majina yao, ambao walipata kadhia tofauti katika kipindi hiki, sasa nakuja katika mada.

Mhe. Spika, nataka nianze na Shirika la Bandari nilikuwa na hamu sana awepo Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria ili hili nitakalolizungumza hapa Mhe. Waziri wa

Miundombinu ashirikiane na Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria, ili kuwasaidia Wazanzibari walioamua kujitolea muhanga kufanya biashara, ili kuweza kutoa ajira kwa watu wengine.

Mhe. Spika, kuna kadhia kubwa sana ya muwekezaji mzalendo ambae amenunua meli iliyokuwa ikiitwa Sepideh na sasa hivi meli ile imeshabadilishwa jina baada ya kuuziwa kwa njia ya mnada na Serikali, kwa bahati mbaya sana Mzalendo yule ameshatumia karibu bilioni moja baada ya kununua hiyo meli, karibu bilioni moja kuifanyia *renovation* meli ili ianze kazi. Ni kitu cha kusikitisha sana, kwamba leo meli ile tulitegemea ingeliweza kusaidia kuondoa au kupunguza tatizo la usafiri baina ya Unguja na Pemba na Tanzania Bara.

Mhe. Spika, meli ile imezuiwa haifanyi kazi, sasa mimi nilikuwa naomba sana Waheshimiwa Mawaziri waliokoe hili, hakuna kitu kizito kama mwananchi kujitolea kutoa pesa zake akaamua kuwekeza, hatujui hawa wafanya biashara pesa hizo wanazitoa wapi. Tunajua biashara nyingi zinaendana na mikopo, leo kama mtu bilioni moja hiyo ameikopa benki, si mtakuja kusikia mtu ameshapata *stroke*, hizi *stroke* usifikirie watu wanazipata tu mawazo na fikra zinawazidi kimo, sasa hili naomba liingiliwe kati.

Kwa sababu meli ipo pale maana tunaambiwa Shirika la Bandari wanadai, lakini sasa mnadai imekuwa kama ile hadithi ya nyoka wa mdimu; nyoka wa mdimu anakaa kwenye mdimu yeye ndimu hali anayekuja anamfokea, kwa sababu meli kama mnadai mngekubaliana kwa maandishi na mimi niko tayari kuwa wakili, tumepitisha sheria hapa ya *arbitration* na hili Mhe. Waziri wa Biashara naomba pia na wewe uingie kati mlisaidie, tena nakuombeni Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Waziri wa Miundombinu.

Waziri wa biashara hebu likalieni kitako, muliangalie hili hamuwezi kulitatua kama mnamnadi yule tena basi, yeye hiyo meli ilikuwa inadaiwa na Shirika, yeye kabla hajainunua imepigwa mnada kila anayedai ajitokeze wao hawakujitokeza, leo mtu keshabarikiwa tena imepigwa kwa njia ya mahakama. Naomba sana Mhe. Spika, mukae na mdau yule ili mukubaliane aanze kazi basi iweze kulipa kidogo kidogo wenzetu Tanzania bara, ndio wanavyofanya wanapokuwa wanadai hizi meli au makampuni ya meli, wanaandikiana mikataba kila mwezi utalipa limalize na ile meli ifanye kazi, si hivyo tutakuwa wafanyabiashara baada ya kuwapa moyo tutakuwa tunawaangusha na watakimbia hilo moja.

Lakini utendaji wa Shirika la Bandari kwa kweli nafurahi wanakwenda vizuri isipokuwa tu katika kile kiambatanisho namba sita(6), nilikuwa naomba Mhe. Waziri aje atupe maelezo, kwa sababu naona idadi ya meli kutoka mwaka

2013/2014/2015 zinapungua. Hebu Mhe. Waziri aje atupe kuna sababu gani, hili nilikuwa kidogo nataka maelezo.

Nakuja Mamlaka ya Uwanja wa Ndege, kama nilivyosema kauli imebadilika; tunawapongeza, tunaona maboresho kama alivyosema Jana *Professor* Mshimba, tunaposafiri sisi nchi za watu tukaona pale viwanjani vinavutia na vinapendeza na sisi kwa kweli tulikuwa tunaona choyo. Sasa hivi kidogo tunaanza kuona hali inaanza kubadika.

Nna ushauri eneo la uwanja wa ndege bado ni dogo, ule ukuta tunaojenga Mhe. Spika, nchi yetu tunategemea si muda mrefu tutapata rasilimali kubwa sana ya kiuchumi, nchi inapoanza kuingia katika uchumi wa mafuta na gesi uchumi wake unakua kwa haraka. Eneo la uwanja wa ndege ni dogo, kwa sababu hapa tukiweza kuvuna gesi na mafuta yatakuja makampuni mbali mbali kuwekeza. Watu watataka kuweka ma-*ai*r *house* pale, kuna madege ya *air cargo* zitakuja; inamaana itabidi tuwe na uwanja wa *passenger,* tuwe na uwanja wa *cargo.* Lakini vile vile kuna maghala mengi yatahitajika kujengwa katika uwanja wetu wa ndege, ili uweze kuhudumia abiria wengi.

Sasa nilikuwa nataka kujua je, tuna *master plan* ya uwanja wa ndege wa Zanzibar, na kama hiyo *master plan* tumeweza kujaribu kuangalia mahitaji ya baadae, sasa hili nilikuwa naomba, Mhe. Waziri aje anisaidie maelezo.

Kuna suala, *hear say* baadae inaweza ikaja ikawa ya kweli; tuna taarifa kwamba kunatakiwa kufanywa marekebisho ya masaa ya kazi kwa wafanyakazi wa mamlaka ya uwanja wa ndege, badala ya kufanya kazi masaa nane watatakiwa kufanya kazi masaa kumi na mbili. Sasa Mhe. spika, kuna sheria za kazi duniani sisi Zanzibar sio kisiwa kwa jina tu lakini tuko katika mfumo wa dunia, Sheria za kazi duniani, ufanyaji wa kazi ni masaa manene(8) zamani watu walikuwa wanafanyishwa kazi bila ya muda, wakaandamana ndio maana mpaka leo tuna siku ya wafanyakazi duniani.

Sasa mtu anapozidi kufanya kazi masaa manane ina maana hapo uangalie utaratibu wa *overtime,* lakini Mamlaka ya Uwanja wa ndege wamo wafanyakazi wanawake; dume linaweza kufanya kazi masaa 12, lakini wanawake tofauti. Mwanamke akizidi masaa manane kufanya kazi itabidi akakoge, ndio nawapongeza sio nawadharau. Nawaboresha kwa sababu mwanamke anatakiwa awe anapendeza kila wakati. Mtu kashapiga shedo zake, rangi za mdomo masaa manane yamepita uso utakujaanza kuonekana una mabaka hapa rangi ya buluu, hapa rangi nyekundu, tunajua watu siku hizi wanavyoishi.

Kwa mfano kama sisi tunaopita pita pale VIP, unapopita unatakiwa uone sura ya *VIP*, yaani sasa unapoteremka *international flight* yule *air hostess* unamkuta kwenye ndege ukija pala VIP awe wamefanana fanana, leo masaa 12 watakuja kufanana fanana.

Kuna safari moja nilikwenda Mwanza, basi la Mwanza kuanzia 12 asubuhi mpaka saa 6.00 usiku, tumekaa mara tumeanza kusikia mmmm mmm utafikiri mna ng'onda mle, sasa kufika njiani kuna abiria mmoja akaja akateremka ile harufu yote ikatoka. Sasa hatujui kuna mazingira gani yalitokezea mule kwenye basi baada ya kuteremka yeye, sasa yasije yakatukuta na sisi katika mazingira yetu. Sasa hili nimejaribu kulitolea maelezo mengi, tunataka tu kujua je, kweli na kama watafanyakazi masaa 12 mfululizo, je, tumefuata sheria ya kazi Duniani. Hilo nilikuwa nataka niliwache hapo.

Jengine Mhe. Spika, nakuja katika Idara ya Ujenzi na utunzaji wa Barabara; mimi kwa kweli nawapongeza sana kama walivyowapongeza wenzangu. Nilikuwa nataka kujua tu Mhe. Waziri tupitishe sheria za Tawala za Mikoa sasa hivi inaruhusu Halmashauri na Mabaraza ya Miji kuweza kufanya baadhi ya kazi. Kuna kazi siku zote tulikuwa tunawalaumu Wizara ya Miundombin, kuna hizi *feeder road* na katika sheria tuliyoipitisha kwamba sasa hivi Zanzibar kutakuwa kuna mji na kutakuwa kuna jiji. Moja kati ya masharti ya jiji, hizi barabara za ndani ndani *feeder road* zile zote zinatakiwa ziwe katika kiwango bora tena ikiwezekana kiwango cha lami. Sasa je, Halmashauri tayari watakuwa wameshapewa hiyo kazi katika hii programu ya mwaka unaokuja wa PBB, kwa ajili ya kuweza kujenga hizi barabara ili tuweze kujua.

Hilo naliulizia kwa sababu nashukuru sana Wizara ya Miundombinu baada ya kelele zangu za muda mrefu, kile kibarabara changu nilichokuwa nakipigia kelele kwa Abasi Husein mpaka mboriborini mpaka kule Makamo Makuu ya Chama cha CUF pale kwa rafiki yangu Mazurui, ile barabara tunashukuru imeboreshwa kwa kiasi fulani. Zile kelele za wananchi wangu zimepungua, lakini Mhe. Waziri nilikuwa nakuomba; maana yake imekuwa kama nakwenda kunyoa ukanikata panki, nywele upande mmoja zimekwisha upande mmoja zimebakia.

Sasa basi nilikuwa naomba Mheshimiwa najua rafiki yangu Mheshimiwa Gavu ananitizama huku anacheka cheka maana mwanzo aliniambia ile barabara haipishani gari, lakini sasa hivi baada ya kuitia lami gari zinapishana kweli kweli, waimalizie na ndio maana nikauliza je, hii kazi kama imeshapewa Halmashauri na Baraza la Miji kufanya hizi kazi za *feeder road*, sawa nitahamisha hoja yangu nitaipeleka huko. Lakini kama bado barabara zile watazishughulikia wao basi nilikuwa naomba ile sehemu iweze kumaliziwa.

Mhe. Spika, naona unaniangalia sana; kimsingi nilikuwa sina mambo mengi sana katika Wizara hii lakini kwa kweli kama nilivyosema nawapongeza sana kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya.

La mwisho kabisa kabisa nilikuwa naomba; pamoja na kwamba tumepitisha hizi sheria za *local government* ambazo hizi kuna makampuni yatakuwa yanapewa tenda kwa ajili ya ujenzi wa barabara, lakini bado naomba sana tuige mfano wa wenzetu China; hii Idara ya *UUB* iongezewe nyenzo kwa ajili ya kufanya kazi pamoja na kazi nyengine zitapewa kampuni binafsi, lakini bado kampuni ya Serikali nayo inatakiwa lazima ipewe zana, iboreshwe ili iweze kufanya kazi vizuri. Kama walivyosema wenzangu tunashukuru wale vijana ni hodari sana, wanafanya kazi vizuri. Kwa hivyo kitu kikubwa tunachotaka kwamba wapewe nyenzo za kufanyia kazi, ili waweze kutuboreshea barabara zetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache kwa kweli nakushukuru sana kwa kuweza kunivumilia na hoja hii, sina wasi wasi nayo nitaiunga mkono na yale ambayo nimeyauliza nitaomba tu Mhe. Waziri aje anisaidie ufafanuzi, ili niridhike nisije nikapinga kifungu kwa kutaka ufafanuzi wa ziada, nakushukuru sana Mheshmiwa Spika.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia machache katika bajeti hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kufika hapa katika ukumbi huu nikiwa na afya njema *Alhamdulillahi* na pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi.

Mhe. Spika, naomba nimpongeze Mhe. Waziri, kwa uwasilishaji wa hutuba yake hii kwa umakini na ikafahamika, pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara hii akiwemo Katibu Mkuu, Naibu, Wakurugenzi na watendaji wote kwa kufanikisha hotuba hii.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze moja kwa moja katika ukurasa wa 5 katika mradi wa Uimarishaji wa Viwanja vya Ndege, Pemba.

Mhe. Spika, nataka niseme kiwanja cha Ndege Pemba imekuwa ni wimbo wa taifa, imekuwa ni wimbo au shairi na kiitikio. Kila siku kiwanja cha Ndege hiki tokea nimeingia katika Baraza hili na nina imani tokea walioingia mabaraza ya nyuma pia walikuwa wakilipigia kelele suala hili. Lakini nizungumzie hapa hapa baada ya kuingia mie katika hili Baraza.

Baada ya kuingia mie katika hili Baraza kila siku nasikia hapa linazungumziwa suala la kuwekwa taa katika uwanja wa ndege wa Pemba. Tokea wengine hawajawa mawaziri walikuwa wanalisisitiza suala hili mpaka kwa bahati njema wakapata uwaziri na wao wakalizungumza hili, mpaka wakafikia kusema kwamba pawekwe mishumaa na mpaka leo hii. Linasikitisha kuwa Uwanja wa Ndege ule wa Pemba kila siku unazungumzwa kwenye vitabu, lakini kwenye utekelezaji haujaonekana na hatuna tamaa ya kuoenekana utekelezaji wake.

Mhe. Spika, nasema hili kwa sababu, nataka nianze kwenye huo uwekaji wa taa zenyewe. Kuna kipindi cha karibuni walikuja pale watu wakafanya kuchimbua chimbua siku mbili tatu wameshaondoka hawapo. Sasa hapa ninamuomba Mhe. Waziri atakapokuja, anipe majibu mazuri yatakayoniridhisha na kuwaamini hasa kwamba lini Uwanja wa Ndege ule wa Pemba, zile taa zitawekwa pale angalau kuondosha matatizo yanayojitokeza mara kwa mara. Mara ndege inakwenda kwenye majani, mara ndege inatua hapa. Kwa hiyo naomba sana hili Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe majibu ya kuridhisha.

Nikija katika eneo jengine Mhe. Spika, pale pale katika Uwanja wa Ndege wa Pemba; katika eneo la kusubiria abiria, hapana tofauti na ule uwanja wa mpira au uwanja mwengine. Pale wanaosafiri ni watu wa aina tofauti, wengine wagonjwa na wengine wana watoto wachanga, jua linaloingia mle ndani linasikitisha. Utawakuta watu wanavuja jasho kama waliokuwepo kwenye michirizi ya maji wanaovujiwa na mvua. Sasa naomba Mhe. Waziri atwambie ni lini hasa eneo lile nalo litatayarishwa lionekana ni eneo ambalo abiria wanasubiri kuingia kwenye ndege au kupanda ndege, ili na wao wajisikie katika lile eneo kama ni watu.

Mhe. Spika, nasema hili kwa sababu hakuna lisilowezekana. Uwanja wa Unguja kabla ya matengenezo wa lile geti Nam. 5 wanapopanda abiria kwendea Pemba palikuwa na tatizo kama hilo, tulikuwa tukiingia pale juwa kali, joto hapakaliki. Lakini kwa muda mfupi sana pamefanyiwa matengenezo sasa hivi ukipita pale panaridhisha, unajisikia hasa, hata kama ndege imechelewa kuondoka au kuja basi pale hupati tabu, upo katika hali nzuri.

Kwa nini Pemba iwe eneo lile haliwezi kutayarishwa. Je, Mhe. Waziri siye wapemba pale hatulipi kodi ndio maana ikawa sisi tunaonewa kiasi hiki au kulikoni? Inasikitisha Mhe. Spika.

Ukija katika eneo jengine kuna eneo, sasa hivi wasafiri tumekuwa wengi, ndege ni nyingi, abiria ni wengi, sasa pale watu wanakuja na mizigo, baada ya kupitishwa katika eneo husika la kuonekana ndani ya mzigo huu kuna kitu gani cha hatari au cha salama, mizigo inapitishwa mvunguni pale inatiwa karatasi ya jina lako inakwenda, hapajulikani kama mzigo ule una kitu cha hatari au vyenginevyo.

Kwa nini Pemba pameshindikana napo kuwepo kitu cha kuchunguza pakajulikana kama kitu hiki ni cha salama au si salama. Imebakia pale wapemba tukiingia pale mzigo umeshapita kule, unapapaswa papaswa, wewe kutizamwa una nini au huna nini. Hili ni tatizo na tunaiomba Wizara hii ilione suala la Uwanja wa Ndege, Pemba nalo angalau uonekana ni wa Uwanja wa Ndege na wanaosafiri pale ni binaadamu. Kwa sababu viongozi wote wakubwa hawapiti pale, viongozi wakubwa wanapita VIP, lakini wale abiria wetu wanyonge wanaopita pale ndiyo wanayoiona ile balaa. Kwa hivyo naomba katika hili.

Mhe. Spika, halafu kuna taarifa ya Jumuia ya Afrika Mashariki katika uwanja wa ndege huu, ilikaa na kufanya kujadiliana au kukaa kikao cha pamoja au vyenginevyo, kufanya tathmini kuwa wanataka kusaidia Zanzibar. Miongoni mwa malengo waliofikiria ni kusaidia ule uwanja wa ndege wa Pemba. Lakini wenzetu Wabunge kutoka Zanzibar wakilihoji hilo wanaambiwa upembuzi yakinifu bado haujawa tayari. Hivi niulize huu upembuzi yakinifu ni mwaka wa tano tokea waingie wabunge wa awamu hii wanaliulizia suala hili, sijui huko nyuma na mpaka leo haujakamilika. Unachukua muda gani na unagharama kiasi gani au labda hakuna wataalamu hapa Zanzibar wa kufanya hilo? Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa pia anijibu.

Mhe. Spika, nikiendelea katika sehemu nyengine ya mradi wa ujenzi wa barabara tatu za Pemba. Niipongeze sana serikali kupitia Wizara hii kwa kutengeneza barabara hizi tatu Pemba, zilizochukua muda mrefu na sasa nashukuru, zimekamilika. Lakini hakuna kitu kisichokuwa na changamoto; katika ujenzi wa barabara tatu hizi, Wete/Gando na Wete/Konde na ile inayotoka Wete kuelekea njia ya kutokea Micheweni, Wingwi, barabara zile zimezua migogoro mikubwa baadaye.

Mhe. Spika, katika utengenezaji wa barabara kuna mambo matatu au zaidi huwa yanafanyika.

- Kuna watu wanaopimiwa awali, kwa kuvunjiwa majumba kwa sababu ya kupita barabara;

- Kuna watu ambao hazikuvunjwa nyumba zao lakini baadae zimepata athari kubwa mpaka kuanguka kwa sababu ya kupita zile zana nzito za barabara; na

- Kuna watu ambao pia nyumba zao zinapata mipasuko baada ya hatua ya mwisho ile ya kutengeneza na kutia lami na mambo mengine.

Sasa mambo haya yote yamejitokeza katika hatua hii katika mabarabara haya ya Wete/Gando na Wete/Konde. Cha kusikitisha;

- Kuna watu wamefanyiwa tathimini ya awali hawajalipwa;
- Kuna watu wamefanyiwa tathmini ya awali wamelipwa; na
- Kuna watu ambao nyumba zao zimevunjika kabisa na nimeziona kwa macho yangu, sio kwa sababu nahadithia au nasema jambo nisilokuwa na uhakika nalo, nimekwenda mimi katika ile barabara kuzikagua nyumba na nikazikuta nyumba nyingi zimeanguka nusu nzima, ziko chini na watu wale mpaka leo hii hawajalipwa.

Mhe. Spika, cha kusikitisha zaidi kuna baadhi ya nyumba nyengine wale waliokuwemo ndani ya zile nyumba maeneo ya Chanjaani ni masikini wa Mungu, wanyonge, halafu ndani ya nyumba moja kuna mama mmoja ana mama yake ni kipofu haoni. Nimekwenda nyumba hiyo ipo chini, mvua yote inanyeshea ndani mvua hizi zilizopita na mpaka leo hii ninavyozungumza hapa hawajalipwa. Wapo wengi hao kuanzia Madaniwa, mpaka Gando, mpaka Junguni, mpaka Uvinje, Chanjaani, kote watu hao hawajalipwa na wanapouliza katika Wizara, majibu wanayopewa wanaambiwa mpaka barabara hii ifunguliwe. Wengine wanaambiwa baada ya Rais kuja kufungua, ndio watalipwa.

Hivi je, Mhe. Waziri naomba niulize hatma ya watu hawa waliovunjiwa majumba yao katika njia tatu tofauti hizo nilizozitaja hapa zitalipwa lini? Ramadhani hii inakuja watu wanapika nje, wapigwe na jua na kama kawaida mnavyowajua watu wetu wanakaa pahali kifamilia, pengine Kijiji kizima kina watu ndugu. Sasa nyumba zote zimevurugika hapana hata mmoja anayeweza kumsaidia mwenziwe. Kiukweli hili linatusikitisha, tunahitaji sana maendeleo ya watu wa Zanzibar, tumezifurahia sana barabara, lakini athari zilizojitokeza kwa barabara zimekuwa kubwa kuliko hiyo faida yenyewe.
Tunaomba sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe majibu mazuri, ni lini watalipwa watu hawa. Na ni kwa nini kwa muda wote huo hawajalipwa.

Mhe. Spika, cha kusikitisha zaidi kuna baadhi ya nyumba zilifanyiwa tathmini ya mwanzo na wamelipwa, lakini baada ya kulipwa wakajenga nyumba nyengine, lakini baada ya kwisha kujenga nyumba nyengine zikafanya mtikisiko baada ya ujenzi zimefanyiwa tena tathmini mpya wanategemea walipwe tena. Hili linasikitisha mnavyowaumiza watu katika kuwanyima haki yao hii kwa muda mrefu. Mtu akikosa pakukaa ndiyo tayari keshaumbuka. Mtu anahangaika na kutafuta mahali pa kuishi miaka na familia yake, kisha anakaa jumba linaanguka, haliulizwi anatiwa kikombeni akitiwa kisahanini, haipendezi! Mimi si mtu wa tabu

katika kuchangia bajeti, lakini hili kwa vile lilivyoniuma kama sijapata majibu mazuri, nitawashawishi wenzangu hii bajeti tusiipitishe.

Mhe. Spika, sasa naomba nije katika sehemu nyengine ya Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara, nimeona hapa majukumu yao ni pamoja na kufanyia marekebisho madogo madogo kama kuna mashimo, kukata majani, kukata miti. Hili lengo waliloliweka ni zuri lakini utekelezaji wake nao pia unakuwa mgumu. Nasema hivi kwa sababu katika hii barabara inayokwenda Kaskazini kuna hii barabara inayotoka Bububu mpaka Mkokotoni, ile barabara katika barabara zilizojengwa kwa umadhubuti na umakini mkubwa ni barabara ile. Lakini sasa hivi imeshaanza kufanya athari, ina mashimo kila eneo tena mashimo yenyewe ni mabaya mengine yapo kati, mengine yapo pembezoni. Barabara hii ina watu wengi, abiria wengi, wageni wengi wanaopita, watalii wetu ambao ndiyo wanaotuingizia pato la taifa. Sasa lakini barabara kama ile inaachiwa, kwa sasa basi itaishia kuharibika kabisa kabisa iwe sisi tayari tunahitaji kujenga upya wakati watu wa zamani walisema usipoziba ufa utajenga ukuta. Naiyomba sana wizara ilione hili, zile barabara zianze kufanyiwa matengenezo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Pemba barabara ya Mkoani ni barabara mbaya sana iliyokuwa na krosi nyingi kila mmoja anaiyona. Lakini kwa bahati kuna maeneo mengine unapopita kutoka Chake-Chake, kwenye Mkoani basi huiyoni gari inayokuja kutoka huku kwendea huku kwa sababu ya lile pori lililopo. Sasa sijui hii Idara iliyosema kwamba kazi yake ni utunzaji na kuna baadhi ya maeneo yao waliyosema ni usafishaji na mambo mengine, sijui wanaliangalia vipi hili.

Naomba Mhe. Spika, Waziri asilikalie kimya awaagize watu wa Idara yake waende katika maeneo husika na waangalie katika kona zile za kutokea Mkoani kwenda Chake Chake, kuna maeneo ya hatari sana na yatasababisha ajali kwa sababu huwezi kuona kilichopo mbele yako kwa mapori yaliyopo na mapori mengine hata hayana ulazima.

Mhe. Spika, nije katika bandari sasa. Mimi bado nitaendelea kuwa na kilio changu katika bandari. Lakini hapa niliona kama kuna uboreshaji au utengenezaji wa bandari ya Mkokotoni na Tumbatu. Ni jambo zuri kwa sababu ni pahali palipokuwa kuna watu wengi. Maeneo ya visiwa kukitengenezwa Bandari tutapata maendeleo na mambo mengine. Lakini nataka niseme jambo nililoliona jana asubuhi katika Bandari ya Mkokotoni tumeshuhudia gari ikiingia ndani ya bahari, ilirudi nyuma katika kuteremsha mzigo kwa bahati mbaya ikatumbukia ndani ya bahari, lilitangazwa kwenye vyombo vya habari tukaliona. Kwa hivyo naiyomba sana Wizara maeneo yaliyokuwa kidogo hayapo vizuri; yana hatari yafanyiwe marekebisho kwa nguvu zote.

Halafu tukija kwenye upande wa Pemba; jamani sisi Pemba tumekuwa mayatima sijui tumekosa nini, Mwenyezi Mungu atusaidie. Hivi jamani tokea ilivyozama MV. Spice tunapiga kelele na kuendelea kupiga kelele mpaka leo hii bandari ile ya Wete imekosea nini na Watu wa Kaskazini kwa ujumla kuachwa katika hali duni kama ile, Mhe. Spika.

Mhe. Spika, naiyomba Wizara ituonee huruma Wazanzibari wa Kisiwa cha Pemba hasa Mkoa wa Kaskazini tunapata tabu jamani. Serikali kila siku inatafuta wafadhili, wawekezaji, hebu naomba jamani ile Bandari ya Wete nayo iyoneeni huruma, maana yake tumechoka kila siku kuambiwa kesho, kesho, kesho, mtoto wa kuku, tusaidieni jamani, tunaomba, chonde chonde jamani, tusaidieni Wakaskazini Pemba, tumechoka kudhalilika!

Mhe. Spika, kiukweli katika hili la Bandari ya Wete kila siku tunalipigia makelele na ni kwa sababu sisi watu wa Kaskazini Pemba tunafanya kazi za biashara, asilimia kubwa ni wafanyabiashara. Lakini tunachokifanya sisi kutoka pale Wete, wafanyabiashara kutoka Wete, Micheweni, Madenjani na sehemu nyengine. Kutoka pale mpaka kufika Mkoani na biashara, hasara watakayoipata ni kubwa sana.

Sasa imekuwa wafanyabiashara wa maeneo haya hawapati faida isipokuwa wao wanaendelea na kula hasara na kuwalisha madereva tu.

Mhe. Spika, kwa hivyo naomba Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla ilitizame hili kwa moyo wa huruma ili ile bandari ya Wete ifanikiwe na ikifanikiwa bandari ya Wete tutapungua na haya matatizo ya vijana wetu wote kuhama wakaelekea katika miji hii, ikaonekana kwamba vijana hawataki kukaa kwao.

Vijana wetu wanapenda sana kukaa kwao, lakini kwa sababu hakuna kazi ya kufanya. Lakini bandari ile itakapokamilika watu watapata ajira pale. Wafanyabiashara itakuwa rahisi, tutapata safari za kwenda Tanga na Mombasa na sisi tutakuwa miongoni mwa watu tutakaojitegemea.

Mhe. Spika, pia kuna watu waliobomokewa na majumba, sasa hapa Mhe. Waziri naomba anijibu katika maeneo matatu;

Kuna watu waliovunjiwa kwa sababu ya barabara wale watalipwa lini;

Kuna watu walioharibikiwa wakafanyiwa tathmini mara ya pili; na

Kuna watu wengine ambao wao hawakufanyiwa hata tathmini.

Lakini ukiziangatia kama mimi nikiangalia naona hizi nyumba zote zinahitaji kulipwa, kwa sababu zimekatika viambaza vyote vipo chini. Lakini wale wanaopiga tathmini wanawambia watu kwamba hawa hawawezi kulipwa kwa sababu wao wapo mbali na barabara, lakini ukiwaangalia wapo karibu na barabara na chanzo cha kuharibikiwa ni barabara.

Mfano huu upo katika barabara hii inayoelekea Micheweni/Wingi, Mzambarau Karimu. Pale kuna baadhi ya vijana kama sita; mmoja nyumba yake ilikuwa bekari lakini imevunjika kwa sababu hiyo. Watu wa mara ya mwanzo Wizara ilipokwenda ikafanya tathmini ikamwambia itamlipa lakini baadae wakageuka wakasema hawawezi kuwalipa kwa sababu wako mbali.

Sasa nawaomba kabla Mhe. Rais hajenda kufungua barabara zile za Pemba walipwe watu haki zao bila ya hilo mtawaweka watu katika wakati mgumu watakuja kusema maneno yaliyokuwa hayasemeki, na lengo letu ni kufanikisha watu kupewa haki zao.

Nakushukuru Mhe. Spika, sitounga mkono hii hoja mpaka nitakapopata majibu mazuri katika maeneo hayo ya kiwanja cha ndege Pemba, barabara hizi watu wanaodai haki zao, na maeneo ya bandari ya Wete lini na sisi tutapata kujengewa ile bandari. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Asante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Wizara ya Miundombinu, wizara ambao ni muhimu kwa kila kiumbe hai anaihitaji Wizara hii. Nichukue fursa hii vile kumpongeza Mhe. Naibu Waziri, rafiki yangu Issa Ussi Haji (Gavu) kwa kupata mtoto jana wa kike na amjaalie mtoto huyo awe wa kheri na amjaalie afya njema na aendelee vizuri.

Baada ya hapo nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote, kwa jitihada na umakini wanaofanya. Nimwambie tu Mhe. Waziri na watendaji wake, sijui mganga wako nani safari hii alikuwa. Maana katika Wizara iliyokuwa ikipata shida moja wapo ni Wizara hii. Sisi sote mashahidi Wizara hii katika bajeti zilizopita ilichezea mikwara mingi na uliipitisha bajeti hapa kwa aina yake sijawahi kuona.

Kazi waliyoifanya Wajumbe ni halali na niwapongeze kwa dhati kabisa, kuna msemo unaosema "Hohe hahee nacho kilindo" Ndiyo haya matokeo yake, Wizara hii kuonekana *improvement* yake. Hatuna nia mbaya kupiga kelele ila ni kuwasaidia na matokeo yake tunayaona.

Mhe. Spika, nianze na hii Wizara yenyewe ilivyo mpangilio wake siji kama ni Wizara ya Miundo Mbinu au miundo mibovu. Haiwezekani Wizara, Ofisi ikajengwe nje ya Mji kama kweli unataka kuwatumikia wananchi. Ofisi imejengwa

maeneo ya Fumba huko, wameacha eneo lao walilokuwa wakilitumia karibu miaka miwili, mitatu, kisingizio chenyewe nafasi ile pale ni ndogo. Ndiyo vile vile na huko ukenda Ofisini labda uwanja mkubwa tu wa *parking* ya magari. Lakini mimi sijaona hoja ya kuhama pale katika jengo lao walilokuwa nalo wakilitumia. Sio lile la zamani. Leo mwananchi atatoka hapa kumfuata Waziri kule, hakumkuta, Naibu Waziri hakumkuta? Bado wizara haijawa tayari kuwatumikia wananchi.

Niende na Uwanja wa Ndege, kwanza na mimi niungane na Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa kumshukuru Mkurugenzi wa Uwanja wa Ndege kwa kazi aliyoifanya; sote tumeiyona na ajue tu kuwa hatukuwa na nia mbaya na yeye, matokeo yake ndiyo haya anayoyaona. Kuisaidia serikali na kuihoji, ndio kazi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Kuhusu uingiaji wa magari ya viongozi yenye nembo za SMZ na nembo za Mawaziri, leo ikawa gari ya Mhe. Hija kama kiongozi vile vile pale kalipa shilingi elfu mbili huu ni ubaguzi. Ikawa gari ya SMZ au nembo ya Waziri inaingia pale bure, hiki si kitu halali, sisi sote tunatembea tunaona, hapo tu kwa ndugu zetu Dar es Salaam ikaingia gari ya kiongozi wala haiulizwi chochote, hata ikawa *private* kama kiongozi ukionesha kitambulisho chako inapita VIP. Kwa hivyo Mkurugenzi ajirekebishe, hii hoja sio ya Waziri au Naibu Waziri, gari ya SMZ hili alirekebishe. Amefanya kazi kubwa sote tumeiona, nina ushahidi na hili niko tayari kubishana kwa vyovyote lipo.

Niendelee kumpongeza tena katika utanuzi wa Uwanja wa Ndege, jitihada alizochukua ni kubwa sana sote mashahidi, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Lakini kwa masikitiko mengine yale mabasi yaliyokwenda kununuliwa kama ndio mkopo wa PBZ yale hayaendani na wakati. Zile ni daladala. Tumeona mabasi yanachukuwa abiria yalivyokuwa marefu na makubwa, zile basi kwa wenzetu ni daladala hazilingani na hadhi ya kuchukua abiria mule. Hivyo tujipange angalau mawili au moja kubwa, lakini lionekane lile basi angalau watu wengi wanaingia. Zile hazikidhi pale kwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa.

Nije sehemu nyengine ndogo; hii kila wakati ninaipigia kelele eneo wanapotoka abiria kufika mbele unazunguka, pale patafutiwe utaratibu mwengine abiria anazunguka. Abiria akishakuteremka tu pale anazungushwa nyuma, eneo pale liko wazi hakuna sababu kama usalama si kweli kabisa.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 6 ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri; huu wimbo umekuwa wa taifa siku zote unapigwa humu ndani, hakuna ukweli, uongo. Siku zote wimbo huu unapigiwa mziki lakini mwisho wake hakuna kinachoendelea. Sasa mimi niombe Mhe. Waziri, watendaji wake fanyeni kitu kwanza halafu

mtuletee, msituuzie mbuzi kwenye gunia. Hii kila siku hadithi inakuja ya Mpigaduri, Mpiga dodo, Mpiga embe, hakuna lililoekea.

Nije ujenzi wa meli mpya; ujenzi wa meli mpya imeitwa MV Mapinduzi II, hebu tuulizane hiyo Mapinduzi I iko wapi? Sasa kwa nini isiitwe Mapinduzi ikaitwa Mapinduzi II mtu akaja akauliza Mapinduzi I nioneshe iko wapi? Huu ni upangaji mbovu. Hili jina lifikiriwe. Hesabu inaanza moja, haianzi mbili. Haiwezi kuitwa Mapinduzi II, moja iko wapi. Lakini uzoefu unaonesha Shirika la Bandari walikuwa na meli ngapi. Mhe. Salim wa Mtambwe alizungumza palikuwa na meli nne, hakuna kilichozalika hata kimoja. Hii ni sawa sawa kuchukua sukari kutia kwenye maji ya chumvi, hutopata maji matamu.

Shirika lijipange, hii meli iliyogharimu karibu milioni thalathini dola, hapa vile vile Serikali ilikuwa na uwezo wa kununua meli nne mpya kwa pesa hizi. Chombo kimoja huwezi kufanya kazi. Milioni thalathini na tatu dola ni meli karibu tatu au nne za kileo, tena mpya unanunua. Leo meli yenyewe moja hii itafanya kazi kweli?

Shirika la Bandari bado halijajipanga, lina kazi kubwa Mhe. Waziri tena panataka umakini wa hali ya juu. Palikuwa na meli karibu nne hakuna hata meli moja iliyopatikana mpya kutokana na meli hizi. Hili sijui tuseme litaendelea kuwa shamba la bibi vile vile, lakini tuendelee.

Mhe. Spika, naendelea katika Shirika la Bandari ndani ya Bandari. Nimpongeze sana Mkurugenzi kwa jitihada anazozichukua, amekuwa msikivu Mkurugenzi Mkuu wa Bandari na jitihada tunaziona, lakini bado hali inahitaji maelekezo pengine hayaoni labda tumsaidie. Kule Tanzania Bara wenzetu kuna kitengo cha kushushia makontena wanapewa tiketi, sijui kama utaratibu unaendelea. Juzi nimeuliza humu Naibu Waziri yuko mbele akajibu anavyofahamu yeye, lakini ukweli wakati unataka kufanya maendeleo tulinganishe na wenzetu. Kazi anayofanya mtu binafsi na watu wengine tofauti. Bandari yetu imekuwa ni ndogo, haikidhi. Bandari ile tayari imeshadidimia hivi sasa, tutafanya kazi kwa mazingira gani?

Chengine cha kushangaza kuna bandari Forodha mchanga imefungwa lakini tunashuhudia meli za Serikali zinakwenda kule zinakaa pale siku tatu, siku nne tunafanya kwa vigezo. Serikali wafanye, wananchi wasifanye tunaambiwa marufuku Kamati ya Ulinzi na Usalama imeamua sasa wanaofanya nani? Mhe. Spika, linasikitisha sana hili.

Kuhusu bandari kufanya kazi masaa; 24 hili suala alifikirie, mbuzi anakula majani kutokana na kamba yake. Sasa msongamano wa meli zile zilizokaa muda mrefu pale mpaka saa 12 kuja kufunga gati zikawa zinapishana, kwa nini zifanye kazi

masaa 24 kama suala la ulinzi na usalama. Mimi sifikirii, mtu anayetaka kufanya lake kuna njia nyingi za mitego ya panya za kupita. Hii Kamati ya Ulinzi na Usalama ikae ikalifikirie suala, tunahitaji mapato sisi Serikali. Lakini mapato sisi tunayavujisha wenyewe kwa kisingizio cha Kamati ya Ulinzi na Usalama.

Ipo haja kama wenzetu tusome. Wenzetu wanafanya kazi masaa 24 Mombasa pale, na benki zimo ndani lakini ukahoji hakuna muelekeo. Dar es Salaam, mimi Kamati ya Bunge nimeuliza tu ulipaji wa pesa na kulipa nje baadae kukubaliana siku ya pili wakafungua benki ndani CRDB na NMB.

Mhe. Spika, nije katika Idara ya UUB; niwapongeze sana na hii karibu mara ya pili kabla ya bajeti kutaka kusomwa utakuta zile njia zote wanazitia viraka viraka, ni jambo la kupongezwa, inapunguza ile kasi ya wajumbe kuhoji. Mumepiga hatua, angalau njia za mjini kule mumetia viraka. Lakini hata hiyo njia anayokaa Naibu Waziri rafiki yangu Issa Gavu hairidhishi kule kwenda Fuoni, hali mbaya.

Jengine, hili ombi *special* ndugu yangu Cosmas Mnazimmoja inataka kusaidiwa hasa wagonjwa tunapowateremsha mle ndani na mashimo makubwa na wanaumia. Maradhi aliyokuwa nayo na yale mashimo yaliyokuwemo ndani mle hayaridhishi. Hili niwaombeni sana ndugu zangu wa UUB, vile viraka kawasaidieni wenzetu Wizara ya Afya. Angalau mkazibe kama kesho au keshokutwa, lakini hali hairidhishi kwa wagonjwa pale.

Mhe. Spika, kwa kumalizia nimeliona jambo ambalo kidogo linaendelea kuua, sijui wizara itatuambia chanzo chake nini, maana yake hii ninafikiri malaria haiui zaidi kuliko ajali zinavyotokea hivi sasa ya vyombo. Siku moja karibu ajali mbili, tatu, nne tofauti na malaria, hebu tueleze chanzo chake nini ajali hizi, hata tusiweze kulitibu suala hili?

Mhe. Spika, baada ya hapo nije katika ununuzi wa vifaa vya kuinulia mizigo bandarini. Zabuni kwa ajili ya ununuzi wa *crane* 2, *terminal tractor 2, traillar 2, reach stacker 2, Fork lift 3 na Empty Handler*. Hii kila bajeti ukiangalia huko nyuma utakuta hadithi hii hii. Hata Sherehe za Mapinduzi mwaka uliopita zimetiwa hizi, utekelezaji wake *zero*. Hii ni kuandika ambayo ni rahisi kuliko vitendo. Kuandika utaandika, vitendo havipo. Hili suala limepigiwa kelele Mwenyekiti wangu wa Kamati ndio shahidi na Idara ya Forodha inalia kutokana na vitendea kazi kutokuwepo. Kwa huu wimbo utaandika na bajeti atayejaaliwa kuja mwakani ataikuta hivi hivi hii. Hebu tuambie hiyo *tender* imetangazwa lini kwenye gazeti, kwenye TV, kwenye chombo gani? Hili ndio tatizo kubwa.

Halafu Mhe. Waziri mimi nikuombe sana; nilifikiri Bodi ya Bandari itakusaidia sana, lakini nashangaa Bodi ya Bandari inakuja kutaka hati miliki za minara tena

kwenye vyombo vya habari. Inatangaza hati miliki za minara, baada ya kukusaidia waziri ndani vitendea kazi, ili bandari ikaonekana ya kileo, wanakwambia katika vyombo vya habari wanataka hati miliki za minara.

Bodi ya Bandari hiyo, itakusaidia maendeleo ya ndani mule, pale pale tu bandarini padogo. Huwezi leo mtu anakusikiliza unataka kudai minara, inataka hati miliki miaka na miaka hatujasikia Bodi ya Bandari ikadai hati miliki. Mule ndani maelekezo mia mpaka mia mbili. Mule ndio unamopata kula, watafute njia angalau za kujadili, leo atafute gari moja baada ya mwaka mmoja *crane* nyengine. Lakini tokea nilivyokuja, mimi nimezaliwa shamba, nimekulia shamba, nimesoma shamba, ilipokuja Mapinduzi mpya nilikuja kuiona. Lakini zile kazi tokea siku zile mpaka leo hakuna, zimeongezwa mbili zile nazo zimeshakufa tumeambiwa mpya.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sitounga mkono hoja hii mpaka nipate maelezo, lakini kwa kumalizia niombe tena kwa jicho la huruma UUB katembeleeni Mnazimmoja pale msaidie yale mashimo angalau kuzibwa. Ndugu zetu Wizara ya Afya wana majukumu mengi. Ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, ninakushukuru sana nami naomba nitoe mchango wangu kwa ufupi kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Miundombinu, ili kuweza kutoa maoni yangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwenye Mapato na Matumizi kwenye kitabu chake Mhe. Waziri alituonesha kwamba kazi za kawaida mwaka 2014/2015 wizara iliidhinishiwa bilioni 5.7 hadi April 2015 wizara imepata bilioni 3.7 sawa sawa na asilimia 65. Lakini kazi za maendeleo mwaka 2014/2015 wizara iliidhinishiwa bilioni 8.4, lakini halisi hadi mwezi April ni 6.02 sawa sawa na asilimia 72.

Mhe. Spika, kwenye makusanyo hasa Idara ya Leseni wizara ilikadiriwa kukusanya milioni 426 lakini mwezi wa April, imekusanya milioni 315.3 sawa sawa na asilimia 74. Kwa ujumla hoja yangu hapa ni kwamba mapato ya wizara kwa maana ya kazi za kawaida na kazi za maendeleo yameingia kwa wastani ambao unaridhisha. Niipongeze wizara hasa Wizara ya Fedha kwamba kwa wizara hii mapato ya wizara yameingizwa kwa wastani mzuri kidogo, maana ni zaidi ya asilimia 65.

Lakini kwenye Idara ya Leseni kuna mapato ambayo yamekusanywa mwaka jana 2014/2015 makadirio ni milioni 426, lakini mapato 315, lakini mara hii Mhe. Waziri anatwambia Idara hii anakusudia kukusanya bilioni 1.712.

Sasa atuelimishe tu kidogo kutoka milioni 364 mwaka jana mpaka milioni 1.2 ni juhudi gani au vigezo gani ambavyo anakusudia kuviweka, ili kupanda mapato mara tatu mwaka jana. shoot

Mhe. Spika, hii ndio hoja yangu Mhe. Waziri atufahamishe mwaka jana walikadiria kukusanya milioni 364 kwenye Idara ya Leseni, lakini mara hii wame-*shoot* mpaka bilioni 1.2. Sasa atusaidie tu ni juhudi gani ambazo anazichukua ili kufikia hatua hiyo.

Mhe. Spika, hoja yangu ya pili kwenye hotuba hii kuanzia ukurasa wa 4 Idara ya Anga. Miradi ya Sekta ya Usafiri wa Anga Mhe. Waziri ametueleza hapa kwenye kitabu chake ukurasa wa 4 kwamba mradi huu ulikuwa na lengo la kujenga maegesho ya njia ya kupitia ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Zanzibar na umekamilika mwezi Disemba 2014 na kufunguliwa rasmi mwezi Januari, 2015.

Mhe. Spika, mimi niipongeze wizara hasa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa kukamilisha ujenzi huu kwa wakati na hadi pale analipofungua Januari, 2015. Lakini wizara imekiri kwamba ujenzi wa jengo la abiria *Terminal II* ni jengo ambalo lina historia ndefu. Muda mrefu wawakilishi na wananchi wamekuwa wakilalamika na hadi leo Serikali inakiri kwamba imefikia asilimia 32 ya hatua ya ujenzi. Jambo ambalo limekaa zaidi ya miaka 4, sasa hadi hii leo Serikali imefikia asilimia 32 ya ujenzi wa jengo lile.

Waheshimiwa Wajumbe jengo hili tulisahau, limepitia historia ndefu, fedha nyingi ya walipa kodi imekwenda tena ni kwa njia ya mkopo. Jengo hili limekuwa na changamoto nyingi kusema kweli, lakini majibu ya Serikali yamekuwa ya siri mno, hakuna uwazi uliokusudiwa. Hadi hii leo Mhe. Spika, waziri anakiri hapa kwamba jengo lile limefikia asilimia 32. Kwa hivyo asilimia 32 maana yake kwamba jengo hili halimaliziki katika awamu hii ya Dr. Shein miaka 5 na maana yake jengo hili litakamilika pengine awamu ijayo. Kuchelewa si hoja kubwa, hoja ni kiasi gani jengo hili limegharimu. Fedha nyingi za walipa kodi. Kwa kweli Wazanzibari wamekopa ili kujenga jengo hili na mikopo ni mikubwa sana, fedha nyingi na hadi hii leo mradi huu unasua sua.

Nina imani wale wote waliosababisha matatizo madogo madogo, makubwa, basi angalau wangechukuliwa hatua za kuonywa, ili wengine wakajifunza na miradi ile ambayo inakusudia kuleta maslahi kwa wananchi.

Mhe. Spika, ukurasa wa 5 ninaona hapa *paragraph* ya juu kwamba kwa mradi huu Serikali imekiri hapa kwamba kwa mwaka 2014/2015 mradi huu ulipangiwa jumla ya shilingi bilioni 1.95 na hadi kufikia mwezi Machi, 2015 jumla ya bilioni 2.797

kama asilimia 145 zimepatikana. Wizara imekiri hapa kwamba wamekata vifungu vyengine, wamekata kwenye mifuko mengine ili kufidia ujenzi wa jengo la abiria la uwanja wa ndege. Hii nini maana yake, maana yake hii kwamba idara nyengine miradi mengine imekula hasara kwa sababu ya kufidia makosa ya watu wengine. Mhe. Spika, kwa kweli si jambo zuri lazima Serikali ijifanyie tathmini ili pesa ambazo zimekatwa katika maeneo mengine maana yake idara nyengine zimeumia. Maana yake miradi mengine imekufa kwa sababu ya kufidia makosa, pengine yaliyofanywa kwa sababu tu ya kutokuwa makini kwa watendaji wetu au kwa Serikali kwa ujumla.

Mhe. Spika, hata hivyo ninamshauri Mhe. Waziri kwamba makosa haya ambayo yametendeka tujifunze na Serikali itathmini na miradi mengine ambayo itapatikana kwenye wizara mbali mbali, basi iwe ni funzo kwa miradi hii. Hatuwezi kuwatia wananchi katika madeni makubwa kwa makosa ya watu wachache, lazima makosa ya watu wachache yazingatiwe, yarekebishwe na yachukuliwe hatua, ili wananchi waendelee kupata maslahi na wasiongezewe madeni.

Jana bajeti ya Muungano nadhani ilisema waziwazi kwamba kila Mtanzania ana deni la laki nane na kidogo. Bajeti ya Wizara ya Fedha kesho ikija hapa nitaeleza mimi Mzanzibari ana deni la shilingi ngapi kila mtu. Makosa haya madogo madogo ambayo yanasababishwa na watu wachache kwa ajili ya kutia hasara taifa. Mimi nimuombe Mhe. Waziri, niiombe Serikali kwamba kwa kweli ijifunze na iendelee kutusaidia wananchi wanyonge, ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Spika, ukurasa wa 5 huo huo Mradi wa Uimarishaji, Kiwanja cha Ndege Pemba, humu ilivyoandikwa kwamba mradi huu wa uwekaji taa umeanza. Mimi nimefika juzi kutoka Pemba lakini bahati mbaya nimejaribu sana kuangalia zile taa zilizowekwa sijaziona, nimeona vitaa vile pale chini vya sampuli moja rangi ya pinki sijui manjano hivi na kimoja ni blue zimewekwa kama sampuli.

Sasa mimi nikawauliza wale wenzangu, sasa huu ndio mradi umeanza au ndio sampuli watu watoe maoni yao au vipi. Sasa unapoandika kwamba mradi umeanza misingi inachimbwa na taa zinatengenezwa sisi hatujaona pale uwanja wa ndege kiasi hicho lakini labda Mhe. Waziri atueleze, imeanzia upande gani na ni kampuni gani ambayo tayari iko kwenye *field* ambayo inafanya kazi hii.

Mhe. Spika, lakini uwanja wa ndege wa Pemba kuna wafanyakazi pale ambao waliajiriwa kwa *daily paid* kwa mkataba wa miezi sita sita; wafanyakazi hawa wamefanya kazi huu ni mwaka wa 7 inasemekana na hapa Mhe. Waziri atusaidie kwamba hivi sasa wamekusudia kuajiri wafanyakazi wapya na wanaletwa wafanyakazi wengine wapya nje ya hawa 13 ambao wameajiriwa mwaka huu wa 7 kwa *daily paid*. Sasa unawachukua watu miaka 7 kwa mkataba wa miezi sita sita,

halafu unaamua kuajiri wafanyakazi wapya, huwazingatii wale ambao wamepata mafunzo pale chini ya usimamizi, wengine hawa ni wafanyakazi wa VIP, wengine hawa ni wafanyakazi wa *security*, wengine hawa ni wafanyakazi wa mabondeni. Mimi ushauri wangu ni kwamba wale ambao mumeajiri kwa *daily paid* Mhe. Spika nadhani mungewachukua wale wale badala ya kuleta wengine kwa sababu hawa tayari mumewachukua, mumewaamini na kwa kweli wana mafunzo mazuri ya kufanya kazi katika Viwanja vya Ndege. Hivyo kuwaleta watu wengine kwa kazi zile zile ambapo kwa uwezo ule ule wa kielimu nadhani haitokuwa mnafanya jambo la busara.

Mhe. Spika, ukurasa wa 7, Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Ole/Kengeja, kifungu cha 35 serikali imekiri hapa kwamba tayari hatua mbali mbali zinachukuliwa kwa kilomita 11 kwa hatua ya upimaji, na kilomita 5 tu ndio wametia kifusi kwa hatua ya kwanza. Lakusikitisha na Mhe. Waziri amekiri hapa kwamba mradi huu ulitengewa milioni 500,000,000 lakini hadi leo hakuna shilingi iliyoingia, maana yake nini?

Maana yake yale maneno ya wawakilishi mwaka jana namfahamu Mhe. Mohammed Haji Khalid wa Jimbo la Mtambile alisema hatutegemei mradi huu kumalizika 2015, kwa dalili hizi za fedha kutoingizwa maana yake mradi huu unaenda mpaka 2020.

Mhe. Spika, wawakilishi wa Pemba wanaposema kwamba miundombinu Pemba inadharauliwa isionekane wanakusudia kubagua, hawakusudii kubagua lakini serikali imekiri hapa kwamba milioni 500,000,000 tu za Mradi ule wa Barabara hadi hii leo zimeshindikana. Na mimi nimekuwa mstari wa mbele kuzifuatilia na unapowafata wale wahandisi wanakueleza mengi juu ya mradi huo.

Mhe. Spika, hatuoni mwanga kwenye Mradi huu wa Ole/Kengeja nadhani serikali sasa ikubali kwamba iongeze nguvu kwenye mradi huu na maneno haya ya kupanga panga ya kutia tamaa nadhani sio wakati wake, mutueleze maneno ya msingi ya kushika ili serikali na wananchi waweze kujengeana imani juu ya miradi mbali mbali.

Mhe. Spika, lakini niombe tu mradi huu kwa vyovyote utaelekea Mwambe kwenda kupata kifusi, watu wa Mwambe hawakatai kuchimbwa kifusi kwa ajili ya kujenga miundombinu, lakini pale ambapo mtachimba kifusi kwa mara nyengine basi nawashauri kwamba muendelee kufikiria jinsi ya kufukia maeneo ambayo yataathirika kwa ajili ya kuchimba kifusi.

Mhe. Spika, ukurasa wa 9 Idara ya Usafiri na Leseni mimi niwapongeze kwa jinsi ambavyo wametoa leseni za magari na leseni za madereva. Lakini niungane na

hoja ile ya Mhe. Jaku kwamba ukiangalia takwimu za ajali Zanzibar zinaongezeka siku hadi siku, na hii kuna sababu zake nyingi. Sababu moja ninavyojua ni kwamba serikali imepuuza ile sheria ya adhabu ya papo kwa papo, polisi wamekuwa na msongamano wa kesi nyingi za madereva na ni kwa sababu tu hawana ile kanuni haijakamilika ya adhabu ya papo kwa papo. Nadhani hili Mhe. Waziri atukubalie kama tatizo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, basi sheria ile ya adhabu ya papo kwa papo ingekamilika, ili kuwapunguzia mzigo polisi pale wanapokamata kesi ambazo zinahitaji kutolewa maamuzi ya papo kwa papo. Kufanya hivyo pia ni kuondosha rushwa ambazo hazina msingi wowote.

Mhe. Spika, serikali imekuja na sheria hapa ya sera ya hifadhi ya barabara kwamba ziko taratibu za kuhifadhi barabara, lakini ajali nyengine zinachangiwa na sisi wenyewe viongozi kwa matakwa yetu, kwa tamaa zetu.

Mhe. Spika, barabara ya Mlandege kuelekea Malindi kwenye *corner* ya barabara ile limewekwa kontena, na kontena lile liko sambamba na sheli limekuwa likisababisha ajali. Hoja yangu mimi hapa na hapa namuomba Mhe. Waziri anieleze vizuri ni nani aliyetoa kibali cha kuweka kontena kwenye kona ya barabara ile jambo ambalo ni hifadhi ya barabara, si utaratibu wa usafiri barabarani, si utaratibu wa usalama barabarani.

Kontena liko chini ya barabara kwenye *corner* jambo ambalo ni kosa kitaratibu za usafiri barabarani na limewekwa, sera ya ile hifadhi ya barabara ipo, sheria zipo lakini kontena limewekwa chini ya barabara. Kwa hivyo, hoja yangu Mhe. Waziri hapa aniambie ni nani aliyeruhusu kuweka kontena kwenye barabara ile ya Mlandege kuelekea Malindi. Ni barabara ambayo kwa kweli iko kwenye *corner* na kontena liko chini ya barabara ile.

Mhe. Spika, Shirika la Bandari ukurasa wa 12; mimi niendelee kuwapongeza kwamba licha ya changamoto mbali mbali ambazo wanazipata lakini kwa kweli wamekuwa wakifanya kazi kubwa mno. Mimi nadhani wawakilishi tuwe tayari sasa kuiomba serikali badala ya kutegemea fedha ya Shirika la Bandari ya makusanyo ya bandari. Nadhani serikali ikubali kuwapa kibali bandari kukopa fedha katika mabenki yetu, ili kuimarisha bandari zetu. Kwa sababu inaonekana kwamba bandari wanatoa huduma nyingi nzuri, lakini fedha kutoka ndani ya shirika ni chache mno kulingana na mahitaji ya bandari.

Kwa hiyo, serikali kupitia Wizara ya Fedha ikubali sasa kutoka kibali kwa Shirika letu la Bandari kukopa fedha nyingi ili wazalishe, walipe deni na waongeze mapato kwenye serikali vyenginevyo tunaweza kuwalaumu tu. Kwa *nature* ya bandari, bandari inahitaji fedha nyingi, bandari haiwekezi kwa fedha ya kikapu lazima fedha ipatikane nyingi ili waweze kuwekeza. Nimuombe Mhe. Waziri ajenge hoja

serikalini, ili bandari wakopeshwe na wanakopesheka ili bandari ipate fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ya bandari. Haya malalamiko ya ma-*creen*, malalamiko ya makontena, malalamiko ya chelezo yaweze kuondoka haraka ikiwa bandari watapatiwa fedha kwa ajili ya kuwekeza katika maeneo mbali mbali.

Mhe. Spika, wizara hii imefunga taa barabarani, taa ziko Malindi, Mkunazini, Mombasa, lakini taa zile zinategemea jua tu siku ambayo kuna mawingu basi taa haziwaki. Sasa dunia ya leo uombe Mungu kila siku litoke jua ikinyesha mvua inakuwa hatari. Nadhani Mhe. Spika, mimi nina wasi wasi kwamba hakuna mshauri mwelekezi wa ndani wakati wa uwekaji wa taa zile, nina wasi wasi kwamba bado tumekuwa tukiwaachia wataalamu wa nje kutufanyia mambo yetu.

Mambo haya lazima kuwe na mwelekezi wa ndani, mshauri wa ndani ili aweze kutusaidia kitaalamu, kwa sababu ukipita pale baada ya nusu saa mataa yanazimika, hujui kwa nini. Sasa kama hatukuwashirikisha wataalamu wa ndani kuweka taa zile hasara yake ndio hii. Mradi ukiondoka ule maana yake sasa nchi inaingia hasara, jambo ambalo sio malengo ya serikali.

Mhe. Spika, mimi nishauri kabisa kwamba wataalamu wa ndani wasidharauliwe wapewe kipaumbele na wao ndio pekee watakaoweza kutusaidia mwelekeo wa maslahi ya miradi mbali mbali ya serikali.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Spika, mimi nishukuru sana serikali, muungwana akishindwa na jambo husema na mimi naishukuru serikali kwa hili, kwamba kwa miaka karibu 15 serikali imeshindwa kujenga barabara ya Mgagadu/Kiwani kilomita 7.4. Leo imeelekea serikali imeshindwa sasa imetwambia kwamba serikali imeshindwa kujenga barabara ile ya Mgagadu/Kiwani. Nimekuwa nikisema mara zote kwamba barabara ile isiingizwe fedha kwa kisingizio cha barabara kumbe ni mgongo wa watu kula fedha.

Halafu serikali ninavyoona huku kwamba barabara ile imewashinda, si jambo zuri kwamba mtu akishindwa na kazi husema nimeshindwa. Kwa hiyo, kwa miaka hii 50 ya Mapinduzi Zanzibar barabara ya kilomita 7.4 ya Kiwani imeshindikana. Ni hatua nzuri ya serikali kukiri kwamba wameshindwa kujenga barabara ile na watu wa Kiwani watakueleweni kwamba mumeshindwa, na *inshaallah* mukiingia mwakani baada ya uchaguzi pengine atakuja waziri au serikali ambayo itasaidia kujenga barabara ile ya kilomita 7.4

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu hayo niseme tu kwamba nahitaji maelezo kwenye maeneo ya barabara ya *corner* ya Mlandege kuelekea Malindi nani aliyeweka kontena ambalo linasababisha ajali. Na pia nipate maelezo ya kwa nini mataa ya kwenye *traffic light* pale Kwamchina, Mkunazini na Malindi yamekuwa yakizimika bila ya kiwango ambacho kwa dhana yangu nadhani wataalamu wa ndani hawakushirikishwa na hatimae madhara yanaendelea kuongezeka.

La mwisho kabisa niisisitize serikali hasa Wizara ya Miundombinu ijenge hoja kwamba bandari iwawezeshe kukopeshwa mtaji mkubwa wa fedha, ili wajenge miundombinu ya bandari Unguja na Pemba. Mhe. Spika, baada ya hoja hizo naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kama ilivyo kawaida na leo tuna vijana ambao wamekuja kwa ajili ya kujifunza shughuli zetu hapa na kuona namna zinavyoendelea. Wageni wetu wa leo ni wageni wa Mhe. Hamza Hassan Juma ambao wamekuja hapa kwa ajili ya kujifunza. Wageni hao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mafunzo ya Amali kilichoko kwa Mtipura, jumla yao wako 38 wakiongozwa na walimu wao wawili Mwalimu Abdulkarim Gharib Khalfan na Mwalimu Ibrahim Hamad Ibrahim, naomba wageni hao wote pamoja na walimu wao wasimame ili kusalimiana na Waheshimiwa Wajumbe. (*Makofi*)

Ile ni timu ya Mhe. Hamza Hassan Juma iliyoko Kwamtipura *Vocational Centre* ambao wanajifunza mambo mbali mbali mengine ameyataja hapa. Niyataje lakini hiyo sasa itabidi aende kwenye redio, ili kutangaza wapate mapato kule, maana ni mambo mengi. Lakini kuna chuo hapa ambacho wajumbe mnaweza mkaenda mkasikiliza mambo yaliyoko huko. Karibuni sana. (*Makofi*)

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunivumilia, Gavu keshaniroga…

Mhe. Spika: Iko sawa hiyo sasa.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia machache kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano…

Mhe. Spika: Endelea.

Mhe. Viwe Khamis Hamad: *(Hapa hakutumia kipaza sauti)* ...ya vyema ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Spika, nianze na mchango wangu kwenye Shirika la Bandari Zanzibar. Shirika hili linasimamia meli zote za usafiri ambazo zinachukua abiria wanaokwenda Dar es Salaam na Pemba. Ni kwamba kuna matatizo ya uuzwaji wa tiketi, uuzwaji huu wa tiketi kama unataka tiketi unakwenda Pemba Jumamosi uende ukakute tiketi Jumatano, lakini ikipita siku hiyo ya Jumatano tiketi hizi zinaanza kuwa hazipatikani.

Mhe. Spika, utakapokwenda pale siku ya Ijumaa utazikuta tiketi zinauzwa kwa bei ya juu zaidi zimo mikononi mwa watu, lakini ukienda kwa wahusika wanaouza tiketi hizi wanakwambia zimemaliza. Kwa hiyo, tiketi hizi za mikononi unazikutia kwa watu wanaouza tiketi hizi.

Mhe. Spika, hili ni tatizo mwananchi ameshajipanga mwenyewe ana kiasi fulani cha fedha juu ya tiketi ile, leo unakwenda pale unamwambia tiketi ya mkononi shilingi 23,000. Mhe. Spika, niiombe wizara inayoshughulikia mambo haya ya uuzwaji wa tiketi wasimamie vyema uuzwaji huu wa tiketi na hasa tatizo hili linakuwepo wakati wa Disemba, wakati wa kufungwa skuli sasa skuli zinafunguliwa wanafunzi wanarudi majumbani kwao au wanarudi shuleni basi hili linakuwa ni tatizo kabisa.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye barabara inayojengwa kutoka Ole mpaka Kengeja. Barabara hii tayari imeshaanza kufanya kazi na tayari barabara hii imeshaanza kufanya kazi takriban inatimia kama mwaka mmoja au miezi sita kama sikosei. Mheshimiwa kuna baadhi ya wananchi wanaokaa kwenye maeneo haya ambao nyumba zao zilipita maeneo haya ya barabara lakini matokeo yake wanaambiwa kama wao hawamo kwenye hesabu ya watu watakaolipwa fidia kutokana na vitu vyao vilivyoharibika na nyumba zao.

Kuna mwananchi anakaa Ole Kiziwamaji mwananchi huyu barabara imepita chini ya nyumba yake, na nyumba hiyo hivi karibu imeanguka lakini waliokuwa wanapita wanakusanya taarifa za ukusanyaji kwa wale waliokuwepo karibu kwenye maeneo ya barabara yeye aliambiwa hayumo. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri afuatilie kwa kina kuhusu mwananchi huyu ili kuepusha malalamiko ambayo yeye mwenyewe analalamika. Mwananchi huyu ni mnyonge, hana msaidizi, hata mume hana angalau kama atamjengea kibanda cha mgongo. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri hili alifuatilie.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii niipongeze serikali kwa kusimamia vyema barabara ambazo zilichukua muda mrefu zikawa hazijatengenezwa, barabara inayotoka Wete/Gando, barabara inayotoka Wete/Konde barabara hizi zilichukua muda mrefu lakini barabara hizi sasa hivi zimetengenezwa, barabara hizi ni nzuri kabisa katika Mkoa uliokuwa una barabara nzuri ni Mkoa wa Kaskazini Pemba. Barabara

inayotoka Mzambarauni inayokwenda Kinyasini mpaka Mapofu, barabara hizi ni barabara nzuri na niwapongeze sana wakandarasi ambao walikabidhiwa ujenzi huu wa barabara.

Mhe. Spika, yote hiyo ni kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi, pamoja na kwamba tunasema Wapemba tumetupwa lakini sisi tunaona maendeleo yako na yataendelea kuweko, kukosekana kujengwa bandari ya Wete yote hiyo ni mipango ya serikali na ninaamini serikali yetu iko makini na bandari ya Wete itajengwa.

Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Waziri bandari hii ya Wete au Shirika hili la Bandari waisimamie, ili vijana wetu waweze kufaidika na bandari hii ambayo itajengwa kwenye mji wao. Vijana wetu wengi wanakaa hawana ajira wanasumbuka matokeo yake wanajiingiza kwenye madawa ya kulevya. Mhe. Waziri nimuombe pamoja na serikali hili alifuatilie kwa kina ili tujue usumbufu huu utamaliza lini.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niende kwenye miundombinu ya mawasiliano. Kwa kipindi kikubwa tulikuwa tuna huduma ya *ZANTEL*. Sisi Wazanzibari wengi tulikuwa tunatumia mtandao huu wa lakini cha kusikitisha sasa hivi ni kwamba wamekuwa na usumbufu mkubwa sana na tunasikia kwamba mradi huu umeshauzwa kwenye Kampuni ya *Tigo*. Kwa hivyo, kuna usumbufu mkubwa tunaoupata wananchi tunaotumia mtandao huu, unaingiza pesa yako sasa hivi shilingi 5,000 pesa ile hujaitumia unalala ukiamka asubuhi wameshaichukua. Hili ni tatizo.

Jengine unapigiwa simu hupatikani hata ukija ukipatikana unaambiwa kwamba simu yako ilikuwa umeizima wakati simu ile iko wazi. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa aje atwambie ni sababu gani zinazosababisha mpaka mtandao huu ukafikia usumbufu huu walionao.

Mhe. Spika, pia nina masikitiko makubwa, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alibahatika kufungua Msikiti mkubwa sana katika kijiji cha Kiuyu Minungwini, Mkadini. Mhe. Rais alipokwenda pale wananchi wa kijiji kile waliomba huduma ya barabara na umeme kutokana na usumbufu wanaoupata. Namshukuru kwanza waziri anayeshughulika na nishati ya umeme baada ya kutoa ahadi ile, Mhe. Rais nilimfuata na ahadi ile aliitekeleza. Lakini mpaka leo hii kuna ahadi ambayo ilitolewa wananchi wale waliomba kutengenezewa barabara, barabara yenyewe ya kiwango cha fusi tu, kutoka skuli ya Minungwini mpaka Kiuyu Mkadini.

Mhe. Spika, ahadi ile mpaka leo haijatekelezwa na wananchi wale wanaendelea kupata usumbufu, nimeshamfuata Afisa Mdhamini Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Naibu Waziri wa wizara hii nimemwambia zaidi ya mara tatu na

yeye alinambia kwamba atalifuatilia, lakini mpaka leo tupo hapa tunapitisha bajeti hii huu ni mwaka wa pili bado ahadi ile ya Mhe. Rais ambayo aliyoiweka na watendaji wa wizara walikuwepo na kuweka ahadi kwamba wataitekeleza bado iko vile vile haijaulizwa na mtu hata mmoja.

Namuomba Mhe. Waziri aje anambie ni lini ahadi ile ambayo wanakijiji wale waliomba itatekelezwa. Hii ni ahadi ya Mhe. Rais na Rais anapotoa maagizo watendaji huwa wanatekeleza.

Mhe. Spika, mwisho kabisa kwa niaba ya vijana wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naunga mkono bajeti hii kwa asilimia 80, asilimia 20 naweka mpaka Mhe. Waziri atakapokuja kunipatia jawabu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha siku ya leo tukawa hai siku ya Mrisho hii na tukaweza kutoka katika maeneo yetu hadi hapa. Hii ni hadhina kubwa aliyotujaalia *Allah* na kwa vyovyote hatuna budi kumshukuru.

Mhe. Spika, nadhani sitatenda haki kwamba sikufanya mambo yafuatayo kabla ya mchango wangu huu. Kwanza kabisa ni kukuomba radhi kutokana na kuchelewa kuingia katika hili jengo, hii ni kutokana na jana nililazimika kulala sehemu za Kusini, Kajengwa katika shughuli hizi za kujitayarisha na mambo ya Mrisho. Kwa hivyo, nakuomba radhi sana katika hili.

Pili, ni kukushukuru kwa kunipatia hii fursa ya kuweza kueleza machache kuhusu hii hoja iliyopo mbele yetu. Mimi huwa nasikiliza sana michango ya Mabunge haya ya *Common Wealth*, Mabunge mengi tu huwa nasikiliza michango yake hasa michango ya akinamama. Kwa kweli siku za nyuma nilikuwa sipendezwi hata kidogo na *performance* ya *contribution* ya akinamama katika Baraza la Wawakilishi, lakini kwa sasa kama kuna Bunge lenye akinamama wanaopaswa kupongezwa sana ni akinamama wa Baraza la Wawakilishi kwa jinsi wanavyochangia vyema. *(Makofi)*

Mimi kwa sababu ndio hatua zangu za mwisho mwisho katika kusema maneno kwenye hili jengo, naomba kwa hili niwapongeze sana kinamama jinsi walivyobadilika, yaani nimeangalia yale Mabunge mengine kwa kweli wamebadilika sana wanawashinda hata lile Bunge la Kenya nimeliangalia hivi juzi tu nimeona *performance* yenu nzuri, nimeangalia Mabunge yale ya *Monarchy*, hata katika lile Bunge wanaloliita *Majlis-ash-Shura* wamo kinamama mule mmewashinda kwa kuchangia.

Kwa hivyo, nasema katika hili nimpongeze Mwenyekiti wa UWAWAZA kwa kweli amejitahidi sana, hayupo lakini naomba sana Mhe. Spika, atakapokuja umpe salamu zake.

Mhe. Spika, nianze sasa na mchango wangu kwa Shirika la Bandari. Kama kuna shirika muhimu sana kwa nchi za visiwa kama Zanzibar basi ni Shirika la Bandari ni shirika muhimu sana kwa nchi za visiwa na linahitaji umakini na umahiri katika uendeshaji wake.

Mhe. Spika, Shirika la Bandari limekuwa likihudumia kwa mujibu wa tulivyoelezwa katika kitabu hiki, limekuwa likihudumia meli pamoja na wananchi tena wananchi wakaazi pamoja na wageni. Kwa vile hii ni *interest gate* ya nchi ni sehemu ya lango la kuingilia katika nchi, kwa vile ni uso wa nchi, hivyo bandari inatakiwa iwe safi sana katika utendaji, iwe safi katika uendeshaji ili watakapokuja wageni waone kwamba Zanzibar inaingilika.

Haitakuwa vizuri kama anakuja mgeni kuangalia asubuhi uso umejaa utavu au tongo, samahani kama hizi lugha itakuwa zinachosha, lakini uso siku zote unatakiwa uwe safi sana ili uweze kucheka na wageni pamoja na wenyeji.

Mhe. Spika, kwanza katika hili kwa bandari ya Zanzibar napenda sana niipongeze serikali pamoja na Mhe. Said Salum Bakhresa. Mfanyabiashara yule ni wa kupongezwa sana kwa sababu juzi tu hapa amekuja Rais wa Ujerumani na hakuamua kuja kwa ndege aliamua kuja kwa boti, tena Rais wa G7 nchi kubwa hizi aliamua kuja kwa boti. Sasa alipofika bandarini pale alifikia katika *jet* ya Ndugu Said Salum Bakhresa, *jet* iliyokuwa safi sana, tangu anafika pale kutua tu kaingia katika *jet* hiyo kuanzia alipoteremka kwenye boti yake hakupata jua wala mvua mpaka *VIP*, jamani dogo ilo? Kwa kweli amejitahidi sana Ndugu Said Bakhressa kwa hili naomba tumpongeze.*(Makofi)*

Mhe. Spika, hivi ndio nchi inavyotakiwa iwe, lakini nimeangalia upande mwengine wa nchi yaani katika kile kisiwa cha Pemba nikaangalia bandari yake, hapo sasa. Kama yule Rais wa Ujerumani angeamua kwenda Pemba ingekuwa tatizo kubwa kwa kutumia boti mana hakuna bandari kuna tuta sasa Rais huyo tungempeleka tutani ingekuwaje. Tangu ambapo angeteremka pale Bandari ya Mkoani Rais yule angepigwa na jua na mvua mpaka kwenye gari yake jamani sio aibu kwa nchi hii? Si aibu kwa Pemba ni aibu kwa nchi hii.

Mhe. Spika, hili ni tatizo Pemba ni sehemu ya Zanzibar na wageni wanaweza kuamua kuja aidha Unguja au kwenda Pemba kwa kutumia hiyo hiyo meli au boti. Mimi binafsi siku moja niliwahi kufanya mazungumzo na Ndugu Said Salum Bakhresa pale bandarini *VIP* akanambia amejaribu kuwaeleza serikali kama

anataka kufanya kitu kama alichokifanya pale Unguja, vile vile akifanye kule Pemba. Sasa mazungumzo yale bado yapo na kama serikali haiwezi basi kwa nini haimruhusu tena Bakhresa akaweza kufanya kitu kile, alisema yeye kama atapewa Mkoani au Wesha, au atapewa Wete atafanya. Je, mazungumzo yale yapo au hayapo tena ya mfanyabiashara huyo?

Mhe. Spika, Ndugu Said Salum Bakhresa mimi namsifu sana katika hili kwa sababu mkono wake hakuufunga. Mimi siku moja nilikuwa nina shida ya banda la skuli katika skuli ya Jeshi nikamtumia Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, nampongeza sana akaonana na Ndugu Bakhresa wakanipatia banda moja kule katika skuli ya Jeshi alipokuwa Waziri wa Ulinzi akamuita pale wakazungumza nikapatiwa banda kule lime-*cost* karibu shilingi 40 milioni.

Sasa mimi naamini ikiwa kasaidia kijiji je, akashindwe kusaidia bandari kujengwa kama vile alivyojenga Unguja? Kwa nini asipewe jamani kama kweli anataka au kama anataka hapewi basi wao serikali wajenge kama vile Unguja kutoka kwenye tuta lile mpaka wafike juu watujengee sehemu na watuwekee viti vya *VIP*, watuwekee viti vya kukaa watu wa kawaida kama hawawezi apewe yeye japo kwa kutumia ile *private partnership* tuliyopitisha juzi humu, ule mswada Mhe. Spika wewe unaujua *Public Private Partnership (PPP)* tulipitisha juzi, yeye apate katika bandari hiyo na nyinyi mpate, huyo Bakhressa mpeni na sisi tuwe na bandari kule Pemba.

Mhe. Spika, hiyo ni sehemu ya Shirika la Bandari, sasa tuangalie katika usafiri huu wa bahari. Usafiri wa bahari ndio *only affordable transport in the island*. Sasa nimepata kauli hapa kwamba kuna tetezi kuwa unataka kupandishwa bei usafiri huu, kama *first class* sasa itakuwa shilingi 50,000 ukitaka kuingia kwenye ile meli ya mbio *Royal*, unatakiwa ulipe shilingi 6,000 ya kodi hee, hiyo meli ya serikali na ije bwana, tatizo tutashindwa 50,000 nusu ya laki. Mkulima wa Vitongoji kule au mvuvi ende akamudu kusafiri, tutarudia mashua tutaendelea kufa kwenye mashua.

Mimi naona ni tatizo, hebu tafuteni mahala pengine pa kutafuta mapato serikali sio katika suala hili la usafiri, kwa sababu sisi ni visiwa huku tuko na kule tuko. Mtumbatu yuko Tumbatu yuko Mwambe, haya atakwenda kuangalia jamaa zake Mwambe shilingi 50,000 azipate wapi Mtumbatu huyo, au Mmakunduchi Kajengwa kule ana ndugu yake Chake Chake kila baada ya mwaka anataka aende akamuangalie na kupata baadhi ya mambo kule, atasafiri vipi huyo kwa shilingi 50,000.

Mimi nadhani tu-*review* bei za vyombo hivi serikali iingilie na iwateremshie ushuru hawa watu wa vyombo vya bahari kwa sababu ni tatizo ikiwa sasa unataka kwenda tiketi ya baharini shilingi 50,000 tutatengeneza gharawa na mashua

tuendelee kufa humo baharini. Mhe. Spika, hii itakuwa ni tatizo kwa sababu kuna wengine wana wake watatu, wana wake wanne na wengine wako kisiwa hiki, wengine wako kisiwa kile kule watakwenda vipi zamu watu hao? Ni tatizo kubwa sana Mhe. Waziri katika hili la bei za vyombo lidhibitiwe hasa hivi vya *private*, naamini wakishateremshiwa kodi na wao watateremsha moja kwa moja bei za tiketi.

Mhe. Spika, sasa nielekee katika huo huo usafiri baharini. Meli tuliyonayo sasa hivi ni Maendeleo ndio inayofanya kazi, hiyo *Royal* ni muda mdogo mdogo tu. Maendeleo imeshakuwa inahitaji *major repair* tukifanya mchezo tutakuja kulia sana.

Mimi nahisi sasa hivi Meli ya Maendeleo izuwiwe hasa inatumia masaa 13 au 14 siku nyengine baina ya Unguja na Pemba. Watu wameshasema humu, leo tunasema, kesho tutasema kwamba Maendeleo sasa inahitaji kufanyiwa matengenezo makubwa, huku inafanyiwa matengenezo na huku meli yetu iletwe haraka na hii boti ya MV. Sepideh jamani wanavunjwa moyo wawekezaji.

Mhe. Hamza Hassan Juma kasema hapa kwamba mwekezaji katumia *one billion shillings* kwa ajili ya kutaka kuleta *service* na ile boti ina kifua sio kama hizi ndogo ndogo, kwa mkondo wa Nungwi tu haishindwi inasaidia sana usafiri baina ya Pemba na Unguja, leo inazuwiwa kwa nini?

Kama kuna mambo ya kudaiana basi wadaiane huko lakini huku awe anafanya kazi yule kijana. Mimi nadhani kama ni hilo tunataka tuione kesho iko baharini hii. Mhe. Waziri atumie busara zake, mimi naamini ana busara sana na serikali hii ina busara na inasikia maneno tunayoyasema sijui kuyatekeleza tu, lakini kwa kuyasikia wanayasikia vizuri. Kwa sababu tunayasema vizuri tunayapanga hasa maneno katika kuyasema. Kwa hivyo, nadhani katika hili waliangalie sana la boti ya Sepideh.

Mhe. Spika, sasa niende katika usafiri wa nchi kavu, kama kuna usafiri muhimu sana katika nchi hii, ni usafiri wa nchi kavu. Kwa mfano hapa Unguja tuna kiwanja kimoja tu cha ndege. Kwa hivyo, mtu hawezi kutoka Makunduchi akaenda Tumbatu kwa ndege kwa sababu Makunduchi hakuna Uwanja wala Tumbatu hakuna uwanja. Kwa hivyo, hulazimika kupanda gari tafauti na nchi nyengine kwa mfano unaondoka Dar-es Salaam unakwenda Mwanza kwa ndege, unaondoka Mwanza kwa ndege unakwenda Arusha kwa ndege ni tofauti, sie tunatumia gari tu katika nchi hii ndani ya visiwa hivi.

Sasa Mhe. Spika, usafiri wa nchi kavu ni moja katika usafiri muhimu. Kwa hivyo, barabara zinatakiwa ziwe na umakini mkubwa. Leo hivi sasa kuna barabara ya Ole

- Kengeja na hii ni moja katika barabara muhimu sana na inayoweza kuinua uchumi wa nchi hii, kwa sababu inaunganisha watu wa Mashariki wa Kisiwa kizima cha Pemba pamoja na kisiwa cha Unguja, kwa sababu ukimtoa huko Micheweni unakuja nae mpaka sehemu za Mtambile huku, halafu unamuunganisha na Bandari ya Mkoani pale anaenda zake.

Kwa hivyo, mambo yanayozaliwa huku kama Ole, Mtama ambayo yana afya sana mnaweza mkatumia hapa Unguja ndani ya mwezi huu wa Ramadhani. Lakini barabara kila siku tunaambiwa hivyo hivyo, nashangaa sana kila siku barabara ile. Sasa sie huku Kusini Pemba tumekosa nini barabara zote mnazotuletea sie ni za kusizima hamtuletei makampuni yale makubwa makubwa ya kujenga barabara kama *H-young* haya mambo kama Kojifa mnawapelekea Kaskazini tu. Sie wengine mkituletea barabara ni ile ya kusizima kwa mkono hivi kama nyumba ya kienyeji, tushachoka na barabara ya *sample* zile.

Tatizo jengine barabara ile ya Ole Kengeja majumba ya watu wameshateketezwa wala hajalipwa fidia, juzi kuna *bulldozer* katika kukata muembe liliingia muembe likainamia nyumba tatu, zote zikavunjika pale Ole. Haya sasa Mhe. Waziri matatizo haya kwa nini watu waliofanyiwa tathmini hawajalipwa fidia hadi leo hii. Wale watu wote waliofanyiwa tathmini katika nyumba zao kama zitavunjwa hadi leo hajalipwa fidia ni kwa sababu gani.

Mimi nafikiri kutafika siku mtasema sie hatutaki maendeleo, lakini tutakuja kukaa barabarani watu kuanzia Ole pale mpaka Kengeja, hapana ruhusa ya kujenga mpaka tulipwe fidia mkisema hatutaki maendeleo basi tutakuwa hatuyataki. Kwa hapo sie mnatudanganya tu siku zote mtalipa wala hamlipi. Hivi karibu hata huyu Mhe. Naibu Waziri anafahamu kwamba mlikata miti, Wizara ya Mawasiliano ndio matatizo yenu haya nyie mlikata miti yetu, mimea yetu na mashamba mkayakoroga mkapeleka umeme Mawasiliano kule. Watu mpaka sasa hawajalipwa, yaani sisi tumekatiwa miembe mtu muembe mmoja kwa mwaka unazaa mara mbili na kila mzao wa muembe mmoja tu boribo ana-*collect* laki tatu, mizao miwili laki sita. Kwa masikini ya Mungu ni pesa nyingi kwa muembe mmoja hizo.

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mwenyezi Mungu akipenda tukijaaliwa nataka zitoshe hizo hizo.

Sasa Mhe. Spika, tatizo lililopo ni kwamba Wizara ya Mawasiliano ni dhuluma munatudhulumu kwa sababu mumetukatia mimea yetu, huu ni mwaka wa pili hamjatulipa. Mwisho waziri aliepita wa Mawasiliano imekatwa miembe akasema kuwa hakujakatwa miembe kule kumekutwa Mibuyu na Mivumo. Tangu lini

Vitongoji mibuyu, aje aangalie mibuyu na mivumo, ile ni miembe. Sasa katika hili la barabara mkija mkisema hatutaki tutakaa barabarani kuandamana mpaka tulipwe fidia zetu. Sasa kwa mara ya mwisho mwisho tena nasema katika chombo hiki.

Mhe. Spika, niende katika Idara ya Usafiri na Leseni nimalize na naona muda hauko. Sasa niende Pemba airport. Nimeona kuna ule mpango wa kuiboresha Pemba airport, napenda kusema kwamba ule mpango uwe endelevu, usigande. Isiwe kwamba kumeshapigwa misingi tena ikawa ile misingi taa zikatiwa mwaka wa kwanza, taa zitatiwa mwaka wa pili, mtupe *specific time, project* hii itaanza lini mpaka lini.

Mhe. Spika, pale Pemba kuna vijana wanafanyishwa kazi *temporary;* lakini huu karibu mwaka wa sita wale vijana wako pale wanafanyakazi za usafi, kazi za bustani lakini wanapewa mikataba ya miezi mitatu, mitatu, wameshakaa mwaka wa sita sijui sheria za Utumishi Serikalini zinasemaje. Mtu kumtumikisha miaka sita bila ya kumpa mkataba wa kudumu, wapo vijana wale 13 pale, wakiwemo wamama, wakiwemo na vijana wa kiume. Hii ni kuwadhulumu. Wapeni mikataba.

Hivi sasa kumeshatangazwa ajira pale, sidhani kama watachukuliwa wao wakati kila siku wanaambiwa kwamba tukiajiri hapa tutawaajiri nyie, ajira zinapita na wao hawaajiriwi. Je, Mhe. Waziri vijana hawa kumi na tatu ambao mwaka wa sita wanafanyakazi pale mnawapa mikataba feki hii. Je, mtawaajiri wao au mtawatafuta wengine kuwaajiri. Mie naomba muwaajiri, hawa ni wazalendo, wanafanyakazi sana wale vijana.

Mwisho nimalizie na Idara ya Usafiri wa nchi kavu na leseni. Idara hii ni muhimu sana. Kwa sababu idara hii kama haikuwa makini huwenda tukamalizika humu kwa kuwapa leseni vijana ambao hawastahiki. Sasa mimi naomba kitu kimoja hivi sasa watu wa daladala wanalipa *road license*, wanalipa mambo haya ya lesini zao alimradi ukifanya *collection* ya kodi wanazotoa ni karibu laki tatu kwa daladala. Lakini sasa tatizo lililopo hawa wanalipa kodi kwa mwaka, lakini wanafanyakazi nusu mwaka tu, kwa sababu siku wanatoka siku hawatoki.

La kwanza Mimi naomba tuwaangalie hawa kwa sababu kazi zenyewe siku hizi zinajulikana, ili angalau wakatwe nusu mwaka baada ya kulipishwa kodi mwaka mzima.

La pili, usafiri wa barabarani unakumbwa na vikwazo kwa hii miti mibovu mibovu, iliojengwa kwa lengo la kuzuia mmomonyoko. Lakini kuna miti imekuwa mikongwe sana mle barabarani huwa inaanguka siku nyengine inaweza ikaathiri, hata abiria inaweza ikaathiri hata watu wanaopita na vipando vidogo vidogo, ile miti iliyo pembezoni ambayo ni mikongwe ikatwe.

Mimi siku moja nimeshawahi kuona karibu na msafara wa kiongozi unapita muembe mkubwa unaanguka, haya isingekuwa tatizo. Mungu bariki yule kiongozi wetu alikuwa keshapita. Sasa naomba sana hili lifanyiwe kazi.

Halafu hawa daladala wanalipa kodi ya maegesho, kila siku utoe elfu pale. Lakini hebu angalia maegesho Pemba katika mji wa Chake Chake, hakuna maegesho, matokeo yake magari yanagongana. Mimi juzi moja nilipita hapo hapo ndio maegesho barabarani mpaka sasa mkono unaniuma huu kwa kupigwa na *site mirror* na daladala, mambo haya mpaka lini.

Mnajenga mambo yaliokuwa hayana umuhimu, mambo ya maegesho hamfanyi, kwa mfano hapa Unguja Pale CCM, wakati Rais wetu Chama chake kiko pale Kisiwandui ndio maegesho hapo hapo, watu wanataka kwenda kuomba kura wapite pale pale huku madaladala. Tatizo mnajenga mnara pale ule mnara utatusaidia nini baada ya lile eneo lingeekwa kituo cha daladala ikawa watu wanalipa kodi.

Mhe. Spika, nataka aje anambie Mhe. Waziri ule mnara kwa mwaka utawatilia kiasi gani, ambapo pale mngejenga kituo cha daladala watu wa daladala wangelipa kwa mwaka zaidi ya bilioni.

Mhe. Spika, mwisho nikushukuru kabisa na nakutakia mwisho mwema. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kuchukuwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambae ametujaalia uhai tukaweza kukutana hapa katika Baraza lako tukufu na kuendelea na utaratibu wa kazi zetu.

Mhe. Spika, pia nichukuwe fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi ili niweze kusema machache katika Hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, kwa mwaka wa Fedha 2015/16.

Mhe. Spika, kabla sijaanza kuingia katika mchango wangu naomba uniruhusu niseme lile ambalo leo lilinikera katika nafsi yangu. Mhe. Spika, wakati anachangia Mhe. Hamza Hassan Juma kitendo alichokifanya leo nilihisi kimetudhalilisha wanawake. Kumsema mwanamke katika chombo kikubwa kama hiki kwa hali ya kumdhalilisha, si kitendo kizuri. Maneno yale bora tungekuwa tunaambizana wenyewe tu hivi nje. Kwa sababu ahisi Mhe. Hamza Hassan Juma mwanamke yeyote ni mama, kwa hiyo na yeye amezaliwa na mama. Kwa hiyo, maneno mengine haifai kusema mahala kama hapa.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo napenda nichukuwe fursa hii na mimi kuanza kutoa mchango wangu.

Kwanza kabisa nianze kwa kuipongeza wizara hii, nimpongeze mwenyewe Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote ambao wanahusika katika wizara hii kwa kazi kubwa na ngumu kabisa ambayo wanapambana nayo wizara hii.

Mheshimiwa wizara hii ni kubwa na kweli changamoto ambazo zinaikumba si kama inajitakia, isipokuwa hii wizara miradi yake yote ni mikubwa ambayo inahitaji fedha nyingi sana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa tuone basi changamoto ambazo inaipata hii wizara si kama inajitakia, hakuna mradi hata mmoja katika wizara hii unaoendeshwa kwa fedha ndogo. Kwa hivyo, fedha ni nyingi kabisa na tuone wenzetu wanajitahidi na tuwapongeze kwa pale ambapo jitihada inaonekana imefanyika.

Mhe. Spika, mimi nianze mchango wangu katika miundombinu ya viwanja vya ndege. Kwanza nichukuwe fursa hii na mimi kumpa pole Mkurugenzi wetu huyu ambaye amepata matatizo ya ugonjwa na *inshaallah* Mwenyezi Mungu amjalie kile la kheri na azidi kumpa afya njema.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Rais wa Zanzibar ambae amekusudia kuufanya Uwanja wa Ndege huu ambao unaonekana umepata sifa ya kupewa jina la kuwa ni kiwanja cha kimataifa. Kwa kweli kupitia Mkurugenzi huyu ambae amechaguliwa katika sehemu ile, kweli inaonekana sifa hiyo inakwenda na kulingana na hali halisi.

Mhe. Spika, nichukuwe fursa hii basi nayo kumpongeza sana Mkurugenzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ambae mwezetu huyu ameonekana jitihada yake kubwa na mtakuwa mashahidi hapo nyuma kabla ya kuwa hatukuelewa nini anachotaka kukifanya Mkurugenzi, alikuwa akilaumiwa na Baraza hili hili. Lakini sasa ule muelekeo umeonekana, kumbe mwenzetu huyu alikuwa anapigania mambo ya pale yaende vizuri. Kwa hiyo, na mimi nachukuwa fursa hii kumpongeza. Kweli uwanja wetu unastahiki kila sifa, unaonekana tayari ni mzuri unapendeza na *inshaallah* kila lile ambalo limepangwa kufanywa basi liweze kufanyika.

Mhe. Spika, niombe kupitia Mkurugenzi huyu serikali inapokuwa na ujezi au matengenezo ya jambo lolote katika uwanja ule ni vizuri tukachukuwa hatua ya kumshirikisha na yeye mwenyewe Mkurugenzi kwa sababu yeye mwenyewe ndie

mwenye nyumba ambayo anaishi na kwa kuwa huyu mtu ni mzoefu, basi inaonekana anajua mambo mengi na yeye kupitia viwanja hivi vya ndege.

Tutakapomshirikisha maana yake tutaweza na sisi kupata ujuzi ambao na yeye ana ufahamu na kwa kuwa nyumba inayojengwa pale ni ya kwake si vyema basi akaambiwa wewe kaa kando na subiri uje ukabidhiwe tu kiwanja, na yeye apate fursa ya kutoa mawazo kama ulivyo usemi wa kiswahili mjenzi na mjengewa. Sio wewe ujengewe japo fundi anapeleka ukuta upande wewe basi unaangalia tu, hapana unatakiwa na wewe utoe mawazo wako.

Kwa hiyo, niombe huyu mkurugenzi ashirikishwe panapokuwa na matengenezo yoyote au ujenzi wowote katika kiwanja kile cha ndege, ili tupate mawazo yake yachanganyike na yale ya wengine, ili tuweze kupata kitu kizuri katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu huu niende katika Miundombinu ya Bandari. Kwa kweli pia nichukuwe fursa hii kumpongeza Mkurugezi wa Shirika hili la Bandari na yeye analingana na yule wa Uwanja wa Ndege kwa jitihada kubwa anazozichukuwa na kuzifanya. Nataka nitoe yale ambayo tumeona katika kupitia kitabu chake hiki. Kwanza katika matengenezo ya sakafu, eneo la kuhifadhi makontena bandarini Malindi. Hapa kulikuwa na changamoto kubwa ya kuhamisha makontena yale, lakini wakakaa shirika na kaona iko haja ya kuvunja yale mabanda pale na wamevunja na wametumia milioni mia nne katika kujenga ule uwanja pale, na sasa makontena yamepata kupungua, kwani yalikuwa yakihangaika huku na huku. Sasa wana nafasi nzuri ambayo wanaweka makontena yale.

Pia shirika hili limetengeneza minara minane Unguja na Pemba; minara hii inakuwa ni ya kuongozea meli. Kwa kweli Mheshimiwa hiki ni kitendo kizuri ambacho kitazifanya meli zetu ziweze kwenda vizuri zikiwa zinaongozwa bila ya kupotea njia. Hili ni jambo la faraja na la kupongezwa. Pia nimpongeze Mkurugenzi huyu kwa ununuzi wa *tag* mpya. Hili ni jambo zuri na linamufaa.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu huu hili hili Shirika la Bandari katika mpango wake wa ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Kwa kweli lengo la pale ni zuri na tuombe kheri na fanaka itokezee pale ili ile bandari iweze kujengwa. Hapa serikali itajiongezea mapato hata na vijana wetu wataendelea kupata ajira.

Pia nasisitiza kwa ule ujenzi wa Bandari ya Mkokotoni ambao unaonekana harakati harakati zake zimeanza na niseme bado Shirika hili liendeleze ujenzi ule wa Bandari ile ya Mkokotoni, kwa sababu inaonekana Bandari ile imekuwa kwa kasi na inamahitaji mengi.

Pia niombe kupatikane basi vile vitu ambavyo vinahitajika viwepo katika bandari zetu au katika viwanja vyetu vya ndege. Lazima katika Bandari pawe na kituo cha Afya, lakini hata kile cha kilimo ambacho saa nyengine kunahitajika pale karantini mbali mbali, kunakoharibika mazao pahala pale inatakuwa wao wawepo waweze kukagua, waone kile kinachoingizwa katika nchi yao kiko salama. Kwa hivyo, Mheshimiwa hata na mgonjwa inapotokea *emergency* yoyote pale basi anaweza akatibiwa kama pale kipo kituo cha afya. Kwa hiyo, nasisitiza mambo haya yawepo katika bandari zetu.

Mhe. Spika, pia katika Shirika la Bandari kuna mamlaka ile ya *ZMA*. Kitengo hiki nacho kinajitahidi kwa kadiri ya uwezo wake. Lakini niseme bado kitengo hiki hakijaweza kusimama kwa miguu yake miwili, bado ni kichanga. Kwa hiyo, niombe sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu pale huwa kinashughulika na mambo ya maafa na hawa na wao huwa waokozi katika kitengo chao hiki wao ni waokozi wakubwa ambao wanahusika na mambo ya uokozi. Basi pale inapopatikana misaada katika Ofisi hii ya Makamu wa Pili waweze na wao kupatiwa kama vile vifaa vya kuokolea, vile wapewe na wao.

Pia naomba wangepatiwa boti kwa sababu inapotokea hitilafu yoyote wanapigiwa wao simu. Lakini hawana kitu hata kimoja cha kuendea, wangepatiwa boti ya kisasa moja angalau linapotokezea tatizo wakaweza kukimbilia katika hilo tukio. Lakini leo wao ndio waokozi lakini hawana zana hata moja.

Kwa hiyo, hili naomba waweze na wao kupatia boti ili inapotokea tatizo lolote waweze kukimbilia. Lakini pia hili boti wangepatiwa wangeweza kufanya doria na pengine wangeweza ku-*save* hizo ajali nyengine zinazotaka kutokea. Lakini pia ile doria ingewasaidia kwa sababu kuna vyombo ambavyo vinatembea vyombo vidogo vidogo hivi bila ya usajili. Kwa hivyo, wao wangeweza kuwakamata wale ambao wanakwepa kusajili katika vyombo vyao hivi na kuikosesha Serikali mapato.

Mhe. Spika, niende katika programu hii ya huduma za usafiri wa barabara. Pia, hapa nitoe pongezi zangu za dhati kwa sababu kunaonekana zile barabara tatu zimeweza kukamilika na ilikuwa ni kilio cha muda mrefu, lakini kwa kuwa tumeweza kukamilisha na kama nilivyoanza kutangulia kusema mradi huu changamoto yake ni fedha na fedha nyenyewe inakuwa ni nyingi kabisa. Kwa hivyo, kwa kukamilika barabara hizi basi mimi nitoe pongezi na niombe zile nyengine ambazo bado zipo katika utata wa kukamilika, basi ziweze kukamilika.

Lakini hapa kuna changamoto ambayo hata katika ripoti yetu basi ilielezewa kwamba hawa wanakumbana na changamoto ya kuweza kulipa, saa zote wao wapo katika ulipaji wa madeni na wanashindwa kutekeleza ile bajeti yao ambayo

wanakabiliana nayo kwa mwaka ule. Hivyo, niiombe Serikali iweze kulidhibiti hili la madeni na wao wawaachie watekeleze bajeti yao kama ilivyo.

Mhe. Spika, lakini pia Idara hii kuna na Idara ile ya Leseni ambayo mimi ningeliiomba iendelee kuweka usimamizi mzuri wa magari yetu haya hasa kwa kuzingatia zile ruti za magari, mule zilimokupangiwa kufika basi ziweze kufika na hasa ruti ile ambayo inatakiwa gari za daladala zikageuza kule Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hili mimi ninaliomba sana kwa sababu wenzetu wanapata shida sana, tuseme kuna mgonjwa ndani ya daladala ukimshusha tu Darajani au ukimshusha Kisiwandui halafu ukawa hukumfikisha kule, kwa kweli lazima roho zetu na sisi zijenge imani ya kuona tunasaidia wananchi wetu, penye kazi zetu na ndipo zilipo sawabu zetu hapo hapo.

Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi niiombe Idara hii kushughulikia na yule ambaye atakuwa hataki kufikisha gari yake kule, basi hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa ili watu wetu wapate unafuu. Unamshusha mjamzito Darajani anakuja Hospitali ya Mnazi Mmoja *clinic* au pengine ana matatizo mengine. Mhe. Spika, lazima hili tulifikirie kwa nguvu zetu zote.

Mhe. Spika, niipongeze sana Serikali katika ununuzi wa meli mpya ya Mapinduzi II ambao Mhe. Waziri, alipokuwa anasoma hotuba yake ametwambia itawasili hapa mwisho wa mwezi wa saba. Kwa hivyo, hii ni hatua nzuri kwa Serikali ambayo itaweza kuwasaidia wananchi wetu meli na hii ndiyo meli ya wanyonge, maboti saa nyengine bei kubwa, lakini katika Serikali huwa kuna unafuu fulani wa kuwapunguzia mahitaji wananchi wake. Hivyo, niombe ombi langu katika Shirika hili la Meli kwamba itakapofika hii meli basi tuhakikishe meli hii inapakia abiria kulingana na tani ya uwezo wake iliopangiwa ili tuweze kuitunza meli hii ichukue muda mrefu, lakini pia kudhibiti uuzwaji wa zile tiketi holela za mikononi ambazo zinafanya kuwanyongesha wananchi wetu.

Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi niiombe meli hii ijipange vizuri ili itakapowasili meli hii tuweze kuwaondoshea usumbufu wananchi wetu. Kwanza kuuza tiketi zile za mkononi kuna hasara yake Mhe. Spika. Kununua tiketi mkononi ambayo hukwenda wewe kushiriki katika kile kibanda chenyewe cha uuzwaji wa tiketi, inapotokea tatizo ndipo unapoona sasa. Kwa sababu kipindi kile walichozama wale wenzetu na si jambo la kuomba Mwenyezi Mungu atunusuru lisitokee tena, lakini mtu ambaye atanunua tiketi mkononi, maana yake hatajulikana katika ile ajali ambayo imetokea.

Sasa ununuzi huu tuupige vita ili tuchukue abiria ambao tutakuwa tunawajua na kunapotokea chochote itakuwa inajulikana fulani alikuwepo mahali fulani. Kwa sababu pale kuna kompyuta, unarikodiwa kila kitu lakini ukiuziwa tiketi mkononi

maana yake imeandikwa kwa jina la mtu mwengine. Hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa naomba lizingatiwe sana sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Unazo dakika tano.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante zinatosha, kwani na mimi nimeshamalizia.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii kuipongeza tena sana Serikali kwa kazi kubwa na nzuri inayoifanya kuhakikisha wananchi wake inawapatia mahitaji mbali mbali.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo mimi nichukue fursa hii kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na nichukue fursa hii kuwashawishi wenzangu wote kuona wanaiunga mkono hotuba hii, kwa sababu hotuba hii kama tunavyojua ndiyo mkombozi wetu, bila ya barabara basi maendeleo yanakosekana, bila ya kupatikana bandari, maana yake watu watakuwa hawasafiri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, niombe waunge mkono ili bajeti hii ipite na huduma hizo muhimu ziweze kupatikana kwa wananchi. Mhe. Spika, ninakushukuru sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Mlinde Mabrouk Juma, afuate Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na baadae Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma: Mhe. Spika, ninakushukuru na mimi siku ya leo kupata nafasi hii kuchangia mchango wangu mdogo tu.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi nipo hapa hasa kuwashukuru sana Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano na lazima niwapongeze, hasa ukizingatia kwamba Wajumbe wenzangu waliotangulia kwenye chombo hichi tangu linaanzishwa Baraza hili Tukufu, walikuwa wana lugha moja tu wakipigania barabara ya Bumbwini kutengenezwa, tangu Baraza la Kwanza.(*Makofi*)

Leo hii mimi nimesimama hapa ninajivunjia mafanikio ambayo sasa tunayo, barabara nzuri tumejengewa. Hivi sasa Mhe. Spika, hata kule kulikokuwa kuna matatizo ya kuwafikia wananchi wetu, yaani ninakusudi yale maeneo ya Kiongwe, sasa unatelea, kifusi tayari kimeshatandazwa na ujenzi unaendelea. Kwa hivyo, tunawashukuru sisi wananchi wa Jimbo la Bumbwini kwa Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano kwa ujenzi ambao unaendelea.(*Makofi*)

Mhe. Spika, lakini pia ninapenda niwashukuru tena kwa sababu Jimbo la Bumbwini tulikuwa tuna tatizo la daraja hasa la mto Zingwezingwe. Daraja hili

katika kipindi hichi limejengwa na wananchi sasa wanalitumia. Hivyo, niwaombe tu kwa vile kifusi kinapatikana kule kule Bumbwini, basi ili kuweza kufika kwenye daraja tunahitaji kutengenezewa ile barabara, kuwekea japo kile kifusi kwa sababu wananchi wa maeneo Zingwezingwe na hasa wanaotoka maeneo ya Mahonda kuja Bumbwini wanapata usumbufu mkubwa kupitia katika njia ile.

Mhe. Spika, jambo jengine ninalotaka kusema kuwa tumekuwa na matatizo makubwa katika mji wetu hasa hapa Mjini kwenye suala la vituo vya daladala. Vituo ambavyo vimeanzishwa sijui kama niseme vya muda ama vya kudumu, lakini ni dhahiri kwamba kumekuwa na mtihani mkubwa hasa wakati wanafunzi na wananchi wengi wanaporudi majumbani wakati wa jioni. Leo ukipita pale Makao Makuu ya CCM, yaani kama una usafiri wako unaona bora utafute njia nyengine upite lakini pale huwezi kupita.

Sasa mimi nimeona kuna eneo hapa Mjini, niishauri Serikali ifikirie na iangalie kwa makini kama upo uwezekano na niiombe Serikali eneo liliopo Baraza la Wawakilishi la zamani kupitia mbele ya *Karume House* hadi kijumbe kile barabara ya Maisara, eneo lile viwanja vya mpira vimekufa na panajaa maji ya bahari. Niiombe Serikali basi ifanye maarifa yoyote ili pale paweze kutumika kama kituo cha daladala. Kwa sababu hakuna nchi ambayo haina kituo cha daladala mjini. Sasa sisi kuendelea na vituo hivi ambavyo vipo pembezoni pembezoni vinahatarisha maisha ya watu na hasa wanafunzi. Kwa hivyo, niiombe Serikali kupitia Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano ipaangalie mahala pale, kama upo uwezekano tuweze kupatiwa kituo kile.

Mhe. Spika, jambo jengine barabara nyingi Zanzibar; Unguja na Pemba zipo nzuri zinapitika muda wote, lakini kumejitokeza barabara za hapa Mjini hasa maeneo ya Mwanakwerekwe kuwa ni barabara mbovu sana, pamoja na jitihada zote ambazo zimechukuliwa, niwaombe Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano maeneo yale wayafikirie kwa muda mfupi sana. Kwa sababu kumekuwa kukitokea ajali za mara kwa mara, pamekuwa sasa hapapitiki Mwanakwerekwe kuanzia Polisi hadi *roundabout* na hata pale ambapo maji yalikuwa yamejaa kwenye lile bwawa, sasa hivi imekuwa pia ni tatizo. Kwa hivyo, niiombe sana Wizara hii katika mipango yake ambayo inaendelea nayo, basi mashimo yale wangeyafikiria ili wananchi wakaweza kupita kama ilivyokuwa zamani.

Jengine nishukuru tu kuona mipango mizuri ambayo wameiweka Wizara hii hasa barabara yetu hii inayoelekea Kaskazini, barabara hii imekuwa ni kadhia kubwa inayotoka Bububu kuelekea Mkokotoni kupitia Chaani. Lakini nimeona katika maelezo humu kwamba mambo yamo katika matayarisho. Kwa hivyo, niombe tu hiyo *speed* iongezwe ili tuweze wananchi wa Kaskazini na sisi tuweze kutelea kama wale wenzetu wa Kusini na baadhi ya maeneo ya Pemba. Kwa sababu sasa

hivi nimekwenda kutembea Mtambwe hivi karibuni, nimeshangaa ile Mtambwe ambayo ninayoikumbuka na hii ambayo ninayoiona leo. Kwa hivyo, niishukuru sana Serikali kupitia Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano kwa jinsi ilivyoweza kutandika barabara nzuri na kwa upana wake kwa sisi Zanzibar haujawa tatizo, sababu hatujawa na magari mengi na makubwa kuwa hatuwezi kupishana, tunapishana vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa hivyo, mimi mchango wangu ulikuwa ni huo mdogo tu wa kuwashukuru wa Wizara hii, lakini pia kuwaomba katika eneo lile la Bumbwini Makoba kuna gari zetu za abiria sisi zinafika Muembekitorani. Njia ile ambayo inakwenda Muembekitorani kwa kweli imekuwa haipitiki vizuri kutokana na mashimo. Niwaombe basi wakati wanaendelea na ujenzi wa barabara ya Kiongwe na kipande kile cha kutoka Skuli ya Makoba hadi Muembekitorani wakifanyie kazi ili napo tena ule usumbufu na lawama zile za madereva ziweze kuondoka.

Mhe. Spika, ninakushukuru na ninawatakia kila kheri na ninaunga mkono kwa asilimia mia moja Wizara hii. Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Mhe. Mlinde, tunakushukuru. Sasa ni zamu yake ni Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, atafuata baada ya hapo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi hii asubuhi hii ya leo kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, kabla ya kuanza mchango wangu niseme nimpongeze Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake kwa juhudi zao kubwa wanazozifanya kukamilisha kazi zao. Lakini Mhe. Spika, nikianza na mchango wangu, leo kwa kweli niseme kwamba sina mchango mkubwa sana lakini kitu kimoja tu kinachonifanya nichangie na hicho kinaniuma sana tangu mwaka 2005 mpaka leo hii mwaka 2015.

Mhe. Spika, kwanza nianze na gati ya Mkoani. Kuna tatizo kubwa la usafiri katika gati ya Mkoani na tatizo hili hasa kwa abiria wanapotoka katika banda lile na kuelekea katika meli. Tatizo hili zaidi hutokea wakati wa uunyeshaji wa mvua ambao wasafiri wanasafiri kuelekea katika meli. Mvua ile siku nyengine inakuwa kuna watoto wachanga, kuna watoto wadogo, kuna watu wazima na wao, kutoka pale mpaka kuingia kwenye meli mvua tayari inakuwa imeshawarowesha. Hili ninamuomba Mhe. Waziri, aliangalie sana tatizo hili la bandari ya Mkoani ili kufanya utaratibu pale wa kuweza kujenga mabanda ya kuweza kufika na kujifunika mvua wakati mvua na kujenga mabanda hayo kuelekea katika meli.

Mhe. Spika, lakini pia nije katika Kampuni ya *ZANTEL*. Kama walivyotangulia kusema wenzangu kuwa tunazo kampuni zetu hizi za *ZANTEL, TIGO, VODACOM* na nyengine. Lakini simu hasa zaidi ya *ZANTEL* ina matatizo makubwa sana. Wenzangu wameshakwisha kusema hapo na mimi kidogo tu nitatilia mkazo. Ina matatizo makubwa sana hasa wakati wa upigaji wa simu, aidha, unaweza ukasikia sauti yako inajirudia au wakati mwengine unasikia mambo mengine yanazungumzwa katika simu na kikubwa zaidi ulaji wa pesa katika simu hizi. Hili ninamuomba Mhe. Waziri, aliangalie sana.

Mhe. Spika, pia, nikija kwenye ukurasa wa 12 kuhusu Shirika la Bandari. Shirika la Bandari linahudumia meli katika bandari za Unguja na Pemba, pamoja na kuhudumia bandari lakini Shirika hili bado kuna matatizo kwa vijana wetu, wale wanaosimamia katika mlango wa kuingia katika meli hapa Unguja. Pale tunao vijana wetu askari ambao wanawasimamia watu wanaoingia katika meli na kukagua tiketi pale, lakini kuna tatizo kubwa sana ambalo hasa wakati wa mvua na jua, pale hapana sehemu ya kujibaza wale askari wetu, wakati wa jua tuseme kuna usalama lakini wakati mvua je, na wasafiri wale tayari wanaingia kwenda melini, wanakagua watu na mvua zao na tiketi zile hurowa. Sasa ninamuomba Mhe. Waziri, aliangalie sana kulifanyia utaratibu pale wa kujengewa kibanda askari wale ili wanapokagua zile tiketi wakati wa mvua zisiweze kuroa.

Lakini pia Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 11 kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inaendelea kufanya kazi zake za msingi kuziendesha na kusimamia na kuvitunza viwanja vya ndege. Hapa kuna tatizo kubwa sana nalo, lakini cha kusikitisha kimoja kikubwa, wale wafanyakazi wanaohudumia watu pale ambao wanaingia ndani katika kupimwa, kinachoniuma zaidi siyo ile kuwapekua tu lakini kinachouma kile kinachopekuliwa badala ya kukipata ambacho hukiona hakifai kukipitisha pale au kuingia katika ndege, hilo ndilo tatizo kubwa.

Kwa sababu nyengine unaweza kukutia mtu ana *perfume* kwenye mfuko lakini kaisahau kwenye kuitikia katika mzigo mkubwa, lakini mtu yule *perfume* ile ananyang'anywa na akishanyang'anywa hapewi tena na ukamwambia kwamba aah! nipe hii *perfume* alau nina mtu wangu nje niirudishe inakuwa huipati. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri, aliangalie sana hili kuhusu usafiri na wafanyakazi na vitu vyao. Hili ni tatizo kubwa sana. (*Makofi*)

Halafu hapo hapo Mhe. Spika, alitokea Mwarabu mmoja anasafiri akawa ana *perfume* ikabidi *perfume* ile ajikumutie yote mwilini almuradi asiipate tu yule mtu na kuiacha. Hili ni tatizo Mhe. Spika. Naomba Mhe. Waziri, aliangalie sana wakati wa upekuzi ule na abiria na vitu vyao.

Mhe. Spika, pia, nikija katika Idara ya Leseni kwenye Kifungu cha 9. Mhe. Spika, bado hakuna uhakika wa utoaji leseni, sababu ya kusema hivyo, kuna madereva ambao hawajui taratibu zao wala hawajui Sheria za barabarani. Ukitoka barabara ya Mpendae kuingia ndani ambayo inatoka ndani inakuja nje barabara kuu, pale utakutia gari imewekwa karibu na barabara inayotoka ndani. Sasa mtu anayetoka ndani huku haoni gari inayotokea barabara kuu. Sasa pale inabidi husababisha ajali.

Mhe. Spika, na hili namuomba Mhe. Waziri, awaangalie sana watu wanapopewa leseni, waangaliwe kwamba mtu huyu leseni hii kaipasi au leseni hii kaifeli, isiwe mtu anapewa leseni kwa sababu ya kuwa ni jamaa au ndugu, tutasababisha ajali kubwa sana Zanzibar.

Mhe. Spika, nikija katika Mamlaka ya Usafiri ya Baharini. Bado Mamlaka inashindwa kudhibiti utoaji wa tiketi. Hili ni tatizo kubwa na wenzangu wamesema. Juzi tu Mhe. Spika, hapa tiketi moja ilikuwa inauzwa shilingi elfu hamsini na hili ni jambo kubwa sana ambalo kwa meli ya *MV*. Serengeti, meli ilijaa tiketi ukenda unaambiwa shilingi elfu hamsini. Naomba sana Mhe. Waziri, aliangalie hili la utoaji wa tiketi. Tiketi zinauzwa bila ya mpango na hata tuseme ziuzwe kwa mpango, lakini sasa yule anayekwenda akanunua wanabakia nazo kwa kupata faida zao. Hili namuomba Mhe. Waziri, aliangalie sana kwa sababu hii ni hatari na hili ni tatizo kubwa sana.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 18 naomba nisome kidogo;

> "Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Mamlaka ya Usafiri Baharini ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 1.38 na ilikadiria kutumia jumla ya shilingi bilioni 1.36 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Lakini hadi kufikia mwezi wa Machi, 2015 jumla ya bilioni 1.421 zimepatikana."

Mhe. Spika, hapa kwanza niwapongeze kwa kupata fedha hizi. Lakini sitowapongeza nitawauliza je, fedha hizi ni kitu gani ambacho kilitendeka hadi kufikia fedha hizi bilioni 1.421.

Vile vile, Mhe. Spika, katika mwaka 2015/2016, Mamlaka imekadiriwa kukusanya jumla ya bilioni 2.127 na kutumia jumla ya bilioni 2.127 zile zile. Je, Mhe. Waziri, niseme katika mpangilio wao kwa nini makusanyo yasiwe zaidi na katika matumizi yasipunguwe ikawa kuna akiba. Je, hii bilioni 2.127 ni zile zilizopatikana na hizo ndizo zitakazotumika.

Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri, anieleze, kwa nini wasikusanye zaidi na kutumia kidogo. Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 47(d) kuhusu Utoaji wa Leseni kwa madereva. Mhe. Spika, suala hili nimeshalizungumza, lakini kwa Unguja hii (M) sijui wenyewe wamekusudia nini au magari makubwa ni 57 na Pemba ni moja. Vile vile, katika (a) kuna watu 3,555 na leseni (b)(1) kuna 3,641. Pia, kuna magari makubwa ambayo yanaendeshwa ni (c)(1) 302. Haya ninavyofahamu mimi kwa leseni niliyokwenda kuisoma Mhe. Spika, inayosema (b)(1) ni ya watu 7 ambazo ni gari zetu, lakini kuna (c)(1) ambayo ni magari makubwa, wakati mwengine Mhe. Spika, wale wanaokwenda kuchukua leseni pale mtu anapata leseni ya (b)(1), lakini utamkuta anaendesha gari kubwa la (c)(1).

Mhe. Spika, namuomba aniambie Mhe. Waziri, kwa nini akafanya hivi na wakati (b)(1) ni gari la watu 7 na (c)(1) ni magari makubwa, kwa nini (c)(1) aendesha gari ndogo na (b)(1) aendesha gari kubwa, naomba maelezo zaidi.

La mwisho, Mhe. Spika, bado sijamaliza. Kuna ukurasa wa 22 hili ndio kubwa ambalo lililonifanya nichangie, nilikuwa nimeshalisahau katika ukurasa wa 22. Suala hili linaniuma sana, tena sana, tena sio leo. Namuomba Mhe. Waziri, aliyepo sasa, kwa sababu wamepita mawaziri zamani hawajayatekeleza. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri, na hasa katika kitabu hiki sijaiona barabara ya Mkanyageni Kangani, nilisikia imepelekwa katika Wizara ya Kilimo.

Mhe. Spika, sijui Wizara ya Kilimo. Nakwenda katika Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, hili Mhe. Spika, tangu mwaka 2005 naingia katika Baraza nalipigia kelele kuhusu barabara ya Kangani kwenda Kukuu, barabara hiyo ni ndogo na nimejitahidi sana kutia kifusi barabara ile, lakini bado mimi siwezi kujenga barabara. Serikali wakati haiwezi kujenga barabara, na mimi ndio vile vile siwezi kujenga barabara nitasaidia tu. Suala hili namuomba Mhe. Waziri, aliangalie sana barabara ile ni ndogo lakini ina watu wengi ambao wanaishi huko, ambako kuna wazazi na wagonjwa. Kwa hivyo, wakati wa usafiri inakuwa ni tatizo.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri, aliangalie sana, ambapo mwaka 2005 barabara hii iliwekewa mfuko wake shilingi milioni 50,000,000, lakini kwa bahati barabara hii haikutengenezwa sijui sababu ni zipi na mwaka 2010 vile vile iliwekewa pesa, lakini haikutengenezwa. Hebu niambieni Mhe Spika, ni kitu gani ambacho kilisababisha barabara hii hata pesa zote za mfuko huu isiweze kutengenezwa na mpaka hii leo ipelekwe katika Wizara ya Kilimo. Namuomba Mhe. Waziri, suala hili anieleze limeshatutosha, wananchi wa Kangani - Kukuu tumeshachoshwa kuhusu suala hili. Namuomba Mhe. Waziri, akija hapa anieleze.

Mwisho Mhe. Spika, kuna usafiri wa anga ambapo tunapanda ndege zetu hizi tunavikuta viti ambavyo vina *pilot* wawili. Lakini unapopanda kwenye ndege ile

utamkuta *pilot* ni mmoja. Hili ni tatizo kubwa sana kwa sababu wakati mwengine inaweza kutokea ajali na mtu yule ni mmoja au anaweza kuumwa na yuko peke yake akasababisha ajali. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Spika, atupe uhakika wa uendeshaji huu wa ndege. Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsanate sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa kuweza kuchangia mawili au matatu katika wizara yetu hii ya Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, kwanza naomba kusema kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi. Kwa hivyo, mengi tulikwishazungumza katika ripoti yetu ambayo tumeiwasilisha hapo. Vile vile, nikiri kwamba hayo yaliyozungumzwa humu kwa niaba yangu na mjumbe ambaye amekuja kuyasoma hapo nakubaliana nayo kwa asilimia mia kwa mia.

Nikimaliza hapo Mhe. Spika, vile vile, nielekee kutoa shukrani zangu kwako kwa kunipa fursa ya kuchangia. Pia, nitowe shukrani za pekee kwa Mhe. Waziri wa wizara hii, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote, bila ya kusahau kuishukuru Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, watendaji wote pamoja na makatibu wetu, lakini na Katibu wa Baraza letu la Wawakilishi na timu yake ya watendaji, kwa jinsi tulivyoweza kushirikiana ndani ya miaka miwili na nusu, katika kufanyakazi za kamati hii na hatimaye leo tunafikia tamati ya kuwasilisha bajeti ya mwisho katika wizara hii, ambapo kwa mwaka huu tutakuwa tumemaliza. Nawashukuru sana na niwaombe basi binadamu kwa kawaida wakikaa pamoja huwenda ikawa wametokea kukosana.

Kwa hivyo, kwa niaba yangu na kwa niaba ya kamati, niwaombe radhi, Waziri, Naibu Waziri na watendaji wa wizara hii kama kuna tatizo lolote ambalo ilikuwa tumekwazana, itakuwa ni katika juhudi na taratibu za kuhakikisha kwamba wizara inaondoka pale ilipo na kuweza kufikia katika hatua hii ambayo imefikia kwa sasa. Ni imani yangu kwamba kwa mwenye macho hana haja ya kuambiwa tizama, wizara ilipotoka ilijulikana iko wapi na sasa hivi imefikia katika hatua gani. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu ajaalie kila la kheri kwa wizara hii, na *Inshaallah* iwe ni miongoni mwa wizara bora zaidi katika nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, baada ya shukrani hizo sasa nije katika eneo la makontena ya Darajani. Mhe. Spika, jana nilipokuwa nachangia hapa katika bajeti ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo niligusia suala la Hoteli ya Bwawani. Mhe. Waziri, alijibu hapa baadhi ya mambo kuhusiana na hoteli ile, haidhuru kwamba yale majibu niliyapokea, lakini hayakuniridhisha sana, lakini nilikubaliana na yeye.

Mhe. Spika, katika kitu ambacho kinaniumiza roho, hakuna kama ile hali ya yale makontena yaliyokuwepo pale mbele ya Hoteli ya Bwawani. Mhe. Spika, ni muda mrefu tumekuwa tunalizungumza suala la makontena yale pale Darajani, yanaharibu hasa nadharia na sura nzuri ile ya mji wetu wa Zanzibar, lakini bado hatujapata mustakabali wa suala hili, kwani kulikoni? Nakuomba Mhe. Waziri, hebu utakapokuja hapa utusaidie, ni nini mpango wa serikali juu ya suala la kuweka makontena katika eneo lile. Suala hili tulilizungumza katika miaka ya nyuma sana, lakini bado hatujapata ufumbuzi wa suala la yale makontena ambayo yanaharibu haiba ya mji wa Zanzibar pale Darajani.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, niwapongeze sana Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, kwanza kwa uwanja wetu wa ndege ambao sasa hivi tunaelekea kuwa na uwanja wa kimataifa hasa katika nchi yetu ya Zanzibar, mara baada ya uwanja ule kukamilika kujengwa hapo mwishoni mwa mwaka huu au mwanzoni mwa mwaka unaofuata. Ni matumaini yangu kwamba uwanja ule utakapomalizika na mambo yote yakesha, basi Zanzibar itakuwa imejitangaza na Zanzibar itazidi kuimarisha njia zake za kuzidi kukusanya uchumi wake na kujiona kwamba tunakua tunafanya vitu vyetu kwa uwezo ambao Mwenyezi Mungu ametujaalia.

Mhe. Spika, mimi niwapongeze sana Wizara ya Fedha kwa kazi nzuri inayofanywa chini ya usimamizi wa Waziri wa Fedha, katika kuhakikisha kwamba uwanja ule unakamilika na hatimaye unakabidhiwa na huduma kwa wananchi zinapatikana. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atajaalia uwanja ule utakamilika ndani ya mwaka huu na unakabidhiwa na sisi tutaendelea kuutumia kama ambavyo tunaendelea kuutumia sasa hivi.

Jengine Mhe. Spika, katika ukurasa wa 20 nipongeze vile vile Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa maamuzi yake ya kwenda kununua meli ambayo kwa jina tunajaalia itakuwa inaitwa Mapinduzi *II*. Meli hii itakapofika itaondoa tatizo ambalo liko kwa Wazanzibari wenzetu ambao wanapambana nayo, hususan katika kisiwa cha Pemba katika kwenda na kurudi, ndugu zetu hawa ambao wanasafiria meli hizi ndogo ndogo na meli nyengine.

Mhe. Spika, meli hii ni mfano wa meli ya Mapinduzi ambayo tulikuwa nayo zamani na ni imani yangu itakapofika. Nimeiona Mhe. Waziri. Katika ile bahati ya kuweza kwenda Korea na kwenda kuangalia meli hii na kuona utengenezaji wake. Basi Mhe. Rais katika chaguzi zake alituteuwa baadhi yetu mimi na mwenzangu Mhe. Salmin Awadh Salmin, kwenda kuangalia meli hii na tukaiona hasa tulishuhudia kuwa ni meli mpya na ni meli ambayo itakuja kwa namna moja au nyengine kutatua matatizo ambayo kwa sasa tunayo hapa Zanzibar. Nafikiri ulitaka hivyo tu Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo sasa nielekee katika kilio changu cha kawaida. Nilipokuwa nachangia bajeti kuu ya serikali nilimuomba Mhe. Waziri, atupe maelekezo juu ya suala zima la hizi kodi zetu ambazo tunapaswa kulipa kwa haya makampuni ya simu ambayo yako Zanzibar. *ZANTEL* kwa kwetu ambayo ni ya Zanzibar ilikuwa, Bara kule inatakiwa kulipa baadhi ya *charge*, lakini Makampuni ya *TIGO, CELTEL* na mengineyo ambayo yako Zanzibar, hakuna malipo ambayo wanalipa.

Mhe. Spika, maongezi yamepita, hatua mbali mbali zimeendelea. Sasa nakuomba Mhe. Waziri, sio kwa kampuni tu hata wale *TCAA, TCRA* pamoja na Anga. Mhe. Waziri, utakapokuja hapa nataka kujua mmefikia hatua gani juu ya hatima ya kile kiwango cha fedha, ambacho mmekubaliana upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipate katika taasisi hizi za Muungano ambazo zinafanyia shughuli zake hapa Zanzibar. Naomba sana, ikiwemo na posta vile vile. Naomba sana Mhe. Waziri, utakapokuja hapa kwenye bajeti yako hii ya mwisho utujuze taarifa na sisi ili tuweze kujua juu ya suala zima la haya mapato yetu.

Jengine Mhe. Spika, wengi wamezungumzia hapa masuala ya meli hizi Serengeti, kuna Seagull, kuna Maendeleo, kuna meli chungu nzima ambazo zina matatizo ya hapa na pale. Mhe. Spika, mimi nichukuwe fursa hii kuwaomba, kwa sababu kuna wawekezaji wengi sana wenye vilio katika masuala haya ya meli. Ningewaomba basi hebu wizara kaeni na hawa watu wa *ZMA* muweze kuona kuna nini hasa huku, ikabidi kila mtu ambaye ni mdau wa meli analalamika sana na taasisi hii ya *ZMA*. Nawaombeni sana wizara kaeni na *ZMA* kama kuna matatizo yoyote, basi muweze kuyatatua kwa mujibu wa taratibu za kisheria.

Mhe. Spika, Kamati yangu kwa kushirikiana na hao hao *ZMA* baada ya kuona malalamiko yamekuwa mengi hata sisi tumefanya jukumu la kwenda kuziangalia baadhi ya meli, ikiwemo meli ya Mapinduzi, Mwenyezi Mungu aijaalie isipate matatizo haraka. Ikiwemo meli ya Maendeleo tulikwenda kuiangalia na taarifa yake tutai-*submit* kwako Mhe. Waziri. Lakini pia tulikwenda kuiangalia Seagull na tumo harakatini kumalizia suala la Serengeti ambapo bado haujapatikana wakati muafaka wa kwenda kuiangalia hii Serengeti.

Lakini taarifa ya meli hizi ambazo tumezikagua tutawasilisha kwako Mhe. Waziri, ili baadae wizara na *ZMA* muone utaratibu gani unaweza kuchukuliwa na kuona kwamba masuala haya yanafikiwa pahala ambapo yataleta mustakabali mzuri katika kuona kwamba mambo yetu yanakwenda sawa, sio kama hivi ambapo kila mmoja analaumu upande wake. Hiki ni chombo kikubwa na wizara inasimamiwa na watu ambao wana uwezo mzuri, ni weledi na wana muelekeo ambao ni mzuri, ni matumaini yangu baada ya kwisha kuwasilisha ripoti yetu, pamoja na yale mengine ambayo mtakuwa mumeyapata mtatoa mustakabali mzuri juu ya haya

malalamiko ya vyombo mbali mbali ambavyo vinalalamikiwa juu ya taasisi hii ya usajili wa meli za nje. Vile vile, Mhe. Spika, nisemee juu ya suala lile la uwakala wetu ambao uko kule Dubai. Kamati iliomba sana kwa ajili ya kwenda kuona na kufahamu baadhi ya mambo, kuhusiana na suala zima la uwakala wetu wa meli wa masuala haya ya mizigo, ambayo yako kule Dubai, lakini kwa bahati mbaya hatukuweza kufika, lakini kuna taarifa ambazo tumezipata.

Kwa hivyo, ningeomba kamati itakayokuja ambayo itakuja kusimamiwa na viongozi watakaokuwepo hapo baadae, muwape fursa na nafasi ya kuweza kwenda kuliangalia suala hili kwa kina na hatimaye waje kuleta taarifa yenye kuleta mustakabali mzuri, kwa maslahi na maendeleo ya Wazanzibari wote kwa ujumla.

Mhe.Spika, sio siri kwamba wafanyabiashara wetu wa Zanzibar bado wanapambana na matatizo katika suala zima la kuondosha mizigo yao kutoka Bara Arabu na kuleta Zanzibar. Kwa hivyo, ningeomba pamoja na utaratibu mzuri wa hizi meli zinazosajiliwa huko. Vile vile, mtaangalia na uwezekano wa kuweza pengine labda kuziruhusu na meli nyengine ambazo zitakuja kuomba uwezo wa kuja kufanyakazi Zanzibar huku na kuweza kuleta mizigo yao ya *loose* kama ilivyokuwa zamani. Meli za namna hiyo zipo na *Inshaallah* mtakapokuwa mnaitumia vizuri ofisi yenu ya Dubai, basi huwenda na wao wakaweza kupata ruhusa ya kuja Zanzibar na kuleta mizigo hii ambayo itakuwa *loose*.

Baada ya hapo Mhe. Spika, mimi niwapongeze tu Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano, kwa namna ambavyo wanaendelea na utaratibu mzuri wa kuzitandaza hizi barabara katika miji yetu ya Zanzibar. Barabara kusema kweli ni nyingi ambazo zinaendelea kutengenezwa na nyengine ziko katika utaratibu wa kutengenezwa. Lakini na mimi kwa upande wangu niwashukuru sana wizara, kwa kuweza kutuangalia kwa jicho la huruma, hata na sisi wenye barabara hizi ndogo ndogo za ndani, hususan katika Jimbo letu la Kikwajuni. Kuna barabara tatu ambazo tumeweza kujengewa chini ya usimamizi wa wizara hii, na kwa kazi nzuri na makini inayosimamiwa na swahib wangu Al Hajj Mufti Mhe. Issa Haji Gavu, na kuhakikisha kwamba barabara zile zinamalizika na hatimaye wananchi wanafaidika na harakati za kutumia barabara zile katika mustakabali ambao uliomwema.

Mhe. Spika, mimi ningewaomba tu kwamba bado kati ya barabara ambazo nimeziomba, zile tatu au nne zimemalizika, lakini bado kuna nyengine zimebakia kama nne naomba nazo kwa mwaka wa fedha unaokuja tuziangalie na hatimaye tuweze kuzimaliza. Lakini na barabra nyengine ndogo ndogo za majimbo mbali mbali ya Zanzibar kwa ujumla, nazo muziangalie na muhakikishe kwamba zinamalizika.

Mhe. Spika, baada ya maelekezo hayo sasa nina ombi la kipekee. Mhe. Spika, nawaomba sana ndugu zangu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano waiangalie ile barabara ambayo inaelekea Uzi, nafikiri Uzi Ng'ambwa kule kunaitwa. Ile barabara ambayo waliitengeneza wananchi kwa uwezo wao wenyewe na misaada ya hapa na pale, ningeiomba serikali iangalie uwezekano sasa wa kuifanyia marekebisho au matengenezo barabara ile ambayo wananchi wanapata tabu sana, hata ule upitaji wake pia ni matatizo.

Mhe. Spika, baada ya maelekezo hayo, kwa heshima na taathima naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. Lakini hapo hapo namuomba Mhe. Waziri, anipatie majibu ya ziada, juu ya mambo ambayo nilikuwa nahitaji ufafanuzi wa ziada. Ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Ahasante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa mchana huu ya kusema machache sana katika Mpango huu wa Mapado na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, sikuwa na uhakika kama nitapata fursa lakini bahati nzuri kwa hekima zako umenipa fursa na nakushukuru kwa hilo.

Mhe. Spika, kwa ujumla sina mengi isipokuwa kuna machache tu ambayo nimeyaona nikitaka maelezo kidogo, kwanza niwashukuru kwamba Shirika la Meli hadi leo linaiendeleza ile meli yetu ya Maendeleo japokuwa Mapinduzi imeshazama haipo tana, lakini Maendeleo inaendelea hivyo kidogo kidogo na wakati wowote nafikiri itapata msaada, sasa sijui tu utakapokuja msaada huo wa meli mpya haya maendeleo tutayaweka wapi, tutayaweka *skrepa* tuyauze yaondoke tena yasitusumbue kwa sababu uendeshaji wake utakuwa ni mzito au utaendelea kutoa huduma kama kawaida.

Mhe. Spika, nataka niseme kidogo kuhusu hili Shirika la Meli na Uwakala na kidogo nimepata wasi wasi kwamba wao wanatueleza kwamba mwaka 2014/15 wamekusanya bilioni 4.91 na wakatumia bilioni 3.95, lakini mwaka huu wanafanya *projection* ya kukusanya bilioni 13.3 lakini watatumia bilioni 12.308. Sasa nikiangalia waliyoyakusudia mwaka 2014 nayaona ni kidogo, lakini mara hii 2015/16 naona wamekisia pakubwa sana kiasi asilimia 200 za ziada, sasa sijui Shirika lina chanzo chengine cha mapato zaidi ya hichi ambacho kilikuwepo mwaka 2014/15 na labda wamepanga kutumia zaidi katika nini, kwa sababu nahisi hicho watakachokipata kitatumika pakubwa sana.

Nilipoangalia programu ya miundombinu ya huduma za Uwanja wa Ndege na mengineyo nimeona hata huo mchango wa Serikali utakuwa karibu ni bilioni 5.8, sasa ukiangalia bilioni 12 nahisi ni nyingi sana. Sasa sijui hizi Mheshimiwa, amezipanga hasa zitazaliana wapi, kwa sababu hata kama tupate meli mpya kesho, lakini imani yangu ni kwamba abiria labda wataongezeka mara mbili ya wale

ambao walikuwa wanachukuliwa na Meli ya Maendeleo, sasa hizi milioni 13 sijui zitatokana na chanzo gani kiasi kwamba hivi fedha ziwe ni nyingi kiasi hicho na matumizi yake sijui yatatumika vipi, kiasi kwamba tubakishe moja *point* kidogo tu ya pesa za makusanyo ndio bakaa itakayokuwa imebakia.

Sasa ukilinganisha na hiyo meli ambayo pengine inaondoka utakutia labda haiko tofauti na upatikanaji wa hiyo meli mpya makusanyo yake au bakaa yake itakuwa takriban hiyo hiyo, labda Mhe. Waziri, kidogo angenitosha hapa kwa kuniambia hasa hii *twelve point* inataka kutumika hasa katika nini na wao hii wataikusanya kutokana na chanzo gani zaidi ya hii meli ambayo ipo Maendeleo au pengine na hiyo meli mpya itakayokuja.

Lakini Mhe. Spika, tunaijua historia ya Shirika la Meli na kwa ujumla naweza kusema kwamba Shirika hili halina sura nzuri mbele ya watu na tumefikia hatua ya kwamba Serikali inataka kufanya *reform* na kwa taarifa najua kwamba hivi sasa kuna mpango madhubuti wa Serikali wa kuona kwamba Shirika linatakiwa kufanyiwa *reform* ili itakapokuja hiyo meli mpya iweze labda kuhudumiwa vizuri na kuonekana angalau bakaa kidogo imepatikana na inaingia Serikalini.

Lakini karibuni tu Serikali ilipitisha Sheria ya *PPP*, yaani kuruhusu watu binafsi kuingia katika Serikali na kuanza kufanya kazi na Serikali pamoja, sasa leo tunatarajia keshokutwa kupata meli mpya ambayo kwa maoni ya wengi kukabidhiwa kwa Shirika la Meli kama kutakuwa kidogo kuna wasi wasi, sijui Serikali iko tayari wakati itakapofika meli hii kukaribisha wananchi walio tayari kuingia katika mkataba huu *PPP* ili meli isiendeshwe moja kwa moja na Shirika la Meli na kuwapa fursa wananchi na wao wa kuendesha chombo hichi muhimu na kuwa na uhakika labda wa kuwa tutapata mapato kulikoni yale ya kuachia Shirika ya kubahatisha bahatisha. Labda Mhe. Waziri, hebu tueleze kutakuwa na ofa hiyo itakapofika meli kuja Serikalini kuomba kwa vile tumeshapitisha Sheria ya *PPP* kupata fursa na sisi ya kuja kuingia Serikali kuiendesha meli hiyo.

Mhe. Spika, jengine nilikuwa nataka kusema ni kwamba kuhusu hii Mamlaka ya Usafiri baharini, Serikali imeamua kufuta mkataba wa kampuni hii ya *Filtex* ambayo ilikuwepo Dubai, na labda sijui hivi asa kumeshapatikana kampuni nyengine ambayo inaendesha shughuli hiyo au baada ya kufunga kampuni hii tumebakia pale pale tu tunasubiri sijui mpaka lini kupata kampuni nyengine, kwa sababu nahisi ilikuwa kampuni hii inaingiza chochote. Na kuna mapato ayanapatikana yanakwenda katika mamlaka yetu.

Lakini jengine kufunga kwa kampuni bila ya shaka mkataba kufutwa kulikuwa kuna matatizo ni imani yangu, sasa hebu tueleze kidogo je, kampuni hii kwa nini tumeifungia mkataba, kulikuwa na matatizo gani yaliyofikia hata kampuni hii

ikafutiwa mkataba wake, lakini kabla ya kufuta mkataba unajua makampuni na hii ilikuwa nje haikulitia aibu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika muda wake waliofanya kazi pamoja na kampuni hii, sisi hatuna aibu nje ya nchi kwamba labda alifanya mambo fulani yaliyokuwa hayana sura nzuri kwa nchi yetu.

Jengine labda katika kampuni hii hatuna tunachokidai au sisi hakuna anachotudai kwa sababu mkataba umemalizika, umefutwa mkataba wake je, hajenda serikalini na mashirika mbali mbali ya kimataifa kutushtaki kwamba sisi tumekwenda kinyume na utaratibu wa mkataba wetu, yaani tumemalizana kampuni yupo salama na Serikali yetu ipo salama baada ya kufuta mkataba huu. Mhe. Waziri, naomba kidogo utakapokuja utupe maelezo.

Lakini jengine ni kuhusu Idara hii ya Ujenzi na Utunzaji wa barabara unajua kwamba Serikalini kunakuwa na vipaumbele vya kuangalia nini tufanye na barabara ipi tujenge, kinachonishangaza ni kwamba tulianzisha *Tourist labour* kwa maana ya kuona kwamba tunahitaji tuboreshe huduma hasa za mahoteli kwa ajili ya kuvutia zaidi watalii, juzi nilipokuwa nazungumza suala hili nilisema kwamba watalii wanakuja kuangalia, lakini wakati wa kuangalia wanataka wapate *excess* ya kwenda katika ile sehemu.

Mhe. Waziri, Wambaa hivi sasa kuna sehemu moja mashuhuri sana na inavutia wataliiwengie sana, lakini cha kushangaza ni kwamba kuna kisehemu katibu kilomita tatu au nne, sehemu hii wanapokuja hawa watalii kutaka kuingia inakuwa ni usumbufu kwa sababu wakati wa mvu inakuwa barabara ni tope tupu. Sasa sijui kwa kuona kuna umuhimu kwamba kuna kitega uchumi mkubwa kinachofanya Serikali iingize mapato, labda Serikali imechukua umuhimu gani wa kuona kwamba ile sehemu iliyobakia ya kilomita labda tatu ya matengeneo ya barabara ile tumefikiria labda lini kibarabara kile tukitie lami ili kibarabara kile kiweze kupitika hasa wakati wa mvua na kuwaruhusu watalii kuingia zaidi katika eneo lile.

Mhe. Spika, jengine ni kuwa nafikiria tulifanya majaribio Idara hii ilifanya majaribio ya ujenzi wa barabara hasa barabara ya Mtambile/Kangani, Barabara ya Mizingani/Wambaa, barabara ya Kenya/Chambani au Ukutini na barabara ya Mgagadu/Kiwani, mawazo yangu ni kwamba hapa palifanywa majaribio, kwa sababu hapakujengwa barabara, kwa sababu kwa muda huu hivi sasa barabara zile ziko taabani na mashimo makubwa.

Sasa sijui hivi sasa Serikali imeona vipi au Wizara imeona hakuna haja ya barabara hizi kuziangalia tena upya na kuona kwamba yale majaribio yao yalifikia labda asilimi hamsini basi tukazimalizie. Kwa sababu Mheshimiwa, hivi sasa ile ni aibu kwa sababu barabara ambazo zimejengwa karibu miaka kumi iliyopita nyuma ziko

imara, lakini barabara ambayo najua fika kwamba ilijaribiwa kwa sababu kulipelekwa lami ilikuwa kama uji wa mtoto, au sijui ilikuwa kama ni iliyopelekwa katika barabara ya Mgagadu/Kiwani pale ilikuwa ni majaribio hasa, lakini majaribio hasa.

Lakini majaribio yale yalifeli na Serikali na Wizara inajua kwamba majaribio yale yalifeli na hivi sasa ile barabara sijui inaangaliwa na nani, kwa sababu huyu *UUB* sijui kama inaona kuwepo kwa umuhimu wa barabara zile kwa sababu hivi sasa tayari ilipoanza pale juu, maana ile sio lami nimeona Mhe. Spika, leo nikwambie ile waliyoitia barabara zile za kwenda Wambaa, Kangani ule ni wanja tu wameweka juu pale, ikinyesha mvua haipo tana na hivi sasa wana mashimo matupu.

Sasa nafikiri upo umuhimu wa kwamba barabara zile hivi sasa hasa ukiangalia kwamba au ukizingatia kwamba wakati wowote tutapata barabara inayotoka Ole kwenda Kengeja, kwa hivyo, barabara hiyo itakapofanya kazi itakuwa mzigo ni mkubwa wa barabara zile zinazokwenda ndani hasa za Kengeja na Chambani, lakini hizi ni mbovu, sasa sijui kuna utaratibu wa barabara zile kuzifanyia marekebisho kwani yale ya mwanzo hayakutosheleza.

Mhe. Spika, mimi naomba nimalizie kwa kusema kwamba hivi sasa katika nchi yetu usafiri wa nchi kavu umeongezeka kwa hata kubwa sana na ukiangalia barabara zetu nyingi tulizozijenga hazina taa za kuongozea barabarani na inakuwa ni usumbufu kiasi kwamba anayesubiri upande mmoja ambaye yeye hatoki *main road* anasubiri muda mkubwa, kiasi kwamba wanaopita *main road* wanakuwa wao ndoo walio na haki sasa mara nyengine unaona umesubiri muda mrefu kiasi kwamba unaona aa ujichomeke chomeke na ndio chanzo cha ajali barabarani.

Sasa nahisi sasa umefika wakati kwamba tunapojenga hizi barabara zetu, Mhe.Waziri, tuone sasa ipo haja ya kuweka taa zinazoongoza barabarani. Labda niseme labda hizi taa za sasa za majaribio za sola zina usumbufu, kama tumeziweka pia kwa majaribio basi tuone tumeshafikia hatua kwamba kuziona hizi taa zina usumbufu, ni wakati mwingi ukipita katika taa hizi zinakuwa hazifanyi kazi. Kwa hivyo, upo umuhimu hivi sasa kwa kuona kwamba taa hizi zifanyiwe marekebisho, tupate taa za kisasa na kuna umuhimu wa kuweka taa za barabarani kila panapohitajika, si hivyo, itakuwa siku zote tunachunana viuno, kwa sababu yule anataka apite, yule sio zamu yake ameshakaa muda mrefu bila ya kupata njia ya kupita, hilo lionekane kwamba hivi sasa hata katika kwenye miradi yetu ya kujenga barabara mpya basi wakandarasi waone ipo haja hivi sasa tunapojenga barabara mpya basi tunaweka taa za barabarani.

Mhe. Waziri, juu ya hayo yoote tunasubiri meli mpya, mimi sitaki kusema kwamba siungi mkono hoja hii, nasema niunge mkono, nawapa muda wa Mawaziri na Serikali kwa ujumla, nina imani kwamba ni sikivu, tuliyoyasema watayachukua na kuyafanyia kazi nakushukuru.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunpa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mchana huu na mimi nikaweza kuchangia machache katika bajeti hii. Nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kutuwasilishia Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu utakuwa si mkubwa kutokana na watu wengi wameshachangia mimi nianze na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, niipongeze Idara hii kwa kufanya kazi nzuri ya miradi ya sekta ya usafiri wa anga, kusema kweli wamejitahidi, wanastahili pongezi kwa kukamilisha maegesho ya njia ya kupitia ndege katika kiwanja cha ndege cha Kimataifa ya Abeid Amani Karume nawapa hongeza sana. Pia, niwapongeze kwa ujenzi wa jengo jipya la abiria ambao unaendelea, lakini ninachokiomba katika Wizara hii katika taarifa yake ya Mhe. Waziri, alisema kwamba malipo ya fidia tayari yameshaingia katika ofisi, naomba basi waharakishe kuona wale wanaotakiwa kulipwa fidia hii basi walipwe kwa wakati.

Mhe. Spika, nije katika mradi wa uimarishaji wa kiwanja cha ndege Pemba, mimi niipongeze Idara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa hatua za awali kwa ajili ya uwekaji wa taa katika kiwanja cha ndege cha Pemba, mimi niipongeze, lakini pia niiombe Wizara hatua hiyo iliyokuwa imeanza basi ihakikishe inaendelea kuona uwanja huu unapata taa, kwa sababu kama walivyosema wachangiaji waliopita kwamba malalamiko haya ya taa yamakuwa mengi, kwa hivyo, mimi niipongeze kwa hatua ya awali, lakini naiombe Wizara basi ijitahidi ione hili suala linakamilika kwa wakati.

Mhe. Spika, pia, niipongeze kuhusu ujenzi wa bandari ya Mpigaduru, mimi hapa naipongeza Idara kwa sababu kila bajeti kusema kweli hii bandari inaletwa taarifa yake lakini kazi yake bado hatujaiona, kwa sababu hii bandari ya Mpigaduru sifa zake zote zimo katika kitabu hichi cha bajeti lakini utekelezaji wake bado, sasa naumomba Mhe. Waziri, aje kutueleza ugumu wake ni kitu gani kinachokwamisha kwamba bandari hii haitekelezeki na walitenga milioni mia tano, lakini kwa mujibu wa taarifa wametwambia kwamba pesa hizo hazijaingia, kuna tatzo gani? Kwa hivyo, Mhe. Waziri, akija aje kutwambia kwamba wana tatizo gani kuhusu haya malengo waliyokuwa wamejipangia kwa bandari ya Mpigaduru haitekelezeki.

Mhe. Spika: Hiyo ndio Mpigaduri hiyo.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Mhe. Spika, nije katika mradi wa ujenzi wa barabara tatu za Pemba. Niipongeze Idara kwa kazi nzuri waliyoifanya, wamefanya kazi nzuri. Mimi mwenyewe nikiwa ni Mjumbe wa Kamati ya Ustawi tulipokwenda kuangalia madarasa pale tulikuta ni kweli tumepita katika njia zilizokuwa nzuri sana, wanastahili sifa na pongezi. Lakini hapa pana tatizo la kuhusu Skuli. Skuli hiyo wakati wa kutengenezwa njia imedidimia yote. Yaani maana yake ni aibu hata wanafunzi kukaa katika darasa. Ile skuli nimeisahau jina lake.

Lakini tulivyokwenda pale kama Kamati ya Ustawi wa Jamii tumesikitika sana kuona lile darasa jinsi lilivyodidimia. Baada ya kuuliza darasa lile lilikuwaje, tukaambiwa wakati wa kutengeneza njia magari makubwa yalikuwa yanapita katika lile eneo basi ile skuli ilipasuka, na kudidimia. Katika kuwahoji, wakatwambia kwamba Wizara hii mpaka sasa hivi barua wameshapelekwa lakini hawajapatiwa majibu kuona wanawasaidia katika ujengaji wa lile darasa.

Mhe. Spika, kusema kweli lile darasa lipo hali mbaya na hali hii imesababishwa na ujengaji wa barabara. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri waliangalie suala hili ili wanafunzi wetu wasipate shida, yaani ni aibu kubwa. Sisi wenyewe tulivyoenda pale tulikuwa tunajiuliza hapa pamepata matatizo gani. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, aione ile skuli ili wawasaidie katika ujengaji wa lile darasa ili wanafunzi wetu wapate kusoma.

Mhe. Spika, nikiendelea kuhusu taa za *solar* za kuongoza magari. Mimi niipongeze idara lakini panahitaji elimu, mpaka sasa hivi taa hizi zilivyokuwa zimewekwa lakini bado madereva hawajajua utaratibu. Inaweza taa kuwaka dereva kaganda tu pale mpaka anapigiwa honi nyuma ndio anashtuka na anajua ndiyo tayari anaruhusiwa kupita. Kwa hivyo, naiyomba Wizara ijitahidi kutoa elimu, bado madereva wetu hawajajua kutumia taa hizi za *solar*.

Mhe. Spika, kwa vile mimi nimesema sina mchango mkubwa na wenzangu wengi wameshasema, lakini nije kwenye meli. Mimi naipongeza serikali kama taarifa ilivyojieleza katika kitabu hichi, kwamba tunatarajia Mwenyezi Mungu akipenda mwisho wa mwezi wa saba meli hii itakuja, itafika kwetu Zanzibar. Mimi niipongeze tu Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya na meli kama taarifa zao zinavyoeleza basi ifike kwa wakati kama walivyosema.

Baada ya kusema hayo kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini/Magharibi, naunga mkono hotuba hii asilimia mia.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema aliyetujaalia uhai lakini pia

akatupa na uzima akatuwezesha kuwepo kwetu hapa kutekeleza majukumu yetu, lakini haya yote ni kwa maslahi ya Taifa letu. Lakini pia nikushukuru na wewe, kwa imani yako kubwa kunipa fursa hii na mimi kusema alau neno moja, katika hotuba hii iliyopo mezani wakati huu.

Mhe. Spia, naomba pia uniruhusu nitoe pongezi zangu kwa Mhe. Waziri wakati wa uwasilishaji wake alikwenda *speed* nzuri, lakini pia niwapongeze na watendaji wake.Nami ningesema leo sina la kusema lakini kuna mambo kidogo yananikwaza nimelazimika katika taasisi hii niseme neno. Mimi katika kitabu hichi cha bajeti nakuja katika ukurasa wa 21 kuna neno linalosema "Miundombinu na Huduma za Usafiri wa Barabarani".

Mhe. Spika, niseme kwamba usafiri wa barabarani ni muhimu katika shughuli zetu mbali mbali, kufanikisha mambo yetu mbali mbali ya shughuli zetu za maendeleo ni kiunganishi, barabara baina ya wananchi waliopo vijijini kuja kutoa huduma katika mji na kufanya shughuli zao mbali mbali za maendeleo na za kijamii.

Mhe. Spika, nianze kusema kwamba ujenzi wa barabara ni shughuli moja, lakini matengenezo ya barabara zetu ni shughuli ya pili ambayo ni muhimu sana. Nakusudia kusema kwamba tumekuwa na bahati mara nyingi ya kutumia fedha nyingi, kwa sababu tunajua kwamba ujenzi wa barabara unatumia fedha nyingi. Tunapojenga barabara hizi pale ambapo hutokea dosari ndogo ndogo tunashindwa sana kufanya magengenezo ya barabara zetu. Jambo hili hupelekea kugharimu fedha nyingi na mifano hai ninayo.

Baada ya mvua kubwa iliyokwisha kumalizika muda mfupi huko nyuma mwezi uliokwisha tuzizunguke barabara zetu tuziangalie hizi za mjini wala sio za vijijini. Njoo utokee Kwerekwe Amani, *round about* hapa uiyone shughuli ya mashimo. Sasa mimi nadhani tutumie ile taratibu yetu tuliyokuwa nayo zamani, hawa *UUB* ambao wakitumia sana matengenezo ya barabara zetu wakati ikitoboka kidogo basi unawakuta na lami na kokoto zao wanaziba vishimo vile na mara nyingi huepusha hata ajali. Hivi sasa kama unataka kwenda Mkokotoni maarufu sana njia hii inaitwa njia ya Namba 1. Kuna krosi humo kwenye barabara, kwa ajili ya kukwepa mashimo tu madereva, na tayari maajali mengi yanatokea kwa sababu hiyo.

Mhe. Spika, niiyombe Wizara irudie ule utaratibu wetu basi, jamani nyengine barabara zinakuwa nzima zinaanza kishimo kidogo mpaka zinafanyika mashimo ya kupanda migomba. Ni aibu, zile ni fedha za walipa kodi. Tukitunza pale padogo ambapo pametoboka basi tunapata fursa ya kuendelea kutumia barabara hiyo kwa vizuri zaidi. Nadhani hili kama litafanyika nina imani tunaweza tukaweza kupunguza hata hayo matumizi makubwa pengine ya barabara hizo nyengine zinazohitajika.

Lakini jengine niwakumbushe, nchi yetu ipo kwenye uwekezaji hivi, ile miundombinu ya kuweza kufikisha yale maeneo huru yaliyowekwa kwa ajili ya uwekezaji mna utaratibu upi, mtwambie. Tuna maeneo yametengwa tumeambiwa kwa ajili ya uwekezaji. Lakini jengine ambalo linanipa mtihani kwa barabara hii tunayosema maarufu kwa njia ya Namba 1, yale madaraja mmeyakagua mmeyaona? Jamani ile ni hatari, mabarabara tokea Ukoloni ndiyo lugha ambayo kuwa inatumika hadi hii leo madaraja yote yana mapengo, ni hatari. Muda si mrefu huko nyuma kama mwezi mmoja ilitokea ajali mama mjamzito lile gari lilikuwa linang'inia juu halipo chini halipo. Nakuombeni sana mnipe majibu ya kina yatakayoweza kunitosheleza ili kuweza kuipitisha bajeti hii leo.

Nayasema hayo nikiwa na sababu, nyote mnakwenda Kaskazini, lianzeni daraja la Kazole, mje Mto Mchanga, muendelee tena mzungushe mwende na Chaani, na kwengineko Kitope, hebu zitizameni zile daraja kwa yoyote aliyezoea kuipita ile njia aseme njia hii na madaraja haya ndiyo yanayopita wale wateni wetu kuelekea huko kwenye uwekezaji tunakopata pesa nyingi. Twende tukaone.

Jamani huko ndio tunapeleka watalii, huko Kaskazini sisi ndio tunao watalii hivyo. Sasa ikiwa fedha tunazihitaji kukusanya, lakini sisi miundombinuu ambayo inasababisha wale wageni wetu wapite kwa raha na kuona burudani na kutokuwasababishia ajali. Mashimo hivi ninavyozungumza hapa kama Mhe. Waziri au na watendaji wako na Naibu utaseme tuungie kwenye gari tukitoka hapa twendeni mkaone katikati ya hayo madaraja basi kuna mashimo, ni hatari. Hii ni bajeti ya tatu, nainuka hapa na huwa tunaitaja sana, husaidiwa na Mheshimiwa wangu hapa Abdi Mosi, tulisimama zaidi ya mara tatu. Mhe. Gavu, uliwahi kujibu swali Naibu Waziri kwamba tupo kwenye mpango itaingia na itajengwa, itaanza hapo Bububu na itaelekea mpaka pale kinazini ambapo njia ya Nungwi inamalizia.

Mhe. Spika, niseme kwamba kwa upande wa kukatisha Mahonda kwenda Donge hatuna matatizo tunasema hivyo. Lakini hii njia ya pili jamani ni tatizo, serikali hili mlione na mtupe majibu ya kutosha, hatutaki tena zile hadithi za alinacha. Tunataka hasa tupewe ni lini hasa shughuli yetu itaanza. Jamani hayo madaraja ni hatari sana, yemeshadondoka upande wa pili ukipita huu mmoja umesimama na gari, mwengine umeshakatika kabisa, huna amani katika nafsi yako, ndiyo ukweli ulivyo.

Mhe. Spika, sasa niseme njia yetu hii hii ambayo inatoka Bububu kuelekea huko hapa kuna kituo kinaitwa kwa Nyanya. Hichi kituo hakikujengwa lakini imezoelekwa kwamba magari yanayoishia ya Bububu huwa yanafanya kuzungusha na kurudi. Lila eneo ni gumu, sio eneo mahsusi ambalo linakubalika kwa ajili ya magari kuzungusha, ni hatari sana. Nakuombeni sana sana kabisa muangalie utaratibu pale kwa kuwa imezoeleka kwa wakati huu kwamba ruti za gari nyingi

ambazo zinapitia kule mzunguko wake huwa ni pale na kuna makutano ya njia nyengine ambayo inatokea Mbuzini na wananchi pale huwa wana mfadhaiko mkubwa na mara nyingi hutokea ajali.

Tunakuombeni Waheshimiwa mtwambie, mtengeneze basi kituo cha kufikia pale ambapo ni pa kuzunguusha ambapo patakuwa pembeni na zile barabara hasa. ili tuepushe ajali ambazo zinaweza zikatokea. Kwa sababu pale ni kiunganisho cha njia na zinabaki pale barabarani jambo ambalo halistahiki. Kwa kuwa tunawapenda wananchi wetu na hatuwatakii mabaya basi *Inshaallah* ionekane basi juhudi inafanyika. Kuna sehemu pale kama mtafanya vizuri basi inawezekana kabisa, wapenye ndani kidogo washushe abiria wao na hatimaye waingize magari, yatoke kwa kwenda. Lakini sio kwa utaratibu ule ambao upo, sio mzuri. Naomba sana kwamba wizara iliangalie hilo kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, sasa nakuja kwenye hili Shirika la Meli na Uwakala. Niseme kwamba kwa wakati huu ambapo hizi meli zilizokuwepo zinafanya kazi utaratibu wake sio mzuri. Nalisema hili kwamba naungana na waliotangulia kusema kwamba meli inatumia masaa mengi zaidi, lakini pia inakuwa na abiria wengi zaidi. Jambo ambalo kwa wakati huu tukizungumzia hoja hii Wazanzibari bado tunalengwa lengwa na machozi. Kwa hivyo, kumuachia mtu akafanya uzemba wa kupoteza roho za Wazanzibari wenzetu hatuko tayari.

Niombe uuzaji wa tiketi ni jambo la kustaajabisha, kwamba kuna ofisi maalum inayotoa tiketi, iweje tukute nje kuna tiketi zinauzwa, kulikoni na kazitoa nani. Nani katoa tiketi nje ziwekwe mikononi? Jamani tujifunzeni utaratibu kuwajibika, na hayo ndiyo maradhi yetu hapa Zanzibar. Jamani hivi tunatengeneza Sheria za Rushwa, sisi wengine tena tunatarisha mambo mengine ya kinyume kimbele, inakuwaje. Msingi kama vijana hawana kazi watafutie njia za kupata ajira zao, lakini sio tiketi ya pale kibandani, ule ni usumbufu unasababisha mambo mbali mbali ambayo Waheshimiwa wenzangu waliyataja hapa, kwamba hata kukitokewa tatizo hatutokuwa na takwimu ya kutosha, jambo ambalo hatulitarajii Mwenyezi Mungu asililete *Inshaallah*. Kweli kabisa kwa tatizo kama hili *Wallahi* hatukuwa na takwimu ya watu wetu waliokuwemo katika meli ambazo zilipata ajali.

Naiyomba sana serikali jamani tujifunzetu tabia ya uwajibikaji, tujifunzeni tabia ya nidhamu ya uwendeshaji wa shughuli za kiserikali, taratibu za shughuli za taasisi zetu, tuwajibike na tutumike kwa mujibu wa taratibu na sheria tulizojiwekea sisi. Tuna vituo tumevitengeneza lakini matokeo yake unazikuta tiketi mkononi, haipendezi.
Mhe. Spika, sasa nije na jengine hili la kushukuru kwamba taarifa rasmi tuliyoipata hapa kwamba meli hii itawasili mwezi wa saba mwishoni. Hii ni habari njema, inajenga matumaini, lakini niombe sana kusema kwamba kwa masikitiko makubwa

baada ya kupata meli zetu mbili za mwanzo Mapinduzi na Maendeleo, jambo ambalo limesikitisha kwamba meli zile hazikupata watoto, hazikufanikiwa, tumefanikiwa kutumia lakini hazikufanikiwa kutoa watoto. Niiyombe sana serikali kupitia taasisi hii kwamba meli hii ije izae faida lakini pia itoe huduma ya kuboresha usafiri wa wananchi wetu utakaokuwa hauna usumbufu.

Isiwe Mapinduzi *I*, kafa hakuonekana tena lakini Mapinduzi *II* basi tuwe na mabadiliko yanayoendana hasa kabisa na wakati wa leo. Jamani hii meli ije izae hasa, tuje tupate jibu tuone mtoto wake, lakini tunanunua meli tunabakiwa na meli mpaka anakufa meli. Aaa! jamani, halafu Shirika na mambo mengine, haya mambo hayazungumziki. Mimi nadhani kwamba meli hii ni pesa za walipakodi wenyewe, kwa hivyo, wafaidike nayo lakini itoe matunda kwa manufaa ya wananchi wetu. Nchi yetu ni visiwa, kwa hivyo, tunahitaji meli nyingi zaidi ya hii moja Mapinduzi *II* , ziliopo zimechakaa, zimechoka, zinatumia zaidi ya masaa 12, 13, watu wapo kwenye bahari, ambapo ni pahala padogo watu wanaweza kwenda kwa zaidi ya masaa mawili pengine wameshafika huko.

Mhe. Spika, sasa nizungumzie juu ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Niseme kwamba nimeona humu katika hichi kitabu kwamba kuna mpango kuhusu hiyo programu imeandaliwa ya maandalizi ya kuboresha Uwanja wa Ndege hususan kule Pemba. Napenda niyaseme haya kama nilivyoyasema baje iliyopita, jamani mnajua kwamba kule Pemba ni sehemu katika sehemu ya Zanzibar ambapo viongozi wetu wa Kitaifa wana nafasi na fursa ya kwenda huko. Inawezekana kuna siku wakafanya shughuli zao mpaka usiku, lakini wakatamani kurufi huku hivi taa ndiyo iwe tatizo, linafanana hili jambo jamani, linaingia akilini?

Halikadhalika, kuna shughuli zetu za uwekezaji kule Pemba ambapo tunapata fedha za kigeni, hebu tujiulize endapo wale wageni wetu wapo kule wametamani au wametokewa dharura ya kutaka kurudi Unguja na niwakati wa usiku, hebu tujiulize wageni ambao sisi tunatumia *alot of money* kwenda kutangaza utalii waje wawekeze, wamefika wapo kule na wengine ni watalii wamekuja kutembea. Hebu tujiulize kama imewatokea bahati ya kusema iko haja ya kuondoka usiku Pemba maana yake ishindikane. Ninaiomba Serikali hii mipango isiwe mipango, lakini iwe ndio azma ya huu utekelezaji wenyewe.

Lakini jengine kwamba kama *Terminal II* imejengwa Unguja, hebu nipeni mipango yenu hasa ya kujenga kule uwanja wenyewe hasa wa kileo unaoendana na wakati, hebu nipeni mipango yenu ile ni sehemu katika sehemu ya visiwa hivi viwili. Hebu tuambieni mna mpango gani wa kujenga kiwanja hasa madhubuti cha kileo ambacho na ndege za Kitaifa zitakwenda kule, ni lini na utaratibu gani? Hapa tuna *Terminal II*, tumeandaa mambo mbali mbali na programu mbali mbali, lakini je, kwa upande ule ambapo ni sehemu nako tuna uekezaji, mna utaratibu gani.

Mhe. Spika, naomba unisaidie kidogo niseme na hili moja, hili la Bandari ya Mpigaduru, jamani hii nyimbo ya kubembelezewa mtoto, nyimbo nzuri hubembelezewa mtoto kweli na kweli maana mwaka wa 5 tunabembeleza mtoto kwa Mpigaduru. Tunamaliza kipindi hiki tangu nimehamia Baraza hili 2011 namalizia 2015 kwamba bado tuna Mpigaduru, jamani, ili uchumi wetu ukue lazima tuwe na bandari za aina hii, kweli kabisa tuna nia au tumeiweka tu mipango hii kitabuni.

Mhe. Spika, niseme kwamba ninakushukuru sana kunipatia nami fursa hii, sipendi niweke utata katika hili, ninaloliomba kwamba kwanza kabisa ni yale madaraja ya njia namba moja yaangaliwe kwa kina na ile hali angalau ya dharura, hamjayaona nendeni mkaone. Lakini jengine la pili ni la kituo kile cha kwa Nyanya na jengine ni hiyo ya *Airport*.

Baada ya kuyasema hayo ninakushukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Ashura, kwa mchango huo na wizara hii ina utaratibu wa kila inapofika bajeti kuziba mashimo, hivi mara hii imekuaje. *(Makofi)*

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Spika, na mimi nachukua fursa hii kukushukuru kunipa nafasi kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, pia, naomba nitoe pongezi zangu za dhati kwa Serikali kwa jitihada ambazo imezifanya kujenga barabara na miradi mbali mbali ya maendeleo katika wizara hii. Pia, napenda kutoa pongezi Mhe. Spika, kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wake wote kwa kutekeleza majukumu yao siku hadi siku kwa ufanisi.

Mhe. Spika, mimi ni mjumbe wa kamati, mengi tumeyazungumza kwenye kamati, tumeshauri kwenye kamati, kwa hivyo, sitokuwa na mengi sana ya kuzungumza Mhe. Spika. Lakini nianze na miradi ya Sekta ya Usafiri wa Anga. Hapa naomba nichukuwe fursa hii kumpongeza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kazi aliyoifanya Mkurugenzi huyu ni kazi kubwa hali halisi tunajionea, ukilinganisha miaka 3, 4, iliyopita uwanja wa ndege ulikuwa sio hali hii, hii imetokana na jitihada zake na usimamizi bora ambao amesimamia.

Mhe. Spika, nitakwenda katika mradi wa ujenzi wa meli mpya. Kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa hatua hiyo nzuri ya kuona kuna haja ya kuwa meli ambayo ya kisasa na kubwa itayobeba watu wengi ili kuwapunguzia wananchi

wetu mzigo na hasa kumsaidia muekezaji wetu Bakhresa ili kuwe na meli tofauti ambazo zinabeba abiria na kuweza kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Spika, nataka nichangie katika Mamlaka ya Usafiri Baharini. Hapa naomba nitoe maelekezo, kwa sababu sisi ni kamati tulikwenda kuangalia, mimi mwenyewe nilikwenda lakini katika *MV.* Seagull. Tulikwenda kuangalia ile meli na baadhi ya wenzangu walikwenda kwenye meli ya *MV.* Maendeleo. Tulienda kuangalia *MV.* Seagull na baadhi ya wataalam ambao wapo katika mamlaka ile ya meli, kunaonekana kama ripoti waliyotoa katika mamlaka alipewa maagizo muekezaji huyu kuwa afanya ili akimaliza maagizo yale apewe ruhusa ya kufanya kazi hiyo ya kupakia abiria. Lakini katika ufuatiliaji wetu Mhe. Spika, kunaonesha kuna baadhi ametekeleza na baadhi hajatekeleza.

Kwa hivyo, hapa nilikuwa naomba niishauri wizara ifuatilie suala hili kwa kina kupitia wataalam wetu wa mamlaka na ikiona imeridhika na yale maagizo ambayo ametoa muekezaji yule kufanya hiyo kazi imejiridhisha, basi ninaiomba Serikali itoe ruhusa hiyo, lakini tuangalie haya ni maisha ya watu na tukiangalia matukio ya nyuma, tumeona matukio makubwa tu na yote yaliyotokea haijaangaliwa muekezaji wala nani, imelaumiwa Serikali.

Lakini mimi ushauri wangu ijiridhishe na ripoti hiyo kutokana na wataalam wake wa mamlaka hata ikitoa maamuzi ijue inatoa maamuzi kwa kuwasaidia wananchi wetu. Kwa sababu hapa tunaangalia maisha ya watu, hatumuangalii muekezaji ni nani, tunaangalia maisha ya watu, likitokea halaumiwi muekezaji ila inalaumiwa Serikali. Kwa hivyo, ninaomba niishauri tu wizara itakapotoa maamuzi ijiridhishe kweli hii meli iko tayari kubeba wananchi na bila ya matatizo yoyote.

Mhe. Spika, nitakwenda katika ukurasa wa 19, kuna changamoto hapa ambazo zimeeleza za wizara hii, katika changamoto hizo Mhe. Spika, kuna suala zima la uhaba na uchakavu na zana zinazotumika katika ujenzi na utunzaji wa barabara. Kweli zana wanazozitumia idara hii ni chakavu, kwa hivyo, hapa niiombe Serikali suala hili ilifanyie kazi ili hizi barabara nyingi ambazo zimejengwa na pengine haziendi mbele kutokana na uhaba huu wa zana hizi ambazo wanazozitumia ili kuona kwamba hii kazi inaendelea bila ya matatizo yoyote.

Na kuna suala zima la malipo kwa hawa wananchi ambao wa fidia katika upitishaji huu wa majengo ya barabara hizi basi Serikali ichukue hatua ya suala hili kwa sababu hawa ni wananchi wetu na wanahitaji madhali mtu kapata athari katika kupitisha barabara zile anahitaji alipwe fidia. Kwa hivyo, ninaiomba wizara ilifanyie kazi suala hili ili kupunguza yale malamiko mengi ambayo Waheshimiwa wenzangu wamelalamika.

Mhe. Spika, changamoto nyengine ni upungufu wa raslimali fedha za kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Miradi ya barabara ni mingi Mhe. Spika, na mingi imejengwa iko hatua nzuri tu na ukiangalia tena Pemba kumejengwa barabara nzuri tu Mhe. Spika, nyingi. Kwa hivyo, mimi nashindwa kuelewa wakisema Pemba imetengwa, Serikali haina nia ya kuwatenga watu wake, Serikali haina ubaguzi kuwatenga watu wake, Serikali inawatumikia wananchi wote. Kwa hivyo, suala la barabara kujengwa kwa kweli tunastahiki kuipongeza Serikali kwa dhati kabisa kwa sababu mabarabara yanaonekana, hatua nzuri imechukuliwa na Serikali hii.

Mhe. Spika, kuna suala zima la ukosefu wa vifaa vya kisasa na jengo la kufanyia ukaguzi wa vyombo vya moto, hii nayo ni changamoto ambayo imeelezwa katika ripoti Mhe. Spika, na hivi karibuni tulipata semina ya Idara hii ya Barabara, lakini katika changamoto wamesema ajali nyingi zimetokea. Tukapia hesabu pale kuanzia Januari mpaka mwezi wa Mei si chini ya watu kama 70 wamepoteza maisha.

Lakini kupatikana kwa kifaa hiki ambacho cha kufanyia ukaguzi vyombo vya moto inaweza ikasaidia pengine kupunguza ajali ambazo zinatokea mara kwa mara. Licha ya ajali nyengine zinatokea kutokana na uzembe wa madereva, lakini kikipatikana hiki kifaa kinaweza kikasaidia kwa kiasi fulani kupunguza hata hizi ajali ambazo zinatokea mara kwa mara.

Changamoto nyengine Mhe. Spika, ni ukosefu wa sheria na kanuni katika kusimamia huduma za Miundombinu na Mawasiliano. Hili nilikuwa ninaliomba kanuni zifanyiwe kazi na sheria ambazo zina mapungufu nazo zifanyiwe marekebisho. Kwa sababu sheria itakuwa inatoa maamuzi ambapo sheria hiyo pengine hailingani na lile kosa ambalo mtu amelifanya, kwa hivyo, itakuwa kama hatutoitendea haki Serikali yetu na wala yule mtu hatumtendei haki. Kwa hivyo, naomba pia sheria zifanyiwe marekebisho na kanuni pia zifanyiwe kazi.

Suala zima la uvunjaji mkubwa wa sheria na usafiri wa barabarani, hili kubwa nimuombe Mhe. Waziri, kubwa hapa ni elimu kwa wananchi wetu ilitolewe zaidi ili kujua vyema hizi Sheria za barabarani na kuna suala zima la changamoto ya utegemezi mkubwa washirika wa maendeleo. Miradi mingi yetu ya maendeleo inaendeshwa kutokana na washirika mbali mbali, lakini ishafika wakati na sisi wenyewe kama Serikali tujipunguze katika utekegemezi huu.

Hii kutegemea sana washirika wa maendeleo kunapelekea hata ile mipango yetu ambayo tunayojipangia kama serikali inakwama kwa sababu ushajipangia pengine ujenge barabara 6, lakini unaweza ukajenga barabara 2 kutokana na washirika pengine hawakamilishi ile ahadi ambayo wametoa. Si kama nawalaumu lakini

ninawapongeza washirika wa maendeleo kwa jitihada wanazozitoa kwa serikali yetu, lakini na sisi kama Serikali lazima tujidhatiti tupunguzi utegemezi zaidi tuweze kuitumia katika miradi yetu mbali mbali ya maendeleo.

Mhe. Spika, la mwisho, kuna changamoto nyengine ya kutuama kwa maji kwenye baadhi ya maeneo ya barabara zetu na eneo la nje la uwanja wa ndege na kutokana na ufinyu wa miundombinu, hili nalo Mhe. Waziri, pia mlifanyie kazi kwa sababu uwanja wa ndege sasa hivi uko katika hali nzuri, lakini ikionekana maji yanatuama tuama pia ile hadhi itapungua.

Mhe. Spika, kuna suala zima la madaraja Mhe. Ashura, alisema njia ya Kaskazini, suala zima la madaraja ambayo hayana ubora. Niishauri Serikali iyafanyie kazi madaraja hayo lakini kuwa na madaraja ambayo sio bora kusipelekee yale mazuri yote yaliyofanywa na Serikali ikaonekana hayapo kutokana na daraja hilo tu au pengine kwa njia za kaskazini. Kama Serikali imefanya mazuri lazima tuipongeze, hali halisi inaonekana na kama kuna mapungufu wajibu wetu kama chombo hiki kuishauri Serikali ili kuona shughuli zetu zinaendelea vizuri.

Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nichukue nafasi kuwashukuru, kuna mchangiaji mmoja ambaye namuomba radhi sana amebaki kwa sababu nimepata na maombi mengine kwamba kuna kazi moja muhimu ifanyike hivi punde. Kwa hivyo, huu muda mchache uliobaki ninauweka kwa ajili ya kazi muhimu na kazi yenyewe ni hii ifuatayo:

Kwamba Waheshimiwa wote wale wa Kamati ya Wenyeviti wanaombwa wakutane kwa ajili ya kikao cha kupitisha *appropriation bill* na mkutano au kikao hicho kitakuwa mara baada ya kuondoka humu ndani na nimeweka muda huo ili waimalize kazi hiyo mapema na wende zao mapema pamoja na Waheshimiwa wengine ili jioni tufike mapema sana kumaliza kazi hii ya kupitisha mswada huu tukiwa na akidi nzuri sana ndani ya Baraza hili.

Hivyo, niwaomba Waheshimiwa Wajumbe, tujitahidi tuwahi mapema kwa sababu tutaporudi nitakuwa ninawaita Mhe. Naibu Waziri, hatimaye Waziri ya kufanya majumuisho. Kwa hivyo, yule mjumbe ambaye hakupata nafasi nimuombe basi apeleke kwa maandishi wa Waheshimiwa pale na *Inshaallah* hilo ombi lake litatekelezwa kupitia maandishi atakayoyapeleka pale.

Baada ya hayo machache Waheshimiwa Wajumbe tusisahau kuhudhuria kikao cha kamati ya wenyeviti mara baada ya kuondoka humu ndani. Kikao kinahirishwa hadi saa 11.00 jioni.

(Saa 6.38 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tulikubaliana kwamba tukija jioni tuanze majumuisho, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumkaribisha Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, aanze kutufanyia kazi hiyo. Karibu Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kuweza kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka huu wa fedha 2015/2016. Mhe. Spika, kabla ya kusema mengi naomba na mimi nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Chwaka niseme kwamba naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja kwa mia moja.

Mhe. Spika, mchango wangu nitauelekeza katika kutoa ufafanuzi kwa baadhi ya wajumbe wenzangu waliotangulia kusema ili kwa dhamira na lengo la kumsaidia Mhe. Waziri wangu katika kutoa ufafanuzi wa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, wajumbe wameeleza hoja nyingi na za msingi, imani yetu kwamba hoja zetu zilikuwa zina lengo na madhumuni ya kutaka kujenga na kuimarisha Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika utendaji kazi uliokusudiwa. Kwa kuanza Mhe. Spika, Mhe. Salim Abdalla Hamad, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Viwe Khamis Abdalla na Mhe. Saleh Nassor Juma, wote kwa jumla walitaka kujua kuhusiana na taratibu au mipango ipi ya serikali kuhusiana na suala zima la uimarishaji wa bandari hasa hasa bandari za Pemba kwa maana ya kwamba bandari ya Wesha, bandari ya Wete na bandari ya Mkokotoni ya hapa Kaskazini Unguja.

Mhe. Spika, wizara yangu kwa kupitia Shirika la Bandari inaendelea kuziimarisha bandari zote hizo kama tulivyozitaja. Aidha, kwa kupitia Shirika la Bandari tumetenga kiasi cha bilioni 1.02 kwa ajili ya kazi ya ujenzi wa bandari ndogo ya Mkokotoni. Na kwa hatua za awali tunaanza kujenga upande ule wa Tumbatu baadae tutakuja upande huu wa Mkokotoni. Aidha, kwa ajili ya bandari ya Wete tayari tumekusudia kutenga takriban shilingi 251,000,000 kwa ajili ya kufanya hivyo katika mwaka wa fedha, mwaka unaofuata.

Mhe. Spika, suala jengine liliuliziwa kwa mapana sana lilikuwa suala zima la chelezo katika bandari yetu ya Malindi. Kama tunavyojua kwamba Shirika la Bandari pamoja na mambo mengi linamiliki eneo la chelezo pamoja na huduma za ukarabati wa vyombo vinavyokwenda katika chelezo hicho.

Aidha, chelezo hicho kimejengwa kwa kipindi kirefu hivi sasa, na ni kweli kwamba kinahitaji kuboreshwa au kufanyiwa marekebisho. Lakini kwa kuwa hatua za kufanya marekebisho zinahitaji gharama na ufundi mkubwa, tayari Shirika la Bandari linafanya utaratibu wa kupata mtu wa kuweza kuwafanyia mabadiliko hayo. Kwa hatua za awali mjenzi ama mkandarasi waliyemtumia amewapa zabuni ya *Euro* takriban 8078 ambapo wao walipoziangalia kwa ujumla wameona ni hatua kubwa. Na kiasi hiki cha fedha kilitaka kutumika kwa ajili ya kujenga ukuta wa kuzuia mawimbi (*breakwater wall*). Shirika limejiandaa kuona kwamba kitu hiki bora kiende hatua kwa hatua kwa kuanza na vifaa vya kuimarisha bandari ili baadae hali itakaporuhusu iweze kuchukua hatua ya kuweza kuimarisha chelezo. Aidha, maelezo zaidi yametolewa katika kifungu 45 cha bajeti hii ambayo tumeisoma.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa linauliziwa suala zima kuhusiana na suala la meli *MS. Sepideh*. Meli hii imekwenda mkono wa tatu katika kumilikiwa kwake; mtu wa kwanza aliyekuwa akimiliki aliuza kwa mtu wa pili, mtu wa pili aliyekuwa akimiliki ameuza kwa mtu wa tatu. Bahati nzuri kwamba utaratibu wa ku-*transfer* unapo-*transfer* una-*transfer right* na *liability* zake. Mtu huyu wa pili ambaye alikuwa akimiliki hii meli aliwahi kupatiwa huduma na Shirika la Bandari. Kiutaratibu angepaswa kulipa kwa wakati muafaka, lakini hakuweza kufanya hivyo na yeye amepata nafasi ya kuweza ku-*transfer ownership* yake kwa mtu wa tatu. Sasa shirika lilikuwa limetoa huduma takriban ya shilingi milioni 71,000,000 walikuwa wakidai.

Mwaka 2013 baada ya kuona kwamba shirika halijalipwa wakaweza kufungua shauri katika Mahakama, na kwa bahati nzuri kwamba imetokezea kuwa meli ile imeuzwa kwa mtu mwengine, maamuzi ya Mahakama yamekuja kumkuta mtu wa tatu ambaye anamiliki hiyo meli. Na katika hatua za awali za mazungumzo mmiliki wa tatu hakuonesha kulikubali moja kwa moja, lakini Mahakama imetoa maamuzi ya kutaka meli izuie ili waweze kulipa deni na wadau hawa wako tayari kukutana.

Sisi baada ya kuzungumza na wenzetu wa shirika wao wanasema hawaoni tatizo la kuweza kukutana na mdau wakaweza kukubaliana ili meli hii ikatoa huduma za usafiri kama vile ambavyo imekusudia. Na hawaoni tatizo kwa sababu mmiliki huyu huyu tayari ana vyombo vyengine ambavyo kulikuwa kuna matatizo kama hayo ya kibiashara baina yake yeye na shirika na ameweza kuzungumza na

akaendeleza urafiki na uhusiano mzuri kama *customer* na kama yeye mpata huduma.

Mhe. Spika, suala jengine ilikuwa ni suala la idadi ya meli ambazo mwaka huu zimepungua kuweza kuja kufunga nanga. Hoja hii ni kwamba kadri siku zinavyokwenda ndipo wenzetu wanapopata teknolojia kubwa wanaongeza ukubwa wa meli husika, meli zile zilizokuwa zikija zilikuwa ni ndogo zaidi kulikoni meli zinazokuja hivi sasa. Kama sote tunavyojua kwamba kuna meli zile kubwa wanazoita *PANAMA* ambazo zina uwezo mkubwa zaidi, meli moja ina uwezo wa kuchukua mizigo ambayo ilipaswa na kuchukuliwa na meli mbili ama tatu. Kwa hiyo, idadi hii imeshuka lakini ukienda katika ile *GR* utakuta kwamba huku kumeongezeka kwa maana ya kwamba ukubwa wa meli ambazo zimehudumiwa sasa hivi zinahudumiwa meli kubwa zaidi, ingawa idadi imepungua kulikoni mwaka jana.

Mhe. Spika, ilikuwa suala jengine suala la bandari kuweza kufanya kazi muda wa masaa 24. Hatua hii tayari Shirika la Bandari limeshafika, linafanya kazi masaa yote 24 isipokuwa kuna baadhi ya nyakati hasa za usiku huduma zile ambazo zinahitaji utoaji wa vifaa katika eneo la bandari, serikali imeona ni vyema ukasitisha utoaji wa vifaa, huduma nyengine za kibandari zitaendelea kuwepo. Na hali hii imetokana na mashauriano mazuri baina ya serikali hasa na vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kupitia Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Malengo ni kuona kwamba huduma zinatolewa usalama wa wananchi wetu, usalama wa vifaa vyetu inakuwa ndio kipaumbele kikubwa kuliko hatua nyengine zozote.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni suala zima la uimarishaji wa bandari hasa upatikanaji wa vifaa. Tayari Shirika la Bandari limeshatoa zabuni kwa kupitia magezeti ya Zanzibar Leo, *Daily News*, gazeti ya *East Africa*, gazeti la *Business Week.* Awamu ya mwanzo zabuni hizo zilifunguliwa tarehe 12/05/2015 na kufanyiwa tathmini, awamu ya pili zilifunguliwa tarehe 16 June, 2015 na kazi ya kufanyiwa tathmini itaanza ndani ya wiki hii. Vifaa hivyo vyote vitanunuliwa kupitia mkopo kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar hivi siku za karibuni.

Mhe. Spika, pia, lilikuja suala la hoja kwamba, kwa nini serikali isiliruhusu Shirika la Bandari kuweza kutafuta fedha nje ya mfumo wa kibajeti wa serikali. Tayari serikali imeshatoa idhini na kama utafuatilia vizuri utaona takriban miradi yote inayotekelezwa na Shirika la Bandari hasa ule mradi mkubwa tayari Shirika la Bandari inapata fedha kwa kupitia mkopo, kupitia makampuni ama mabenki yetu yaliopo ndani. Kwa mfano, imefanya mradi mkubwa sana wa ununuzi wa *tag* kubwa ambayo imegharimu karibu shilingi milioni 10,000,000 ambazo fedha hizo zilikopwa katika Benki ya Watu wa Zanzibar kwa kupitia *foreign currents*, yaani

Euro takriban milioni 4 ziliweza kukopwa na tayari utaratibu wa kurejesha deni hilo umeshaanza na takriban shilingi milioni 500 zimeshaanza kurejeshwa *PBZ* ili kuweza kuwa mteja mzuri wa kuweza kukopeshwa mwakani tukaweza kuendeleza miradi.

Kwa hiyo, hoja ya serikali tayari idhini imeshatolewa na utaratibu ni kwamba tayari shirika letu hili limeanza na utaratibu wa kukopa kwa ajili ya kuimarisha na kuendeleza miradi mbali mbali.

Mhe. Spika, suala jengine ilikuwa ni suala kuona namna gani mwenzetu Said Salum Bakhresa kuweza kushirikiana nae. Sisi kama wizara na shirika hatuoni pingamizi yoyote ya kushirikiana na Said Salum Bakhresa. Imeanza hivyo kwa bandari ya Malindi. Imeanza hivyo katika uimarishaji wa vyombo vyake kwa ajili ya kuwapa huduma wananchi wetu, hatuoni tatizo kwa upande wa Pemba. Tumeanza mazungumzo nae ameonesha nia ya kukubaliana na sisi na sisi tuko tayari kukubaliana na yeye. Hatua ya awali tumekuja tukazungumza yeye anakwenda kujisikiliza ili atakaporudi kwetu na sisi tuweze kujisikiliza, na tunaamini tutafika pahali tutakubaliana kwa sababu sote tuna dhamira moja ya kutaka kumsaidia Mzanzibari ili aweze kupata huduma nzuri ikiwemo masuala ya usafiri wa baharini.

Mhe. Spika, ilikuwa suala jengine ni kuhusu kujenga kipaa katika mageti hasa kwa wasafiri wanaotoka katika bandari ya Mkoani, lakini pia kwa askari waliopo katika bandari ya Malindi. Mhe. Spika, suala hili tumelipokea tutawataka wenzetu wa Shirika la Bandari waweze kulifanyia kazi na ikiwezekana waweze kutekeleza kwa vitendo ili kuondoa usumbufu wanaoupata wananchi wetu hasa kwa nyakati za mvua ama wakati wa jua kali, kwani ikitokezea kipindi cha mvua na wasafiri hasa wanaobeba watoto wadogo ni kweli inakuwa usumbufu mkubwa na unaweza ukapelekea hata homa kwa watoto wetu. Kwa hiyo, sisi kama serikali tumelipokea na tuna hakikisha kwamba tutalifanyia kazi baada ya wenzetu wataalamu kuweza kulipitia na kulifanyia tathmini kwa kina na kuona kama inawezekana kutekelezwa basi nalo hilo litatekelezwa.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini *ZMA* kulikuwa kuna hoja nyingi, miongoni mwa hoja ya kwanza ilikuwa ni ushauri wa kamati kuwepo kwa ukaguzi wa meli mara kwa mara ili kupunguza ajali za baharini. Ushauri huu upo na utaratibu wa *ZMA* kwa kupitia mamlaka ambayo wamepewa wanasheria unamruhusu kuweza kukagua ukaguzi wa shaka. Kwa hiyo, ushauri huu sisi tunaupokea na tutawaagiza wenzetu wa *ZMA* wazidi kufanya *rapidly*, maana ya kwamba kama wanafanya mwezi angalau miezi mitatu, minne waweze kufanya ukaguzi huu wa shaka ili kuweza kubaini mapungufu ya vyombo hivi kwa

madhumuni na malengo ya kuimarisha usalama wa vyombo vyetu vya baharini ili kuweza kujikinga na majanga ya maajali.

Lakini kubwa zaidi tutahakikisha kwamba chombo chetu hiki cha *ZMA* kinafanya kazi zake kwa kushirikiana na wenzetu wa chombo cha *SUMATRA* na hii ni faida kwa pande zote mbili, maana kama chombo kitakuwa kinakaguliwa upande mmoja kikagundulikana na kasoro, upande wa pili ukisema hauna kasoro itakuwa tunatengeneza mgogoro. Lakini chombo hiki kinapokaguliwa na pande zote mbili za vyombo hivi vya usalama wa baharini na vikiridhika vyote viwili kama kuna kasoro basi chombo hiki inakuwa rahisi sana kuweza kukidhibiti, na kikiwa kime-*qualify* kinakuwa kime-*qualify sides* zote mbili kwa kuweza kutoa huduma za usafiri wa baharini na hivyo kuhakikisha kwamba usalama ule unakuwa mzuri zaidi kwa wasafiri wa baharini.

Mhe. Spika, suala la pili, ilikuwa ni kwamba ripoti hizi za ukaguzi zinachelewa, ni kweli ripoti hizi zinachelewa, lakini hoja ya kuchelewa inatokana na utaalamu na inachelewa ili kuhakikisha kwamba kile ambacho kimeripotiwa kiwe sahihi, kulikoni kutoa ripoti mapema ikawa ina mapungufu. Kwetu sisi tunaamini kwamba kuchelewa kwake kunatokana na ile kutaka kufanya kazi ambayo haitoacha shaka katika kuona yale mapungufu yaliyobainika ama kama chombo kiko salama ili tu pale kitaporuhusiwa yasije yakajionesha mapungufu mengine ambayo yanaweza yakapelekea kuzalisha kwa majanga ambayo kila mmoja hakuna angependa afurahi kutokea kwake.

Kwa hiyo, nimuombe tu Mhe. Mjumbe, kwamba aendelee kuwa na subra na kuwaachia wataalamu hawa bora wachelewe kutoa ripoti ili tu ripoti itakapotelewa iwe ripoti ambayo imekamilika na yenye kujitosheleza kulikoni kuharakisha kutolewa ripoti ambayo itaacha mapengo yatakayopelekea majanga kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, suala jengine limetolewa suala la vyombo vya uokozi wa baharini, hili bila shaka kama serikali tunakubaliana nalo na sisi kama wizara tunaona ipo haja ya kununua vyombo hivyo na tunaamini kwamba zipo dalili za kuweza kupata vyombo vya kuweza kutusaidia kuweza ku-*allocate* hivyo vyombo, kuweza ku-*allocate* maeneo mbali mbali ya watu, lakini pia kuweza kupata mfumo mzuri zaidi wa kuweza kutoa taarifa.

Na tuombe tu kwamba vyombo hivi vya baharini ni busara wakakaa na wenzetu wa *ZMA* kwa kuona wanafunga mitambo ile ya kisasa itakayowezesha kutoa taarifa pale ambapo kuna hitilafu ikiwa upepo ama majanga yoyote kuweza kupata taarifa mapema zaidi. Kufanya kinyume ya hivyo, itakuwa kama vile wewe unapendelea majanga yale ya kuficha bila ya kutoa taarifa katika maeneo husika.

Mhe. Spika, suala jengine limezungumzwa suala la uuzaji wa tiketi za mikononi, jambo hili ni suala mtambuka haliwezi tu kumalizwa na taasisi yetu ya *ZMA*. Suala la uuzaji wa tiketi linahitaji sisi kama serikali kwa umoja wetu tukutanishe taasisi zote husika ili tuweze kulidhibiti kwa ujumla wake. Tayari sisi kama mamlaka na kama wizara tumejaribu kutengeneza utaratibu mzuri wa kuona kwamba huuziwi tiketi mpaka pale utakapokuwa na kitambulisho ama uonekane kwamba wewe ni kweli unataka kusafiri, lakini bado kama zilivyo desturi za wahalifu wengine wanaendelea kubuni njia mbadala ya kuweza kuona kwamba anaweza kununua tiketi akafanya biashara bila ya kwamba hana kibali, hana utaratibu wala hana duka la kuweza kufanya biashara ya kuuza tiketi.

Sisi tunalichukua na tutahakikisha kawmba tunaweza kushirikiana na taasisi nyengine ikiwemo Jeshi la Polisi, Manispaa na taasisi nyengine *ZRB, TRA* ili kuweza kuona namna gani tunaweza kushirikiana katika udhibiti wa jambo hili. Jambo hili ni biashara ya magendo, taasisi moja hatuwezi kulifanya tukalikomesha lazima tushirikiane.

Mhe. Spika, suala jengine limeuliziwa hapa suala la kupanda kwa bei ya nauli, ni kweli kuna baadhi ya vyombo vimepandisha bei za nauli na wametoa taarifa kwa vyombo husika na sababu zao za msingi wamezieleza ikiwemo kupanda na kushuka kwa sarafu ya Tanzania, kupanda na kushuka kwa huduma za uendeshaji, kupanda na kushuka kutokana na tozo na kodi nyengine, lakini pia taratibu na uendeshaji wa vyombo husika nao pia gharama zao zimepanda.

Kwa hiyo, sisi kama serikali tunaratibu kwa ukaribu sana kuona kwamba upandaji wa bei lazima uje kwa mujibu wa taratibu na sheria. Na ukiwa umekidhi vigezo sisi kama serikali tutaruhusu na kama itakuwa upandishaji wa bei umekwenda kiholela, nalihakikishia Baraza lako hili tukufu tutazuia chombo hicho kisiweze kufanya safari. Lakini kama utakuwa upandaji wa bei umetokana na vielelezo vya msingi hatutokuwa na sababu ya kuzuia chombo hicho kisiendelee na safari.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni suala la *MV*. Maendeleo kuweza kufanya safari zake inaonekana kama vile ina hitilafu. Ni kwamba tumeshazungumza na wenzetu wa *ZMA* watatengeneza utaratibu maalum wa kwenda kukikagua chombo hicho na ikibidi kuwa na mapungufu watachukua hatua, na wakibaini kwamba hakuna mapungufu chombo hiki kitaendelea na safari zake kama kawaida. Aidha, tayari wao wenyewe meli ya *MV*. Maendeleo kwa mujibu wa ratibu yake wamekusudia tarehe 20/07/2015 kwenda chelezoni nchini Kenya katika Mji wa Mombasa kama ilivyo desturi. Katika kipindi hiki ambacho wanaendelea na safari za ndani tayari watakuwa chini ya uangalizi wa *ZMA* wakibainika kwamba kuna

tatizo watazuia, na kama kutakuwa hakuna tatizo wataendelea na safari zao kwa mujibu wa ratiba yao kama ilivyo kawaida.

Mhe. Spika, suala jengine ilikuwa ni suala la ongezeko la mapato yanayotokana na tozo mbali mbali zinazotozwa na Mamlaka ya Usafiri Baharini. Ongezeko hilo linatokana na mamlaka kupatiwa fedha kutoka serikalini kwa ajili ya kuipangisha Ofisi ya Mamlaka.

Mhe. Spika, ni sote kama tunavyokumbuka kwamba mwaka jana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea mwaka 2007 ilikuwa tuna mkataba baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kupitia Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wakati huo na Kampuni ya Malinzi ambapo mwaka jana serikali ilifanya maamuzi yaku-*terminate* mkataba husika. Baada yaku-*terminate* mkataba husika serikali ilifanya maamuzi ya kuanzisha ofisi yake wenyewe binafsi katika Mji wa Sharja ambapo ili tuweze kuanzisha ofisi hiyo, serikali ililazimika kutoa fedha maalum kwa ajili ya kwenda kuanzisha ofisi hiyo. Kwa hiyo, ongezeko hili la fedha linatokana na fedha hizo ambazo imepatiwa mamlaka kwa ajili ya kwenda kuanzisha ofisi huko nchini Sharja.

Mhe. Spika, suala linalofuata lilikuwa ni suala la kukatisha mkataba baina ya *Filtex*, kwa nini serikali ilivunja mkataba, je, kuna deni ambalo serikali inadai au inadaiwa na je, kuna madhara yaliyosababisha kwa serikali.

Mhe. Spika, serikali ilivunja mkataba na *Filtex* baada ya kampuni hiyo kusajili meli za Iran kinyume na vikwazo vya Umoja wa Mataifa. Hadi sasa hakuna madhara aliyopata serikali, mpaka serikali inakatisha mkataba ilikuwa inaidai *Filtex* dola za Kimarekani 121,336. Kutokana na agizo la serikali kazi ya usajili wa meli za kimataifa itafanywa na mamlaka ya *ZMA* yenyewe.

Mhe. Spika, pengine athari kubwa zaidi ambayo serikali itakuwa imeipata ni kule kuonekana kama kwamba Serikali ya Tanzania ama Serikali ya Zanzibar hatukutii yale maelekezo yaliyotolewa na vyombo vya kimataifa (*UN*).

Mhe. Spika, pia kulikuwa kuna hoja ambazo zilielekezwa katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Hoja ya kwanza ilikuwa inauliza suala la uwepo au kutokuwepo kwa mpango mkuu yaani *master plan* ya *airport*.
Ni kweli kwamba katika mwaka 2008 serikali iliandaa mpango mkuu kwa ajili ya viwanja vya ndege vya Zanzibar, lakini sote tunaona mabadiliko ya kisayansi na mabadiliko ya kidunia, wizara pamoja na *ZMA* tumeona kwamba ipo haja na ulazima wa kuweza kuiboresha *master plan* ile. Kwa hiyo, *currently* hatuna *master*

plan, ukitoa ile mwaka 2008 na malengo yetu ni kutaka kutengeneza *master plan* ambayo itaendana na mahitaji na malengo yetu angalau kwa miaka 30 ijayo mbele.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni suala la eneo la uwanja wa ndege kwamba ni dogo. Ni kweli kwamba ukiangalia hati ya mwaka 1997 eneo lile lina takriban hekta 550, na ukiangalia namna ambavyo limetumika takriban tumetumia nusu tu ukielekea ule upande wa kusini mwa eneo zima la uwanja wa ndege.

Mhe. Spika, suala jengine lililouliziwa suala la mfumo wa mabadiliko ya masaa ya wafanyakazi kwamba wanatoka masaa manane kwenda masaa 12.

Utaratibu huu ni utaratibu wa kawaida katika sekta hii ya viwanja vya ndege. Utaratibu huu pia una faida kwa wale watumishi wa viwanja vya ndege. Mamlaka imefanya mabadiliko haya baada ya kuona mfano uliopo katika uwanja wa kimataifa wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere Dar es Salaam, lakini pia kwa uwanja wa Kilimanjaro.

Faida yake kubwa unamuwezesha mfanyakazi kuweza kuendana na yale masaa yanayotakiwa, yaani masaa 40 kwa wiki ama masaa 160 kwa mwezi.

Katika utaratibu huu ukifanya kazi masaa 12 tunakupa wewe nafasi ya kuwa na mapumziko ya siku tatu katika wiki, ukifanya kazi katika mfumo wa kawaida wa masaa manane unakupa wewe mfanyakazi siku mbili za mapumziko na siku tano utafanya kazi katika muda wa wiki.

Kwa hiyo, mamlaka imejiridhisha kwa kuona kwamba itawapa nafasi kubwa zaidi wafanyakazi wao siku tatu za mapumziko na siku nne watakuwa wanafanya kazi, lakini kubwa zaidi itawaondoshea sasa zile *shift* za usiku, kwa maana ya kwamba ukiingia saa moja utatoka jioni unakwenda kupumzika na anayeingia jioni atatoka asubuhi kwenda kupumzika, kinyume yake maana yake atakayeingia jioni angepaswa kutoka saa nane usiku jambo ambalo lingeweza kupelekea usumbufu huko anakokwenda ama kuweza kumpatia shida katika harakati za usafiri.

Mhe. Spika, suala jengine lililoulizwa na Mhe. Farida Amour ilikuwa ni mradi wa uwekaji wa taa kwa Pemba. Jambo hili tayari tumelizungumza takriban mara nne katika kikao hiki kinachoendelea. Suala la taa limeulizwa mara mbili kwa swali la msingi tumejibu na tumeulizwa maswali ya nyongeza matatu kwa sita, lakini kwa sababu tunataka kujenga uelewa mpana tutaendelea kulisema.
Mhe. Spika, nimthibitishie Mhe. Mjumbe kwamba serikali ina dhamira ya dhati ya kuweka taa katika uwanja wa ndege wa Pemba.

Malengo ya serikali ni kuona tarehe 30 mwezi huu mradi uwe umekamilika na hatua tayari zimeshachukuliwa. Vifaa vya awali vya nyaya tayari vimeshafika Pemba, harakati za uchimbaji tayari zimeanza, vifaa vya pili tayari vishafika Dar es Salaam, wajenzi hawa kwa maana ya Kampuni ya *SafeGate* inaandaa utaratibu wa kusafirisha kutoka Dar es Salaam kwenda Pemba ili zikaanze kufanywa.

Tulikuwa tuna kasoro ya fedha, tayari serikalini tumeshaletewa fedha kwa ajili ya mkandarasi wa ndani kwa uimarishaji wa huduma za umeme pamoja na miundombinu mingine.

Madhumuni ya serikali ni kuona kwamba mapema iwezekanavyo mwezi wa saba jambo hili tuweze kusahau na tuanze kuandika historia, kwamba uwanja wa ndege wa Pemba ulikuwa hauna taa sasa hivi unatoa huduma ya kuweza kutua ndege asubuhi na mchana, kuwe na wingu, kuwe na mvua, usiku na mchana wake. Nataka nimthibitishie Mhe. Mjumbe kwamba serikali kwenye hili wala hatutanii.

Suala jengine alikuwa anaulizia adha na kero wanayoipata abiria katika uwanja wa ndege wa Pemba. Mamlaka imelipokea na tayari wameshaandaa mchoro wanafanya marekebisho maalum kuweza kujikinga na jua, kuweza kuweka vipoza hewa ili wasafiri wanaotumia uwanja wa Pemba na wao waweze kupata huduma nzuri kama vile abiria wanaopata huduma hizo katika kiwanja cha Unguja.

Aidha, kulikuwa na suala la ukosefu wa mashine ya ukaguzi. Ni kweli katika uwanja wa Pemba tuna tatizo hilo hatuna mashine ya ukaguzi, lakini serikali kwa kuliona hilo kwa kupitia mamlaka tayari kwa kuwa Unguja tuna mashine takriban nne, tumeshaandaa mashine moja maalum itaondoka katika uwanja wa ndege wa Unguja itakwenda Pemba kwa ajili ya kutoa huduma za ukaguzi katika uwanja huo wa Pemba.

Mhe. Spika, suala jengine aliuliza Mhe. Jaku Hashim alizungumzia suala la abiria wanaowasili kwamba wanapata tabu, wanapata shida. Suala hili pia Mhe. Jaku yeye mwenyewe ameuliza katika swali la msingi, ameuliza katika swali la nyongeza zaidi ya mara mbili na majibu yako vile vile, kwamba lengo la Mamlaka ni kuona tunatengeneza mfumo mzuri wa ile ile *passing* ya *flow*, kuona kwamba anayewasili na anayeondoka hawakutani; ili kuliona hili vizuri tayari Mamlaka wameshaandaa eneo zuri zaidi upande wa kusini, na kama atakwenda hivi sasa ataona kuna ujenzi unaendelea. Eneo maalum kujenga kipaa kwa ajili ya wanaosubiri wageni, lakini hata wale wanaowasili waweze kupata eneo la kuweza kujikinga na jua ama mvua kwa ajili ya kufuata magari yao katika maeneo ya maegesho. Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Mjumbe akubaliane na utaratibu ambao ameukuta unapangwa katika maeneo haya. Si vibaya kutoa mawazo, na sisi kama serikali tumeyasikia, lakini tungemuomba angezitii na angeufuatilia ule utaratibu

ambao umeelekezwa pale basi ulikuwa na malengo ya kuimarisha na kuboresha huduma nzuri zaidi kulikoni kuona tu, kwamba uoni wake yeye ndio uwe sahihi kuliko yale ambayo yamepangwa na wenzetu hawa wa Mamlaka.

Suala jengine lililouliziwa na Mhe. Jaku Hashim ni suala la mabasi kwamba mabasi yale mabaya hayafai kuchukua abiria. Lakini labda tuulizane suala la msingi kwamba kiutaratibu suala la kubeba abiria lingepaswa kufanywa na kampuni husika (*Ground Handling*) ambayo kwa hapa Zanzibar ni Kampuni ya *ZAT*, lakini sote tunajua kuwa takriban miezi sita iliyopita nyuma tulikuwa tunaendelea na ujenzi wa *apron na taxiway* na huduma hizi zilikuwa zinakatwa kusini mbali.

Mamlaka baada ya kuona kwamba athari hizi zikirudi zitapelekea serikali kulaumiwa ndipo ilipoamua kwenda kutupa mabasi kwa ajili ya kutoa huduma za abiria, jambo ambalo haukuwa wajibu wao wa msingi. Walifanya hivyo kwa ajili ya kuisaidia serikali kujikinga na lawama.

Mhe. Spika, mabasi yale yametumika baada ya kukamilika ujenzi wa *apron* na *taxiway*, tayari mabasi yale yanatumika kwa malengo yake ya msingi ambayo ilikuwa ni kuchukua wafanyakazi wa mamlaka ya uwanja wa ndege. Kwa hiyo, mabasi yale hayakununuliwa kwa ajili ya kuhudumia abiria, mabasi yale yamenunuliwa makusudi kwa ajili ya kutoa huduma kwa wafanyakazi wa mamlaka ya viwanja vya ndege.

Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Mjumbe tuwaombe wenzetu wa *ZAT* kama kauli zao ziko sahihi wanatueleza kwamba mabasi maalum ya kubebea abiria yapo Dar es Salaam, tuombe kauli yao hii iwe ya ukweli wayalete kwa lengo la kutoa huduma kwa watumiaji wetu wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume uliopo Kisauni Mjini Unguja.

Mhe. Spika, hoja nyengine zilikuwa za Mhe. Hija Hassan na Mhe. Saleh Nassor Juma kuhusu uajiri wa wafanyakazi. Sote mashahidi serikali katika mwaka 2011 kutokana na mabadiliko makubwa sana ya Sheria Nam. 2 yanayohusiana na suala zima la uajiri ama wafanyakazi katika sekta za umma, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege inalazimika kufuata utaratibu huo na kama mamlaka inalazimika kufuata utaratibu huo maana yake kwamba utaratibu wa nafasi mpya za ajira lazima zitangazwe, zitolewe taarifa, wanaoomba waombe, wafanyiwe usaili, anayefaulu aweze kushinda na aajiriwe serikalini. Lakini kwa kuwa hawa sisi tumesema wana sifa, wana uzoefu, hofu yao ya kuomba ni nini? Kwa sababu ukiwa na sifa za ziada maana yake ukienda kwenye usaili wewe utashinda. Kwa hiyo, sisi tuwashajihishe waende wakaombe, wakafanyiwe usaili, na kwa sababu wao wana sifa tusijenge hofu, watashinda usaili wataajiriwa na serikali, ili kuendana na matakwa na

utaratibu ambao sisi Wawakilishi tumeuasisi kwa kuona kuwa utaratibu wa kuajiriwa unakwenda kwa mfumo wa kutangaza ajira, na hiyo Mamlaka ndio inayotekeleza kama vile ambavyo sheria inavyoelekeza.

Mhe. Spika, suala jengine lilikuwa ni abiria kunyang'anywa *perfumes* ama kitu kingine chochote kinachohatarisha usalama. Malengo ya kukizuia ni kwamba wewe usipewe kile chombo ama iwe *perfume*, ama iwe kisu, iwe uma, iwe kijiko, ni wewe kujikinga na kile kitu kupita nacho kwenye ndege. Kwa hiyo, wanapokichukua wanakiweka ikifika muda wa kukiharibu watakiharibu, utaratibu huu sio kama upo Zanzibar tu, bali ni dunia nzima, ukienda na kitu chochote cha hatari katika uwanja wa ndege watakunyang'anya watakihifadhi wao utaendelea na safari zako, ukifika muda wa kukiharibu watakiharibu ama wata-*destroy.*

Mhe. Spika, suala jengine ilikuwa ni suala la ndege zetu kutumia rubani mmoja. Kiutaratibu ni kwamba ndege yoyote ambayo iko chini ya *pound* 12,000 inaruhusika kwa mujibu wa taratibu za kisheria kurushwa na rubani mmoja, haimkatazi mmiliki wa ndege iwe kampuni au mtu binafsi kuwa na marubani wawili, lakini pia sheria haimlazimishi mmiliki iwe mtu binafsi au kampuni kulazimika kuwa na marubani wawili, kimsingi ndege hiyo itakuwa iko chini ya uzito ule wa *pound* 12,000 ambayo takriban tani tano.

Kwa hiyo, sheria inaruhusu, tungeweza kushajihisha kwamba ndege hizi zitumiwe na marubani wawili lakini sisi tunachoweza kufanya ni kushajihisha, hatuna mamlaka ya kisheria ya kulazimisha hilo lifanywe kwa sababu sheria inampa nafasi ya kuweza kuamua, ama kufanya ama kutokufanya.

Mhe. Spika, masuala mengine yalielekezwa katika Shirika la Meli na Uwakala na jambo kubwa lililozungumziwa ni suala la Meli ya M.V Maendeleo. Tayari tumelitolea maelezo kwamba meli hii sio mbovu ni nzima, na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Baharini inairatibu meli hii na meli nyengine zote kama kuna kasoro tutazizuia mpaka pale kasoro zitakapowekwa sawa ili ziendelee kutoa huduma ya usafiri kwa abiria wa baharini.

Suala jengine ilikuwa ni uuzaji wa tiketi, tayari tumelitolea maelezo. Kuongezeka kwa mapato na matumizi. Mapato na matumizi yanaongezeka kwa ujaji wa meli mpya, yaani ukiangalia mapato yaliyoongezeka katika mipango ile ya kitabu cha bajeti yanatokana na *projection* ambazo tumezitegemea kwamba itakapokuja meli mpya maana yake tutakuwa tuna mapato yanayotokana na meli mbili. Bila shaka mapato yatakuwa yameongezeka.

Jengine ilikuwa ni uendeshaji wa meli ya MV. Mapinduzi/Maendeleo kuwezesha shirika kumudu kununua meli nyengine. Kipindi hicho chote tuliweka mkazo zaidi kwenye kutoa huduma kwa wananchi zaidi kuliko kujiendesha kibiashara.

Baada ya kuona kwamba kipindi chote hicho shirika hili lilikuwa likijiendesha katika mfumo wa kutoa huduma tayari serikali imetoa maelekezo maalum ya kulifanyia *reforms* shirika hili na kuona kwamba sasa linajiendesha kibiashara.

Baada ya kufanya *reforms* hiyo imani yetu kwamba yale ambayo wamekuwa wakilalamikia Waheshimiwa Wajumbe hapa kwa kuona kwamba meli moja inazalisha meli nyengine yatakuwa yamefika kikomo. Shirika hili likiwa limefanyiwa *reforms* bila shaka kipato na mfumo mzima wa kibiashara utakuwa umeimarika, twabaan itakuwa kuna nafasi ya kuweza kununua meli nyengine.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niseme naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri kwa kutoa mchango huo na kuunga mkono hoja. Kabla sijamkaribisha Mhe. Waziri naomba wale Waheshimiwa Wajumbe walioko nje wajitahidi warudi ndani, niwaombe wasaidizi wetu, wanadhimu, wasaidie kuwaita Wajumbe ambao hawajafika hapa ili waweze kuja tumalize shughuli hii.

Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: *Bismillahi Rahmani Rahiim*. Mhe. Spika, naomba nikushukuru tena kunipa nafasi kuja kumalizia sehemu ambayo ameiacha naibu wangu, ambaye kwa muda wake aliokaa Wizara ya Miundombinu ni mwenyeji aliyekomaa zaidi kuliko mimi, na kwa sababu ni msaidizi wangu, nimempa nafasi ya kujibu hoja zile zinazohusu zaidi mashirika na mamlaka yaliyo chini ya wizara yetu, na kwa ufasaha na uchambuzi mkubwa amefanya, namshukuru sana. (*Makofi*)

Ni bahati mbaya kwamba baadhi ya hoja alizokuwa akizijibu Wajumbe waliozitoa walikuwa bado hawajafika. Sasa pale tunapopitisha vifungu mtu akataka kupiga buti tunaweza kumwambia kwamba mzee ulikuwa hupo.

Mhe. Spika, naomba nianze kwa kutaja na kuwatambua wale ambao wamechangia. Lakini kabla ya hapo niwashukuru tena Wajumbe wote wa Baraza hili na wale waliokuwa hawakuchangia kwa mashirikiano yao na maoni mengi waliyoyatoa.

Sina hakika kwamba nina bahati, naona wengi leo wamekuwa wakitupongeza na kutuunga mkono kwa kazi ambayo tumeifanya. Kwa kweli kazi hii sikufanya mimi, isipokuwa mimi na watendaji wangu na kwa kusaidiwa na Mhe. Naibu Waziri wangu, pengine kazi nyengine zilikuwa nusu zimekamilika zilizofanywa na Waheshimiwa Mawaziri waliopita.

Mhe. Spika, lakini kwa vyovyote ile hali iliyoelezwa hapa ilikuwa ya kutia moyo zaidi kwangu, mimi kama waziri na zile lawama nyingi na kama unakumbuka Mheshimiwa kuna wakati hotuba au bajeti ya wizara hii ilikuwa mpaka upitishe hekima zako.

Nategemea leo haitokuwa hivyo, kwa sababu mambo mazuri na asubuhi niliona umechangamka sana hapa, na kucheka kuona leo labda nitapata bashasha ya kupitisha wizara iliyokuwa ina migogoro na watu.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo kwanza kuna Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi inayoongozwa na Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa, ambayo kwa niaba yake ilisomwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Tunaomba kuwashukuru kwa taarifa na maelekezo na maoni yao kwa wizara.

Pili, naomba kumtambua Mhe. Makame Mshimba, Mwakilishi wa Kitope ametupamba sana isipokuwa alichelea tu kontena lisimuangukie wakati akipita barabarani linaenda mbio.

Wa tatu alikuwa Mhe. Abdi Mosi Kombo na yeye tunamshukuru. Mwengine alikuwa Mhe. Salim Abdalla Hamad wa Mtwambe, Mhe. Hamza Hassan Juma nae pia alitupongeza na kutushukuru na kutupa moyo.

Mhe. Farida Amour Mohammed yeye wa viti maalum alitupongeza na kutoa dukuduku lake juu ya Bandari za Pemba. Lakini naona Mhe. Naibu Waziri ameeleza kwa ufasaha hatua tunazotegemea kuzichukua.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub naye alitoa mchango na kutoa maoni yake na akaona uchungu kwamba kule Hospitali ya Mnazi Mmoja kuna mashimo nayo ya kwenda kuzibwa na Idara yetu ya barabara.

Naomba nimtambue tena Mhe. Viwe Khamis Abdalla, naye alizungumza kwa uchungu barabara iliyokuwa imeahidiwa na Mhe. Rais, Dkt. Ali Mohamed Shein kwamba mpaka leo haijajengwa. Majibu ni kwamba hiyo imo katika hatua.

Mhe. Saleh Nassor Juma na yeye kwa ukali na uchungu kidogo ameonesha mawazo yake juu ya hali ya Bandari za Pemba na tumeeleza kwa kiasi fulani nini tutafanya.

Mhe. Panya Ali Abdalla naye tunamshukuru.

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma yeye ana faraja kwamba mambo yake mengi Jimbo la Bumbwini yamenyooka isipokuwa alikuwa na wasi wasi tu wa daraja mbovu zile za Kaskazini A.

Mhe. Mwajuma Faki Mdachi naye tunamshukuru yeye kashughulikia na mambo ya *ZANTEL* na simu zile na mambo mengine ya Pemba kuhusu barabara.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa yeye kwa sababu ni mshirika wa Kamati ya Miundombinu ametueleza baadhi ya mambo, tunamshukuru mwingi ulikuwa ni ushauri.

Mhe. Abdalla Mohd Ali na yeye ametoa maoni yake tunamshukuru. Mhe. Fatma Mbarouk Said yeye alitupa kwa maandishi.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na yeye alisema suala kubwa linalohusu mashimo ikiwemo lile la pale Mpendae kwenye *round about,* na nilivyoambiwa na watu wangu tayari limeshazibwa.

Mhe. Ashura Sharif Ali alisema kwa ukali juu ya daraja zinazokwenda njia ya Bububu kwenda Mkokotoni, na alifika hata kusema hata kwenye lile daraja lenyewe kati kati ya barabara kuna shimo. Ni suala ambalo linasikitisha lakini nalo tutatoa maelezo.

Mhe. Marina Joel Thomas yeye ni Mjumbe wa Kamati amejaribu kutusaidia kutoa maelezo na mwisho ni Mhe. Naibu Waziri wangu ambaye na yeye namshukuru kwa kufanya uchambuzi.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo ukiuliza mjadala uliokuwepo pamoja na hoja nyingi zilitoka kutokana na mashirika, lakini hoja nyingi hasa zilikuwa kwenye Programu ya Ujenzi wa barabara na usafiri wa nchi kavu.

Sasa mimi nitaomba nichukue muda kidogo kutoa maelezo ili tusaidie kutoa ufafanuzi pale panapohusika, na kama kutakuwa mahali tumesahau hoja si dhamiri yetu lakini tulikusudia kueleza ili tusichukue masaa marefu, tunahitaji kumpisha mwenzetu Waziri wa Biashara na yeye atabaruku.

Mhe. Spika, kuna suala lililoulizwa la usafirishaji wa makontena barabarani wakati wa mchana. Utaratibu wa magari haya kutembea usiku unaandaliwa kwa kushirikiana na taasisi husika.

Naibu Waziri amesema hapa kwamba hakukuwa na tatizo la kusafirisha makontena hayo usiku. Lakini mara nyengine lazima kijulikane mle ndani mna nini, ndipo kiruhusiwe na wenzetu watu wa usalama wametwambia si kila kitu kinaweza kusafirishwa usiku katika hali ya nchi yetu hivi sasa ilivyo katika suala la makontena.

Lakini tunamuomba Mhe. Makame Mshimba kwamba lile lililotokea halitatokea, na tutawaeleza madereva wahusika na hatua kali watu wetu wa usalama barabarani wanaohusika na usafiri wa nchi kavu kulitizamia hali hiyo, na ikilazimika hata dereva kumzulia leseni maana inaweza ikatokea balaa.
Mhe. Spika, kulikuwa na hoja ya uvunjwaji wa sheria za barabarani, kuendesha mwendo wa kasi ambalo linahusiana na lile la makontena.

Wizara kupitia Idara ya Usafiri na leseni ina jukumu la ukaguzi na upasishaji wa magari na madereva. Wizara itaendelea kushikiriana na vyombo vya dola kusimamia usafiri wa barabarani. Suala hili naomba ningojee pale nitakapoeleza mambo ya daladala kwa jumla nilichambue zaidi. Lakini kwa jumla tutashirikiana na jamaa wa usalama barabarani kushughulikia hili, maana moja katika sababu hii ndio inayosababisha ajali nyingi. Lakini ajali nyingi zinazotokea zina Mtambuka kuna mambo mengi yanayotokea.

Kulikuwa na suala la upatikanaji wa mkopo kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Wete-Chake. Hili nadhani liliulizwa na Mhe. Salim Abdalla. Tayari serikali imeshatiliana saini mkopo na Benki ya Badea na taratibu za upatikanaji wa mkopo kutoka *Saudi Fund* zinaendelea.

Wizara imeanza kufanya mazungumzo na *BADEA* kuangalia uwezekano wa kutumia fedha zilizopo kuanza utekelezaji wa mradi huo wakati tukisubiri mkopo kutoka *Saudi Fund*. Yaani kulikuwa na fedha ambazo zilibaki walizotupatia kwa miradi ambayo imekamilika kama italazimu basi tuanze na hizo tunaomba ruhusa ili zile nyengine zitakapokuja ile shughuli imeendelea.

Kwa hivyo, ile barabara ya Wete- Chake si kama nayo itakaa kama kukosa Mhe. Farida itakuwa kama vile wimbo, haitakuwa wimbo itaanza kuendelea. Lakini barabara zile zilikuwa ni tatu Wete-Gando na Wete-Konde pamoja na hii Wete-Chake zilikuwa ni pamoja lakini zilikamilika zile mbili, hii moja nayo itapata fedha itaendelea.

Suala lililosemwa kwa uchungu na Wajumbe wengi hasa kutoka wenzetu Pemba ni suala la fidia za barabara hasa tatu za Kaskazini Pemba. Tunavyoelewa sisi kuna nyumba sita katika barabara ya Finya/Mapofu zilifanyiwa tathmini ili kuziondoa kupisha ujenzi wa barabara, lakini baadaye ilionekana kwamba nyumba hizo ziko mbali na barabara na wala hazitoathirika.

Hata hivyo, baada ya ujenzi kukamilika wizara inaifanyia juhudi ya kuangalia kama kuna athari yoyote itajayojitokeza, na kama itathibitika kuwepo kwa athari zilizotokana na ujenzi wa barabara hizo wizara italizingatia na wananchi hao kulipwa fidia. Hatuna nia ya kuwadhalilisha au kuwanyima wananchi wa Pemba nafasi ya umasikini wao walipokuwa wakiishi eti tu kwa sababu tunapitisha barabara, lakini barabara vile vile ni muhimu kwa sababu ikijengwa inatufaa sote.

Mhe. Spika, napenda kulieleza suala hili kwa kutoa mfano wa kuwashukuru na kuwapongeza watu wa Umbuji. Kila mara huwa nalitolea mfano na karibuni tulikuwa na Mhe. Rais mahali tunakagua uwanja wa ndege nikamwambia tena Mhe. Rais kama vile walivyo watu wa Umbuji, akaniuliza Mhe. Rais vile watu wa Umbuji nimesahau, watu wa Umbuji walipotaka kujengewa barabara yao ambayo tumeifungua nayo ilikuwa inapita kati kati ya miti; michungwa, miembe, mishelisheli na miti ambayo na unajua baraka kubwa ya Umbuji ni machungwa.

Sasa katika kutaka kufanyiwa malipo walipata mzee gani sijui mwenye hekima akasema nyinyi kateni kama mia kama ishirini, kama thalathini sisi haja yetu barabarara, yaani walisamehe kabisa miti yote ile kwa kuzingatia kwamba walikuwa na tatizo la barabara.

Ni suala la kupongezwa sana kwamba hawakuweka mbele suala la kupata malipo ya vipando, waliweka mbele kupata barabara, na hivi sasa barabara ya Umbuji kama mgongo wa ngisi, laini *alhamdulillah*, na yale machungwa na vitu vyengine vinapata urahisi kuletwa mjini kwa utaratibu.

Sasa tunaomba na wale wengine tunapojenga barabara hizi, kwa sababu wanatumia watu wengi na sisi pamoja mengine tuzingatie katika misingi hiyo ili kuipunguzia hasara Serikali. Malipo ya fidia ni makubwa sana lakini na lazima barabara tuzijenge, hatutadharau, tutawalipa wananchi kile kinachostahiki baada ya kufanya uchunguzi wa kina juu ya hali hiyo.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ni muhimu katika haya niliyokuwa ninayasema ni upatikanaji wa eneo jengine kwa ajili ya kituo cha daladala na hatima ya kituo cha sasa kiliopo ambacho kinasumbua sana, maana pale Ofisi ya Makao Makuu ya CCM imekuwa kama badala ya Darajani imekuja pale.

Mhe. Spika, nilipofika Wizara ya Miundombinu changamfu ya akili yangu ilikuwa ni suala hili. Maana ilikuwa maamuzi ya serikali yameshafanyika kwamba kituo cha Darajani kihame na kilikuwa lazima kihame, kwa sababu Mhe. Spika, lugha hii nadhani utaifahamu mji wa Zanzibar umecheuka, yaani ule uwezo wake wa kubeba magari na watu inazidi uwezo wake, na hali ilivyo pale Darajani hivi sasa tumeona tumehama kwa sababu pana-*park* magari. Lakini ilikuwa pahali panapo hatari kama vile tunavyoona ilipo hapa Kisiwandui mbele ya Makao Makuu ya CCM.Kwa hivyo, suala la uamuzi wa kuondoka kituo lilishafanywa suala baada yake ni wapi hasa haya maegesho.

Baada ya pale nilikutana na Waziri mwenzangu wa Tawala za Mikoa ambaye aligundua kumbe kisheria suala lile liko chini ya Miundombinu wala haliko kwenye Tawala za Mikoa. Tukakutana sote na Mkuu wa Mkoa Mjini, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Polisi wanaoshughulikia na usalama na wadau wengine wote, hata wale wanaoendesha daladala tukachukua kama masaa matatu Wizara ya Miundombinu kulijadili. Na baada ya hapo nikaachiwa kazi nifanye mimi kama waziri na watendaji wangu. Nikawaita watu wa Bodi ya Usafiri wa Nchi kavu kwamba wafanye mapitio upya, wakapita kituo kimoja kimoja kila kinachohusika na kufanya udurusu huo na wakaja na mawazo mapya wizarani.

Lakini baada ya hapo tukaona haitoshi tukutane na semina na wanafunzi akafungua Mhe. Naibu Waziri wangu Bwawani pale wakaeleza malalamiko yao, tukafanya semina nyengine Baraza la Wawakilishi la zamani na wadau wote ikawa ni mjadala mkali, na mwishowe tukafanya majadiliano na Kamati ya Miundombinu na Mawasiliano ya Baraza la Wawakilishi tuje tufanye sasa Mhe. Spika.

Kamati ya Baraza la Wawakilishi ikasema kunahitaji kufanywa semina ya pamoja wadau wote pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, na nakumbuka Mhe. Spika, ni shahidi wiki iliyopita tarehe 16 kama sijasahau tukafanya semina hapo juu wakawepo watu wote, bahati mbaya Wajumbe wengine walikuwa na dharura hawakuweza kuja,lakini mjadala nao ulikuwa mzuri na mkubwa na tayari nimeshaandika ripoti kamili sasa kwa kuzingatia maoni ya wote wale wengine pamoja na maoni ya hao tuliokutana tarehe 16, na nategemea kufikisha ripoti hiyo serikalini ili kupata maamuzi ya mwisho mabadiliko yaweje.

Lakini kuna masuala mawili matatu, yaliyojitokeza katika kuzingatia hayo ni kwamba hivi sasa tatizo kubwa si kama pale Darajani tu na Makao Makuu ya CCM kukusanyika daladala. Tunaweza kuziondoa pale daladala tukazipeleka hapo pengine tunaposhauri, lakini bado kuna matatizo ya watu wanaotoka Bububu kufika Hospitali ya Mnazi mmoja. Kwa sababu ya hali ya sasa wanatakiwa washuke hapa karibu na Polisi *station* Malindi kwenye Jumba la Baraza la Mji, na watu wanatoka huku juu Kidongo Chekundu, Mwera, Kiembe Samaki na wao

wanataka wafike pwani kwenye boti, wale jamaa zangu wanaotoka Bububu wanashuka pale kwa Bakhressa kuna kituo anabeba kibegi chake masikini anakata barabara anakwenda zake pwani kwenye boti, akirudi pwani anakuja pale anangoja daladala anakwenda zake. Lakini anayetoka Kidongo Chekundu akiitaka pwani anapata tabu sana. Maana inabidi ashuke pengine Haile Selassie halafu aende kwa miguu, na akitoka pwani aburure na watoto aje zake mpaka Haile Selassie au hapo kwenye Makao Makuu ya CCM ndipo apate kwenda ng'ambo.

Kwa hivyo, kuna tatizo hilo la msingi si ya maegesho tu lakini na njia gani zaidi zinatakiwa kuwapunguzia wananchi hawa katika kutaabika kwenye daladala. Unaweza ukamshusha mtu Darajani anataka Hospitali ya Mnazi Mmoja ni mbali, kuna mtu wa Kidongo Chekundu anashuka Haile Selassie anaitaka Mnazi Mmoja ni mbali. Kwa hivyo, si suala rahisi kama tunavyoliona, maoni yote hayo Mhe. Spika, tumeyazingatia na tutapeleka serikalini maoni ambayo yanaweza kutupa ufumbuzi wa kudumu.

Lakini hata hivyo nilitegemea wakati Waziri wa Ardhi anapowasilisha ripoti yake labda bado lakini kuna *Master Plan* kamili ya mji na wapi pawe pahali pa kudumu kama ni *city centre,* nadhani tumeshalizingatia hilo serikalini ili kuondoa tatizo hili. Lakini nadhani wakati wake bado Mhe. Waziri hakulisema na mimi sina madaraka ya kueleza hilo. Kwa hivyo, suala hili linashughulikiwa na tunaomba tustahamiliane mpaka tutakapopata ruhusa. Tatizo la Makao Makuu ya CCM kuwa na *congestion* nategemea litaondoka baada ya maagizo mapya ya serikali.

Mhe. Spika, lakini kuna tatizo jengine ambalo limeelezwa na Mhe. Hija Hassan Hija hapa la kwamba watu hutumia nafasi za pembeni ya barabara kuweka makontena ya biashara au ku- *park* magari pembeni, mule mulitegemewa muwe wanapita wananchi kwa miguu. Siku hizi wananchi wanapata tabu inabidi baada ya kupita pembeni mwa barabara apite kwenye ile ile barabara akumbane na vidaladala vinavyokuja. Hili limekuwa ni tatizo sugu lakini lina matatizo ya aina mbili.

Lina matatizo kwamba wale wanaofanya hivyo wanavunja sheria na Polisi wanapowachukulia hatua wakifika Mahakamani hukumu za Mahakama zinakuwa ndogo na hilo pia linatokea kwenye suala la ajali hizi, akifanya mtu kazidisha abiria au akikamatwa na *Traffic* akipelekwa Mahakamani anatiwa adabu ndogo, kesho anarudi barabarani anamfanyia uchepe askari si ulinitia abadu wewe mbona bado natembea. Kwa hivyo, kunahitaji hata sheria yetu hii kuidurusu kidogo, na sheria kwa kweli sio mbaya maana mumeipitisha Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Juzi nilimsikia Mhe. Hamza Hassan Juma anasema kwamba sheria ile labda tumekosea, kuna mahali hata dereva akizidisha abira yule abiria aliyezidi na yeye alikuwa atiwe adabu, kwa sababu ilikuwa hastahiki kukubali kuingia katika gari iliyozidi. Lakini nayo iko laini au dereva kuwachukua abiria akawapeleka kituo cha Petroli wamo ndani akajaza petroli nayo pia ni makosa, na ilikuwa na adabu si chini ya dola kumi na tano. Lakini akienda Mahakamani anaambiwa toa elfu tano au kumi anarudi na jeuri. Kwa hivyo, suala hili linahitaji mashirikiano ya pamoja ili kulitatua.

La mwisho suala la nani anaruhusu kuweka makontena pembeni mwa barabara. Sisi kama watunza barabara sio kwa mjini hapa ni suala la Baraza la Mji, na juzi tulipokuwa juu hapo Mkurugezi wa Baraza la Mji alikuwepo na lilizunguzwa na alikuwa mkali sana na akasema atalishughulikia. Lakini lile kontena lilioko kwenye barabara ya kutoka Kinazini na kutoka Michenzani karibu na Muzzamil linaudhi bwana, na liko kwenye hatari. Maana ingekuwa si hapa kwenye spika basi ningeigiza jinsi wale madereva wanaotoka huku Michezani kutaka kuunga barabara ya kwenda Malindi inabidi mpaka akaribie kutokeza barabara inayotoka Kinazini ndipo aweze kutizama kwamba kule kunajuka gari au hakuji.

Sasa sijui kwa nini huyu aliyetoa ruhusu hakulizingatia hilo, lakini ni suala la Baraza la Mji na hawa wenzetu tunakutana nao na ikiwezekana lizingatiwe suala hili. Lakini tulivyoambiwa nasikitika kusema hivyo kwamba kulikuwa na mkono wa amri mahali. Sasa wapi huko sijui mimi, Mwenyezi Mungu anisamehe. Mhe. Spika, suala hili nadhani inatosha nilivyolieleza.

Kuna tatizo jengine matengenezo katika eneo la barabara ya ndani Hospitali ya Mnazi Mmoja. Hili alisema Mhe. Jaku Hashim Ayoub lakini tunaomba Mhe. Jaku Hashim afahamu kwamba Idara ya *UUB* ina mashirikiano mazuri sana na Idara ya Mnazi Mmoja. Tutashirikiana naye na hayo mashimo yakiwa yamo ndani ya Hospitali basi tutakwenda kuyaziba Mhe. Ashura Sharif kama tutakavyoziba yale mashimo mengine yalioko nje ya mji au yaliomo ndani ya mji na kule ni muhimu, na hivi sasa tunajaza viraka vingi kama mtapeleleza.

Mhe. Spika, juzi pale ninapokaa mimi Ofisini kwa *DPP* kulikuwa na shimo kubwa sana, sasa dereva wangu kila akipita pale anachokozwa na wafanyakazi wa *DPP* mwambie waziri wako bwana mshimo huo unatumaliza. Sasa juzi nimepita limeshatiwa lami dereva wangu alipata nguvu akaenda akawaambia kwamba hili halikuzibwa tu lakini limetiwa lami limefukiwa. Kwa hivyo, mashimo yanaendelea kufukiwa kulingana na uwezo wa Idara yetu inavyoendelea kufanya.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni ukusanyaji wa mapato katika Idara ya Usafiri na Leseni kutoka milioni mia tatu sitini na nne kwa mwaka mpaka bilioni moja

nukta moja sita. Suala hili lilionekana kwamba si la kawaida kutoka milioni mia tatu mpaka bilioni. Bahati nzuri tuna matarajio ya ongezeko la mapato kutokana na kubadilishwa ada mbali mbali zinazotozwa katika huduma zinazotolewa.

Kuna mabadiliko makubwa baada ya mwaka mpya kuanza, kwa hivyo tunategemea mapato hayo kuongezeka na ndiyo maana watu wetu wamezingatia hivyo, na ukipeleleza sasa magari nayo ni mengi kweli.

Mhe. Spika, adhabu ya papo kwa papo kwa hawa wanaofanya fujo ya kuendesha gari vibaya. Tunamaliza Kanuni tumezifikisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu askari wawe na haki sasa pale pale anapokukuta tatizo na adabu iwe pale pale. Lakini Mheshimiwa ni kweli ajali zimeongezeka na ajali zinaongezeka, kwa sababu madereva wanaoendesha gari ni watoto wadogo, wengine ni chini ya umri. Tatizo ni nini Mhe. Spika, ni vizuri kulieleza.

Mkurugenzi wetu wa Leseni za Barabara ana taratibu zake za kujaza fomu ili upate leseni. Sasa ukishapata leseni, karatasi ile ndipo unapokwenda *ZRB* kushughulikiwa kile kidude kama kikadi. Sasa kule *ZRB* hatusemi kwamba watu wanachakachua lakini kuna watu na kesi tunazo na hata hapa ninazo, mtoto wa miaka 18 anapewa leseni inayostahiki mtu wa miaka 25, na kesi nyengine tumezipeleka Mahakamani.
Sasa vijana hawa siku hizi huku hoteli za pwani Mhe. Spika, ni karibu sana, ikifika Jumamosi na Yarabi Salama Mungu tusamehe keshokutwa vunja jungu, sijui tena litavunjwaje na vijana hawa, wanakwenda huko mashamba wanakula huo muziki wao wa disko, wanakula vitu vyao tunavyovijua, wanarudi sasa kuendesha gari mbio wanaona ndiyo raha.

Na siku hizi ndiyo munakuta ile *T1* (inaitwa tako moja). Hawa vijana ndiyo wanaosababisha ajali nyingi kutokea.

Mhe. Spika, inabidi sasa askari wawe na nguvu ya kuwatia adabu wale wanaostahiki hata ikiwa pale pale anamkamata.

Kulikuwa na hoja ya uchimbaji wa kifusi katika mradi wa barabara Ole/Kengeja. Suala hili linafanyiwa kazi kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira na tumeshawahi kukutana na Mheshimiwa na ninakumbuka karibuni Mhe. Waziri alizungumza hapa kwamba katika kulirekebisha eneo, unachukua ile *layer* ya juu ambayo uliweka kando ukiirejesha mambo yanajipa.

Kuna suala la kutokuwemo kwa wananchi kwenye orodha ya waliofanyiwa tathmini katika barabara ya Ole/Kengeja. Kazi ya tathmini bado inaendelea na hawa wanaohisi hawamo tutaendelea kuwafanyia tathmini.

Kuhusu barabara ya Kiuyu/Minungwini Mkadini. Agizo hili limefanyiwa kazi na kwa kushirikiana na mradi wa *MIVARF* ulio chini ya Wizara ya Kilimo. Kuna barabara fulani zinajengwa chini ya Wizara ya Kilimo katika kusaidia kama ni *feeder roads* zinazotoka kwenye mabonde ya mashamba zinatiwa kifusi cha daraja la kwanza ili ziweze kupita.

Kwa mujibu wa taratibu zetu za Wizara barabara hizi zote baadae, Idara yetu ya Ujenzi itazitia lami. Lakini kwa hatua ya kwanza zipo chini ya Wizara ya Kilimo zinashughulikiwa. Kwa hivyo mule ambamo zimejengwa musifikiri kwamba zimeachwa njiani zitashughulikiwa. (*Makofi*).

Kuhusu ujenzi wa barabara ya Ole/Kengeja. Barabara hii itajengwa kwa kufuata viwango vinavyotumika katika ujenzi wa barabara kuu na inategemea kujengwa kwa lami ya kupika, yaani *asphalt concrete* na siyo lami baridi.

Mhe. Mohammed hapa alisema kuna barabara zimekwenda kutiwa rojo, na kama tumefanya majaribio. Hatukufanya majaribio Mheshimiwa, tumejenga ilivyostahiki na barabara zile baadae zitatiwa lami kama vile zinavyotiwa barabara nyengine.

Kuvunjika nyumba tatu zilizoangukiwa na muembe. Tathmini ya nyumba hizo kutokana na madhara yaliyojitokeza imefanyika na jumla ya milioni kumi na nane zinahitajika kulipia fidia ya nyumba hizo. Wizara inaendelea na taratibu za upatikanaji wa malipo ya fidia za nyumba hizo.

Suala la magari ya dala dala kutofika mwisho wa njia. Idara itaendelea kuzichukulia hatua kali gari zote zinazokatisha njia ili kudhibiti uvunjaji huo wa sheria.

Mheshimiwa hili ni lile lile la Mtambuka ni kwamba tutakapoanza kufanya marekebisho yasiwe povu la soda, tukafanya tukaacha, inatakiwa sote Idara zinazohusika tushirikiane liwe ni suala la kudumu.

Ujenzi wa barabara ya Mkanyageni/Kangani na Kiuyu. Ujenzi wa barabara hii kwa hatua za kifusi itafanyika kwa kupitia mradi wa *MIVARF*. Wizara kupitia Mfuko wa Barabara inajenga daraja la Tasini na baada ya uwekaji wa kifusi, Wizara kupitia Mfuko wa Barabara itaiwekea lami barabara hiyo. Kwa hivyo Mhe. Hija Hassan Hija na wale watu wa Mkoa wa Kusini na akina Bi. Mwanajuma mambo yatajipa tu!

Ujenzi wa barabara Mgagadu/Kiwani. Wizara kwa kupitia Mfuko wa Barabara imeiingiza barabara hii katika bajeti ya 2015/2016.

Uelewa mdogo wa madereva juu ya matumizi ya taa za barabarani. Idara hii itaendelea kutoa elimu kwa madereva husika na matumizi ya taa za barabarani. Taa hizi zimesemwa hapa kwamba vile vile ikitokea mawingu zinazima, ninadhani ni Mhe. Jaku Hashim Ayoub yule.

Utaratibu tumeshafanya tunaita *backup*, kutakuwa na betri nyuma ambayo inaungwa na umeme, utakapopungua ule mwanga wa kutumia mionzi ya jua ile betri ina-*backup* na taa zitakuwa zinaendelea kufanyika. Betri hizo tayari zipo na wale wanaohusika na mradi wameanza kushughulika kuziweka.

Mhe. Spika, kuna matumizi ya leseni ya daraja dogo (B1) kuendesha magari makubwa. Hili nimelisema kule nyuma kwenye matatizo ya daladala, lakini leseni ya daraja ya B1 ni kwa ajili ya magari binafsi yanayopakia abiria wasiozidi saba. Matumizi ya leseni hiyo kwa kuendesha magari makubwa ni kinyume na utaratibu na muhusika anapaswa kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mhe. Spika, suala jengine lililoelezwa kwa urefu hapa ni madaraja ya barabara ya Kaskazini na Kituo cha Daladala cha Kwa Nyanya.

Madaraja haya yanajengwa kupitia mradi wa ujenzi wa barabara ya Bububu, Mahonda, Kinyasini na Mkokotoni. Kwenye hotuba yangu nililisema hili kwamba makubaliano na *AfDB* karibu yanakamilika na kuna pesa zilizobaki tulikuwa tunaomba kama tunaweza kuanza kufanya matayarisho ya awali juu ya ujenzi wa barabara hiyo. Inaonekana inasuburiwa *approval* ya Bodi tu ya *AfDB* ili mradi huu uweze kuanza.

Kwa hivyo utaanza Bububu utapita hapo Kwa Nyanya, tunaendelea daraja zote zile zinazohusika ambazo amezitaja Mhe. Panya Ali Abdalla na mimi ninaziona, maana yake kila mara ninakwenda huko kwetu na hatari iliopo zitashughulikiwa kwa pamoja.

Ujenzi wa daraja hauwezi kujengwa kwa kufanya *repair* ndogo ndogo, unahitaji na una gharama kubwa sana. Sasa tunapojenga tunahitaji tuijenge kwa kufanya ujenzi unaostahiki na bahati nzuri *AfDB* imekubali kufanya shughuli hiyo.

Mhe. Spika, jengine ni gharama za ujenzi wa maegesho na njia za kupitia ndege. Hili alilisema Mhe. Salim kwamba angejua gharama za mradi ule wa *APRON* na *taxiway* umejengwa kwa gharama gani. Gharama za mradi huu zilikuwa ni bilioni 81.512 ambapo hadi kufikia Machi, 2015 bilioni 79.4 zimelipwa kwa Kampuni ya Sogea Satom. Gharama za usimamizi wa mradi wenyewe zilikuwa ni bilioni 4.13 ambapo hadi kufikia mwezi wa Machi wa Kampuni ya Gulf imelipwa bilioni 3.845. Fedha zilizobakia zitalipwa baada ya kumalizika muda wa uangalifu wa

mradi. Fedha zote hizo zinalipwa kupitia mkopo kutoka Benki ya Dunia jumla ya TZ.Shs.1.3 bilioni zimelipwa na Serikali kwa ajili ya fidia ya mali za wananchi.

Kuna kitu kinaitwa *retention fund*, hata ukimaliza mradi kuna bakaa kama *five percent* (5%) ya thamani ya mradi inabakia kwa matengenezo madogo madogo. Kwa mfano, karibuni ilinyesha mvua ikaonekana Uwanja wa Ndege kule kwenye *runway* hasa kumebaki maji. Sasa sisi tunamwita mjenzi tunamwambia mheshimiwa vipi mambo hapa mbona hivi, anaeleza hii ni kwa sababu gani na kwa nini iwe hivyo. Kumbe tukagundua katika ule utaalamu wa kujenga ile barabara, kile kipima maji kile kinakuwa kidogo ule uwanja usikae hivi. Kwa hivyo ikipita mvua tu dakika tano, kumi, maji yamekwisha. Tukapata maelezo yakatosheleza na mambo yanaendelea mpaka utakapomalizika muda wa *retention fund* atapewa pesa zake. Kwa hivyo hizo ndizo gharama zenyewe.

Mhe. Spika, gharama ya mabadiliko ya ujenzi wa jengo jipya la abiria na tofauti kati ya fedha zilizotengwa na zilizotumika katika mradi huu.

Suala la mradi huu wa *Terminal II* limekuwa ni mjadala wa muda mrefu katika Baraza hili. Mradi ule ulianza kwa milioni 58.4 kuufanya mradi mzima kugharamia na umebadilika mpaka dola milioni 128.8 kutoka USD milioni 70.4. Tofauti hiyo ya milioni 84.7 iliyoelezwa ilitokana kutoka 1.95*billions* mpaka 2.79 imehusishwa kutoka vifungu vyengine vya fedha ili kukidhi mahitaji ya mradi.

Ninakumbuka aliuliza Mhe. Hija Hassan Hija huwaje pesa hizi zikatolewa huku zikaletwa huku. Inategemea haja ya mradi wenyewe na miradi mengine; miradi mengine kama tulivyosema, mara nyengine unaziona bilioni 500 zipo lakini hazijatiwa kitu kwa sababu ile *activity* ya ule mradi haukuanza. Kwa hivyo katika haja ya kumaliza ule unaoendelea Waziri ana madaraka ya kumshauri Waziri wa Fedha, fedha zile zihaulishwe ili kuukamilisha tatizo lililopo mbele yetu. Huo ndio utaratibu unaotokea katika kufanya shughuli hiyo.

Mhe. Spika, kulikuwa na suala la maendeleo na hatma ya ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Sisi kama wataalamu wa sekta, kazi yetu ni kutayarisha masuala ya kitaalamu. Kazi hizo taratibu zote za kiufundi ikiwemo upembuzi yakinifu na utafiti wa athari za kimazingira zimeshafanyika na mkataba wa ujenzi tayari umeshatiwa saini.

Taratibu za upatikanaji wa fedha za ujenzi wa barabara hiyo kutoka Benki ya *Exim* zinaendelea. Benki hiyo inaendelea na tathmini ya maombi yetu kupitia nyaraka zilizowasilishwa na Serikali. Sisi wajibu wetu ni kukamilisha haya, kazi iliyobaki ni ya wenzetu Wizara ya Fedha kulishughulikia kuupatia fedha mradi. Kwa hivyo

mradi upo na unaendelea kushughulikiwa. Nyaraka zote zimeshafika kwa *Exim Bank* na wao wanafanya uchambuzi, wakitujibu mkataba wa fedha utatiwa saini.

Suala jengine lililoelezwa ni jinsi ya kuimarisha Uwanja wa Ndege wa Pemba. Benki ya Maendeleo ya Afrika imekubali kuufadhili upembuzi yakinifu wa uwanja huo. Matarajio ya kazi hiyo kuanza mwaka ujao wa fedha. *Study* hiyo ndiyo itakayotupa jinsi ya kuelekea huko, lakini hata hivyo tumetakiwa tuwe na kitu kinaitwa *concept*, yaani tunataka ule uwanja uweje. Hilo tunaiandikia Serikali kueleza kwamba sasa hivi Uwanja wa Pemba unahitaji ukijengwa angalau uongezwe na urefu na zile njia zake zinapita *taxiway* ziwe kubwa zaidi na kwamba mahitaji baada ya kuwa zinatua hivi vi-*charter* iweze kutua angalau *Boeing 767* na kwamba viongozi mara nyengine wanaweza wakawa na shughuli za Kiserikali waweze kuondoka usiku au kutua usiku kwa kufanya shughuli hizo.

Suala tunalifikisha Serikalini kwa kupata uamuzi kabla ya ile *study* haijaanza, ikija *study* tuweze kumwambia yule anayefanya *study* dhamira yetu ni hii. Mhe. Spika, hilo nimepewa dhamana kama Waziri nilifikishe Serikalini kupata maamuzi.

Mhe. Spika, baada ya kutoka sekta ya barabara kulikuwa na masuala machache nimalizie yanayohusu mambo ya mawasiliano (*TEHAMA*). Kuliulizwa suala kuwa makampuni ya simu kama vile *VODACOM, TIGO, AIRTEL*, kwa nini hawalipi kodi Zanzibar.

Mhe. Spika, sisi Idara ya Mawasiliano na *TEHAMA* ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kazi yetu ni ufundi. Kwa kweli mara nyengine si rahisi kufahamu kazi yetu ufundi wa namna gani. Labda nikichukua kama *analogue* ni sawa sawa na kwamba kuna bomba la maji kubwa linapita ukasema ninataka nivute maji kwenye nyumba yangu. Ukifika hapo basi sisi tutakutilia mfereji maji uyapate. Sasa kwenye utaalamu huu wa *TEHAMA*, kazi yetu sisi ni kuvuta waya tukakutilia Wizara yako ukaweza kutumia mkonga, hiyo ndiyo dhamana yetu sisi, lakini masuala ya kodi na utaratibu wote unaohusu mikataba ya fedha ni suala la Wizara ya Fedha. Kwa hivyo, hatuna majibu sahihi juu ya kodi hizi na Mhe. Waziri wa Fedha anaweza akalieleza vizuri zaidi.

Kwa nini vocha za *ZANTEL* zinatumika haraka sana bila ya utaratibu unaoeleweka, hili Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi alisema hivyo. Jamani tumekuwa siku hizi kila mmoja ana *smartphone*, bila ya *smartphone* unaona hujaendelea, kumbe dudu lenyewe linakula kweli kweli.

Sisi tunawaza tu unapeleka *WhatsApp*, unapeleka sijui nini, unatizama *facebook* vitu vinakwenda, unashughulikia vipesa havimo hasa unapokata na hivi vifurushi. Kwa hivyo ni kweli malalamiko hayo yamefika *ZANTEL*. *ZANTEL* imelifanyia

utafiti na kugundua kuwa waathirika wengi wale wanaotumia simu za *smartphone* ambazo zinatumia kwa mfumo wa *3G* unaotumia huduma ya *internet*, na pale inapokuwa mtumiaji wa huduma za *package* hupelekea matumizi kuwa makubwa ambayo yanatumika katika ku-*download*, yaani kuteremsha ma-*files* ya vitu vyengine na ikimaliza ile simu yenyewe inasema hebu jamani jiweke pazuri, yaani uki-*update* na vipesa navyo vinaendelea kuliwa.

Baada ya *complain* hiyo *ZANTEL* inaandaa elimu kwa watumiaji wa *smartphone* ili waweze kuepukana na kadhia hiyo. Hivyo ZANTEL inaandaa elimu kwa watumiaji wa smartphone ikiwezekana kuepuka usumbufu huo.

Mhe. Spika, mwisho kuna suala la Mhe. Viwe Khamis Abdalla kuhusu usumbufu na upatikanaji mbaya wa mtandao wa *ZANTEL* Pemba.

ZANTEL kwa upande wa Pemba hakuna matatizo isipokuwa kuna baadhi ya sehemu hakuna mfumo wa *3G*, hivyo husababisha ukosefu wa mtandao wa *internet*, na hivyo kwa wale ambao wanatumia *smartphone* hupata usumbufu kidogo, lakini siyo sababu nyengine yoyote.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Mhe. Waziri ninakushukuru sana. Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa mwaka 2015/2016 wanyanyue mikono, wanaokataa.

Wote waliomo humu ndani wamekubali. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvivu: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, sasa naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya Wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU P01 - WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Kifungu 06 Idara ya Usafiri na Leseni	Shs.1,169,873,000/=
Jumla Kuu	**Shs.1,169,873,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU P01 - WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza kabisa Mhe. Waziri na Naibu Waziri kwa kuchambua hoja moja baada ya moja, nashukuru sana kwa hilo. Lakini nimechelewa nikiri kidogo nilikwenda kuhakikisha baadhi ya mambo kule kwenye Jimbo la Muyuni, hasa barabara ya Pete inayofanya shimo kubwa pale *crossing*, lakini naishukuru Wizara kupitia *UUB* kwa kuziba shimo lile.

Baada ya hayo, Mhe. Waziri alijibu sana kuhusu suala la Mnazi Mmoja barabara za ndani, na yeye alikuwa ni Waziri wa Afya kwa kipindi kile na Mwenyezi Mungu kamleta huku sasa hivi tuone neema yake, neema ya Mwenyezi Mungu ilivyokuwa kubwa.

Hetu twambie Mhe. Waziri kama wewe ulikuwa Waziri wa Afya na yale mashimo yakakukera. Kipindi kilichopita cha bajeti ile ulimuomba Mhe. Gavu ili akusaidie barabara zile. Leo kama waziri unatoa kauli gani kwenda kunusuru hali ile. Mwenyezi Mungu mkubwa Mhe. Mwenyekiti! *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Jaku Hashim Ayoub amekubali kwamba tulipokuwa tukieleza alikuwa hajafika, na nakumbuka nilipokuwa najitambulisha nilikwambia wengine watakuja baadaye halafu watauliza maswali, lakini ni wajibu wake.

Mhe. Mwenyekiti, tulieleza hapa kwamba tutashirikiana na wenzetu wa Wizara ya Afya na hasa mimi kwa sababu nilikuwa naijua hii wizara na hayo mashimo yatafukiwa hakuna tatizo. Kama vile tunavyofukia mengine, sio suala gumu. Tutashirikiana na wenzetu Mkurugenzi wa Mnazi Mmoja tulifanye suala hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri, kushirikiana wanaweza kushirikiana leo, kesho, kesho kutwa, mwezi au baada ya

mwaka. Atoe kauli wagonjwa wanazidi kuteseka na vile vibaiskeli na anajua kuwa havipo vibaiskeli ni ringi tupu zinazotembea pale hata mipira hazina, wagonjwa wanazidi kuumia.

Kwa hivyo, atoe kauli kama ni kesho au kesho kutwa, na kwa vile waziri ninavyomfahamu kwa umakini wake na hii wizara na uchungu wa wizara hii nafikiri hatofika siku tatu. Mhe. Waziri nataka jawabu kutoka kwako.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nacheka kwamba si angalau basi tumalize hii bajeti. Maana huko mashimo yanaendelea kuzibwa, basi angalau tumalize hii bajeti. Ikimaliza hii bajeti mashimo yatafukiwa siwezi kumwambia kesho, maana itakuwa hata pesa sijapata hata hapa. *(Makofi)*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sawa Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

FUNGU P01 - WIZARA YA MIUNDOMBINU NA MAWASILIANO

KIFUNGU P01 - PROGRAMU YA MIUNDOMBINU NA HUDUMA ZA USAFIRI WA BARABARA

Programu Ndogo S01 Ujenzi na Matengenezo ya Barabara Shs. 33,042,936,000
Programu Ndogo S02

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru tena Mhe. Waziri hapo kajibu hoja. Nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa Mhe. Haji Omar Kheri, katika mtu anayepiga kelele sana kuhusu kituo cha Daladala basi mmoja ni mimi na siku zote napiga kelele Mhe. Haji ananijibu yeye.

Baada ya kutoa ufafanuzi kuwa hivi sasa vituo vyote kwa mujibu wa Katiba na Sheria viko Miundombinu. Sote humu, labda kama Wajumbe watatu ndio wanavaa miwani kama Mhe. Thuwaybah Edington na Mhe. Balozi; watu wawili ndio wanavaa miwani.

Leo kituo cha daladala pale pana gari zinakaa. aah! na Mhe. Abuu. Kuna gari zinakaa kwenye kituo cha daladala kile, tunawadanganya vipi wananchi na gari pale zinakaa lakini daladala zisiende. Je, ni sababu gani ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim ulichelewa kidogo. Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, anamaanisha wapi hapo Kisiwandui au ?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kituo tokea Ukoloni kama wewe Mhe. Waziri hujazaliwa wala mimi, kinatumika Darajani Marikiti. Mtu anatoka Pemba anajua kituo pale ndio kituo chake kikubwa, akifika pale ana watoto sita au saba. Leo cha kushangaza na cha kutia huzuni na unyonge mkubwa kuna gari zaidi ya 100 zinakaa pale, sababu gani gari zikae lakini daladala zisiende pale, kama anafunga afunge pote.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Sasa hoja ni nini mbona sijafahamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hoja utoe ruhusa gari zitumike zote, haki ya binadamu kwa wote. Kama itumike ile na ile itumike.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mjumbe anazungumzia kuondoshwa kwa kituo cha daladala Darajani. Kama maelezo ya Mhe. Waziri alivyoyatoa, kwamba maamuzi ya serikali ni kukiondosha kituo. Kituo kitawekwa wapi ndio hoja ambayo alikuwa akizungumza Mhe. Waziri, kwamba serikali imefanya jitihada za kufanya mikutano na wadau mbali mbali, maamuzi ya serikali wapi kitawekwa kituo bado serikali haijafikia muafaka.

Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Mjumbe, kwamba suala la kurejesha kituo Darajani, serikalini halipo. Madhumuni ya serikali ni kutafuta eneo jengine ambalo litakuwa mbadala, muafaka na litaondosha huo usumbufu ambao serikali imeuona hivi sasa upo katika eneo la Darajani.

Mhe. Mwenyekiti, mategemeo yetu ni kwamba tutafute eneo la maegesho litakalokidhi huduma za wenye daladala, wasafiri wengine na changamoto hizo ambazo tunaziona sasa hivi, ni lazima tujipe upeo wa kufikiria na kesho yake.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Mjumbe kwamba serikali maamuzi ya kuyahamisha maegesho Darajani imeshafikiwa. Kilichopo hivi sasa ni kujadiliana na wadau ama washirika, kutafuta maeneo mengine ama eneo jengine mbadala kwa ajili ya kuweka maegesho kwa huduma za daladala na magari mengine. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimshukuru kijana mwenzangu Naibu Waziri na mimi ni mkubwa wake kidogo kiumri. Lakini kabla ya kujenga hoja niliangalia watu wenye miwani ni wangapi.

Ukweli Mhe. Naibu Waziri tuseme ukweli tupo hapa kwa niaba ya wananchi, haiwezekani Katiba hii inaongoza Wazanzibari. Ngoja nikusomee kidogo ninukuu:-

"Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote kulinda na kupata haki sawa mbele ya sheria".

Kwa nini gari zile mkaziweka pale, kuna magari huwa yanakaa, leo daladala zisiende pale. Watu wanatoka Pemba wanakuja pale wana watoto sita au saba waende wapi na kituo kile kipo kabla ya ukoloni.

Halafu cha kusikitisha zaidi mnakwenda kukifunga bila ya taarifa yoyote, kama ni amri ya serikali, serikali ndio wananchi, wananchi ndio serikali. Serikali itakuwa bila ya kuwa na wananchi. Mkajenge hoja Mawaziri na Manaibu Waziri tuwe makini, jibu hoja ili wananchi wapate kufahamu, tupo kwa niaba ya wananchi!

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba Mhe. Mjumbe, kama yalivyo maelezo yake kwamba anataka tujibu hoja, mimi namuomba tu ajenge hoja.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo na utaratibu wa serikali kituo kimehamishwa. Ni kweli kituo kilikuwepo toka enzi za Ukoloni, toka tuna gari nne, zimekuja gari sita, zimekuja gari nane mpaka hivi sasa kituo kile kimezidiwa. Ndio maana serikali imeamua kwa kuona kwamba eneo hili matumizi yake na magari yanapelekea *congestion*.

Mhe. Waziri ameeleza vizuri sana hapa tena akatoa mfano wa lugha ambayo wewe utaifahamu vizuri. Akasema kuwa mji umecheuka, kwa kumaanisha kwamba maegesho yale hivi sasa yamezidiwa. Serikali imefanya maamuzi kwamba tutafute eneo mbadala kuwa maegesho. Sasa serikali ili tuweze kwenda vizuri, tumekusanya maoni ya wadau na washirika mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi ni sehemu ya watu ambao wanatakiwa kutoa mawazo yao, tumefanya semina. Kwa bahati mbaya kwamba mjenga hoja huyu yeye mtoro, siku zote katika kutoa mawazo yake haji, yeye anajenga utamaduni wa kulalamika tu. Kwa hivyo, mimi nimuombe Mhe. Mjumbe, kama tunataka tujenge hoja na tujibu hoja, na mwenzetu yeye ni lazima atusikilize. Akija hapa na maamuzi yake mfukoni, tutakuwa hatujengi utamaduni mzuri. Ni lazima akija hapa ajenge hoja ya kusema la kwake, na asikie ya upande wa pili.

Sisi tumekiri kwamba kituo hiki kipo cha asili, lakini hivi sasa kimezidiwa na sote tunakiri hapa, hakuna hata mmoja ambaye hajui kama Darajani pamezidiwa na magari. Kama serikali ni lazima tufikirie jambo jengine la ziada, hatuwezi kuwa viongozi tukaja kuongozwa na jambo la karne tukashindwa kubuni jambo jipya.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, natambua kwamba kuna jambo kubwa sana mnalofanya, na siwezi nikasema msiende, lakini hebu tuzingatie na hizi taratibu zinavyokwenda.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe kama ana hoja nyengine ya msingi aseme, kama hakuna hili atuachie tuendelee na utaratibu wetu wa kupitisha bajeti tukafanye kazi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi namuheshimu sana Mhe. Naibu Waziri, pamoja na umri wake mbele yangu. Lakini katiba ndio hii, sikuitunga mimi nimeikuta na inasema watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wana haki bila ya ubaguzi wowote.

Kuna gari pale zinakaa kwa msingi gani au zinasaidia nini serikalini. Ninachozungumza Mhe. Mwenyekiti, ni Kiswahili wala sio Kihindi. Kuna gari zinakaa pale zinakaa kwa msingi gani. Asifanye kukurupuka tu akataka kunionea. Katiba hii ndio inayoniongoza, hoja yangu ni katiba, pale gari zipo kama anabisha twende.

Mimi niko tayari kujiuzulu Uwakilishi kuachia ngazi, kama hapana gari zinazokaa pale. Je, yeye yuko tayari kujiuzulu Uwakilishi au Unaibu Waziri. Tujenge hoja moja baada ya moja, sio aje akurupuke tu hapa. Mimi niko tayari kuacha uwakilishi kama nilichozungumza si cha kweli, ajenge hoja! *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim nafikiri haina haja ya kujiuzulu, muda wenyewe haukubakia mkubwa, nadhani tuendelee kushirikiana ili tumalize Baraza hili la Nane vizuri.

Wanachosema Waheshimiwa pale Waziri na Naibu wake, ni kwamba suala la Darajani linaeleweka, na ni kweli na ni suala ambalo kama linavyokuuma wewe, linatuuma na sisi wengine sote, ila ni jambo ambalo tunataka tuwe na ufumbuzi wa kudumu na ndio maana akachukua hatua alizochukua wakikutana pale juu, ili kuzingatia pamoja na mambo mengine suala hili na sote tulikuwepo nafikiri hata wewe pia ulikuwepo.

Kwa hivyo, maoni yaliyotolewa inabidi yafanyiwe kazi na hatimaye serikali ijue inafanya nini baada yake. Kwa hivyo, sio kwamba hakuna hatua zinazochukuliwa, hapana. Hatua zinachukuliwa, lakini hatuwezi tukakurupuka haraka haraka na kusema kwamba *okay*, basi tunaondoa hapa tunapeleka pahala pengine. Ni jambo linalohitaji kutumika muda, kuzingatia ili tuwe na ufumbuzi wa kudumu juu ya jambo hili.

Nadhani itakuwa sio kufanya maamuzi ya moja kwa moja ndani ya chombo hiki, isipokuwa labda tutakachoweza kusema ni kuhimiza mambo haya yasimamiwe vizuri, ili tupate ufumbuzi wa kudumu hatimaye kupunguza hayo matatizo ambayo yamekuwepo.

Waheshimiwa Wajumbe, kucheuka kwa mji pale Darajani sote tunaelewa, na matatizo yake sote tunayaelewa.Wakati fulani mpaka vijana wanaosoma pale hawasomi vizuri sote tunaelewa. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali yupo anajua, aliyekuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali alikuwa anasema sana jambo hilo. Kwa hivyo, nadhani tuiachie serikali jambo hili ili iweze kulisimamia kwa utaratibu, ili hatimaye tupate ufumbuzi wa kudumu.

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani maelezo yaliyotolewa pale mimi nayaona ni ya msingi sana, na sio kwamba wanakataa kufuata hiyo Katiba uliyosoma, hapana. Tunataka tutekeleze jambo ambalo lina ufumbuzi wa kudumu. Nadhani tuendelee.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumza kuhusu barabara ya Mkanyageni/Kangani. Barabara hii kwa kweli imeshanichosha na inaniuma.

Mhe. Waziri aliniambia kwamba barabara hii tayari sasa hivi inataka kujengwa, lakini bado sijaamini, kwa sababu huu ni mwaka wa 10 hivi sasa kila siku kesho kesho na pesa zile zinawekwa za mfuko ule wa barabara ile ya Kangani/Kuukuu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anihakikishie ni lini barabara hiyo itajengwa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa naeleza nilisema pesa zimeshatengwa katika mfuko wa barabara na tunajenga mwakani. Sasa mfuko wa barabara ni tofauti na bajeti ya Mhe. Omar Yussuf Mzee. Pesa za Mfuko wa Barabara zinashughulikiwa na mfuko wa barabara na wanafanya bajeti na huwa inaamuliwa mapema barabara gani na barabara gani itajengwa. Kwa hivyo, ninachoomba kumthibitishia kwamba hiyo barabara imo mwakani.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Waziri, lakini kuna kitu kimoja tu nimuombe, kwa sababu kila siku kesho kesho imekuwa kama mtoto wa kuku anataka kunyonya kesho mpaka anafikia hatima anakua. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kama hakuna huo mfuko, basi nimuombe japo kifusi tu anitilie ile barabara kwa sababu watu wanahangaika sana, wanashindwa hata pa kupita, akitokea mgonjwa wanashindwa kumpeleka hospitali. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anifanyie japo hivyo, sio lazima kujengewa barabara na lami mimi, tunataka tupate pa kupita tu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri una maelezo zaidi. Kwa hatua za dharura anasema japo kifusi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, wala sio suala la japo kifusi, tunakusudia tumpambe hasa Bi Mwanajuma. Kwa hivyo, naomba aniamini na mwanzo tunaanza na tatizo la daraja, maana tatizo kubwa la daraja pale kabla hata hiyo barabara. Kwa hivyo, tutaanza na hilo daraja, halafu tutafanya na hayo mengine na kama kifusi tutatia, lakini imo mwakani.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante tuendelee namshukuru Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Viwe Khamis Abdallah: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, lakini bado sijaridhika na majibu aliyonijibu.

Mhe. Mwenyekiti, barabara aliyoieleza Mhe. Waziri ni barabara ambayo imefadhiliwa na Mradi wa *MIVARF* ulioko kwenye Wizara ya Kilimo na Maliasili. Wizara inaijua barabara hii kwa kina, kwa sababu Wizara ya Kilimo na Maliasili nimeshaifanyia kazi kwa miaka miwili. Hii ni ahadi ya Rais na ninayosema mimi ni barabara inayotoka Skuli ya Minungwini mpaka inayopita Kiuyu Fimbo, Mkadini. Leo Mhe. Waziri ananiambiaje kwamba barabara hii imefadhiliwa na Mradi wa *MIVARF* ndio barabara ambayo wananchi wangu waliomba na Mhe. Rais ndio keshaitekeleza. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anipe tena jibu.

Mhe. Mwenyekiti: Tumridhishe Mhe. Viwe Khamis, Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kama ni ahadi ya Rais hatuwezi kuivunja kuitekeleza, kama tumetaja sio sisi tuliona ni Minungwini Mkadini na Minungwini kaitaja kama inaendelea kwenda huko kwengine, basi tutaingiza katika Mfuko wa Barabara. Mimi kama waziri ninayo amri fulani katika pesa za Mfuko wa Barabara, kuwaambia jamani tuna ahadi ya bibi Viwe Khamis.

Mhe. Viwe Khamis Abdallah: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Waziri kwa maelezo mazuri aliyonipa sasa hivi, lakini namuomba Mhe. Waziri barabara hii isije ikamaliza mwezi huu kama sijaona dalili yoyote ile.

Tuendelee. *(Vicheko/Makofi)*

Programu Ndogo S02 Usimamizi wa Usafiri wa barabara	Shs.577,732,000
Jumla ya Kifungu P01	**Shs. 33,620,668,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu P02 Programu ya Miundombinu ya Bandari

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kuna msemo unaosema *huruma hailei mwana* na *mtoto umleyavyo ndivyo akuavyo.* Miundombinu ya Uwanja wa Ndege katika nilipochangia asubuhi nilisema kuna gari za Serikali SMZ zinaingia bila ya kubughudhiwa, ikiwa gari ya Mheshimiwa Hija naye ni Mwakilishi anaambiwa alipe shilingi elfu mbili, ni sababu gani imesababisha vile ikiwa Uwanja wa Ndege wa ndugu zetu wa Dar es Salaam wa *VIP* una heshima ya hali ya juu kwa kiongozi, hata ukipita na vespa au pikipiki Mheshimiwa unapita bure.

Ni sababu gani ya msingi Mhe. Naibu Waziri na Waziri mtayotoa hata tuweze kukubali humu ndani? Narudia tena hili suala Dar es Salaam lipo, na kama atakuwa hana nauli mtu twende tukathibitishe ukiingia *VIP* huulizwi chochote na gari, lakini ukipita hapa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar utakiona cha mtema kuni, sasa huo uheshimiwa au uongozi una faida gani ikiwa gari ya SMZ itaruhusiwa, Mheshimiwa haheshimiwi, lete maneno. *(Kicheko)*

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namuomba sana Mhe. Jaku aweze kutengeneza ufafanuzi mzuri sana anapolinganisha kiwanja cha ndege cha Dar es Salaam na kiwanja cha ndege cha Zanzibar.

Sote tunajua na tunaona mabadiliko makubwa sana ya uimarishaji wa miundombinu katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, wenzetu hawa wa Mamlaka wameweza kutafuta kampuni tanzu ya Chui kwa ajili ya kuingia nao ubia, ili tu kuweza kuimarisha mfumo mzima wa *Gate toll* ili kuweza kuona magari yanayoingia yanayoweza kutozwa tozo kwa madhumuni ya kuongeza kipato ili tuweze kuimarisha huduma katika uwanja wa Ndege. Ni kweli unapokwenda Dar es Salaam viongozi wanadili na *passenger* kwa maana ya kwamba yule mtu binafsi unavyotambulikana tu kwamba wewe kiongozi hutozwi tozo yoyote.

Utaratibu wa Mamlaka Zanzibar uko kinyume, utaratibu wetu tulioupanga katika mamlaka ya viwanja vya ndege Zanzibar unapokwenda na gari la Serikali hutotozwa tozo yoyote, unahamisha lile gari lenyewe, tutakuruhusu wewe uingie bure, lakini kiongozi yeyote atakapokwenda na gari binafsi atatozwa tozo. Mimi mwenyewe binafsi nyakati nyingi ninapoendesha gari yangu binafsi

ninavyokwenda Uwanja wa Ndege natozwa tozo na nalipa, sijawahi kulalamika, na ninapokwenda na gari ya Serikali napita bure kwa sababu najua utaratibu ambao tumekubaliana, gari la Serikali litaruhusiwa kuingia bure na kutoka bure, lakini kiongozi binafsi kwa maana ya kwamba atakapobadilisha gari la Serikali atatozwa tozo.

Nina hakika Mawaziri wote mashahidi hapa hakuna aliyekwenda na gari lake binafsi akawa hajatozwa tozo, kwa hivyo nimuombe Mhe. Jaku kulikuwa kuna utaratibu ni kuchagua ama uchague mtu akija gari ya ng'ombe au la punda apite bure, ama mchague kuweka nidhamu kwamba atakapokuja na gari maalum aweze kupata tozo. Au tutengeneze utaratibu wa kutaka kwamba mtu atakapokuja na chombo hiki atapita, atakapokuja na chombo chengine zaidi ya hiki hatoruhusiwa kupita bodi, kwa hivyo maamuzi ya *ZAA* na sisi kama Wizara tunayabariki, kwamba mtu atakapokuja na gari ya Serikali aweze kuruhusiwa bure, lakini yeyote atakayekwenda na gari binafsi atozwe tozo kama ilivyo hivi sasa, kwa madhumuni tu ya kujenga ile nidhamu na kuimarisha huduma katika uwanja wetu wa ndege. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja zangu zitakuwa tatu linolipishwa ni gari au mtu, na kwa maana hiyo utaratibu uliopo *VIP* itakuwa ni ya viongozi wa Serikali tu Mhe. Hija atakuwa si *VIP*. Utaratibu uliopo na hayo makubaliano Mhe. Naibu Waziri mumekubaliana na nani? Yamepitishwa hapa hayo makubaliano ya kuwa gari iingie pale ya Serikali? Makubaliano hayo yamepitishwa wapi pahali gani, hicho kikao kimekaa wapi cha makubaliano?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba tu nimkumbushe Mhe. Mjumbe kwamba tulifanya mabadiliko ya msingi hapa tukapitisha Sheria Na. 8 ambayo imeweka mamlaka ya kuanzishwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar. Katika mamlaka yale Mamlaka ile inafanya kazi pamoja na wizara, kwa hivyo ninapozungumza makubaliano kwa msingi huo, kwamba chombo ambacho kimepewa nguvu na Sheria na sisi Wizara kama wasimamizi kwetu sisi tayari tumetoa baraka, lakini haya tunayoyafanya sisi kama Wizara wenzetu wa Mamlaka wana chombo chao ambacho ni bodi, wanakaa wanachoamua kama kuna kubwa wanatuletea sisi kama wasimamizi wao, na tunakubaliana nalo, pa kuongoza tunawaongoza pa kurekebisha wanarekebisha.

Hoja yake Mjumbe ameuliza kama kinacholipishwa ni nini? Tumesema wazi hapa kinacholipishwa ni gari, kwa maana ya kwamba ukienda na gari ya SMZ hutolipishwa, ukienda na gari ya binafsi utalipishwa. Sasa haimaanishi kwamba wewe unakwenda *VIP* au unakwenda katika kuondoka eneo la kawaida ukiingia tu katika eneo la Uwanja wa Ndege unatozwa tozo, ukienda *VIP* utatozwa tozo, ukienda kwa kawaida utatozwa tozo ya kuingia katika eneo la *Airport* bila ya kujali

kwamba wewe Mwakilishi, Mbunge au Waziri. Ukienda na gari ya Serikali hutotozwa ada ya kuingilia utatozwa ada ya *VIP* ambayo ni elfu ishirini. Ukija kwa kawaida huku na gari yako ya binafsi utatozwa tozo ile ya kuingilia katika eneo la *Airport*, vyenginevyo Mamlaka yetu isitegemee kupata mafanikio, kama tunataka tukate hiyo mianya inayoongezea mapato.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naamini Mhe. Mjumbe kwamba yale uliyokuwa umeulizia yamepata majibu ya kipi ambacho kinatozwa tozo na utaratibu wetu ni huu, sisi hatuangalii mtu kwamba binafsi; huyu Mkurugenzi, Waziri, hapana, tunaangalia ukija na gari ya Serikali hata kama si mtumishi wa Serikali ndio maana gari itaingia bure, lakini wewe ukija na gari ya binafsi hata kama kiongozi lazima utozwe hiyo tozo ndio utaratibu ambao tumekubaliana nao watu wa *ZAA*.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri maelezo yanatosheleza tuendelee.

Kifungu P02 Programu ya Miundombinu ya Bandari na Viwanja vya Ndege

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mimi namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akitoa ufafanuzi kuhusu hoja yangu kuhusu ile meli ya *Sepideh* ambayo inaendelea kuathirika na kuoza pale baharini baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa.

Sasa nilimuomba Mhe. Waziri wakutane Mawaziri watatu; Mhe, Waziri wa Miundombinu, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na Mhe. Waziri wa Biashara. Halafu na mimi niliyejenga hoja si vibaya nikashirikishwa katika hiyo na kwa nini nikamtaja Waziri wa Katiba na Sheria, kwa sababu kuna jambo.

Sasa Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu alisema tu naweza huyu mwekezaji akakaa na Wizara, tumeshaona hawa hawatofikia muafaka na kama hawatofikia muafaka ndio maana tukaunganisha vichwa hivi vitatu pamoja na mimi hata nikifuatana na Mwanasheria wangu Mhe. Makame Mshimba, tukalikalia hili tunaamini tutakuja na *solution* ambayo huyu mwekezaji aliyezuiliwa meli yake akafarijika, na Serikali kupitia Shirika la Bandari wakapata hiyo haki yao, lakini kwa kusema mwekezaji na hawa wenyewe walioizuia ile hawafikii muafaka, ndio maana sasa hivi zaidi ya mwaka mmoja meli ile baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa imekaa pale.

Sasa nilikuwa naomba tu Mhe. Waziri aniridhie katika hili ombi, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Hebu tuchukue na hoja ya Mhe. Mshimba moja kwa moja aliyouliza kwa pamoja

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri, ni mmoja katika mtu mzuri anayejibu maneno kiufasaha na akakuelewa.

Katika hoja yangu mimi ya hapa sehemu ya *ZMA* alinijibu kuhusu habari ya wale wataalamu na alisema wataalamu hawa wanakuwa wanapata muda wa kuweza kukikagua chombo ili wakaweza kufikiri. Lakini Mheshimiwa sijui sheria ikoje, na kama sheria ina mapungufu basi ningeomba Mzee mzima hapa kamanda mwenyewe Hamza tutakaa tuweze kusaidiana kuweka sawa sheria hizo.

Mhe. Mwenyekiti, tunavyoelewa duniani kwanza nimsifu sana Mkurugenzi, Mkurugenzi unapompelekea barua ya chombo kutaka kukaguliwa yeye anakuwa *faster*, na kwa sababu gani anakuwa *faster* kuweza kuitoa kuishusha chini kwa sababu anajua yule ni mteja wake hawezi akamuweka, sasa hawa wataalamu wanapokuwa wanapelekewa barua hakuwa na sababu pale, hakuna kufikiri, ni kwenda kukiangalia chombo na baadae wakaweza kutoa ripoti. Hebu tuangalie je, na hao wengine wakubwa wanafanyiwa hivyo hivyo au wanyonge tu. Sasa mimi ningeomba hapa aniweke sawa katika hili kwa mujibu wa sheria.

Je, wakati wewe unavyokwenda kukagua unatakiwa kufikiri au unaporudi kukagua ndio unapotakiwa kufikiri?

Mhe. Mwenyekiti: Tupate maelezo Mhe. Waziri kwa hoja hizo mbili.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze na hoja ya kwanza ya Mwalimu wangu kamanda wangu Mhe. Hamza Hassan Juma aliyeulizia suala zima la *MEGA SEPIDEH.*

Kwanza naomba nikiri kwamba meli hii imekaa mwaka mmoja, na sababu ya msingi ya kukaa mwaka mmoja kwamba kulikuwa kuna kesi ya msingi ambayo imefunguliwa mwaka 2013 na kesi hii imeisha juzi 2015. Tabaan kwa utaratibu wa taasisi yetu inayoheshimu sheria huwezi ukafanya tukio lolote kama chombo au kitu husika kimezuiwa kwa amri ya Mahakama.

Hivi sasa tayari Mahakama imeshatoa maamuzi, ninachomthibitishia Mhe. Hamza mgogoro mkubwa ulikuwa ni mmiliki kukiri kwamba yeye anadaiwa na hili ndio lililopelekea kwenda Mahakamani kwa muda wote alikuwa hajakiri. Lakini kama atakiri kwamba kweli anadaiwa milioni 71 kesho akiandika barua keshokutwa Jumamosi watakutana Shirika la Bandari na watakubaliana. Kwa nini nasema watakubaliana, mmiliki huyu tayari ana vyombo vyengine ambavyo anafanya kazi kwa pamoja wana madeni, wanashauriana, wanasikilizana na anafanya kazi kwa kuelewana, kwa hivyo mgogoro ulikuwa kulikubali au kutolikubali, na alikacha

kulikubali deni hili kwa kusema tu kwamba deni hili lilipoanza yeye alikuwa sio mmiliki wa meli na huo utaratibu ndio mwanzo nikasema utaratibu unapo -*transfer* una *transfer rights* na *liabilities* zake, na msingi wa Shirika la Bandari wamechukua mfano mzuri wa meli ya *Global* ilipogonga hapa Zanzibar iliuzwa Urusi ikatoka Urusi ikauzwa nchi nyengine lakini waliposhtaki ikakamatwa Panama, yule mtu wa tatu kuimiliki ndiye aliyekuja kuadhibiwa kwa sababu ya kugonga na yeye akalipa.

Kwa hivyo msingi ule ule Shirika la Bandari wamejenga *precedent* kwamba kwa msingi huu huyu mmiliki wa *SEPIDEH* wa mwisho ndiye ambaye anapaswa kutulipa deni letu la milioni 71.

Kwa hivyo nikuthibitishie tu Mhe. Hamza kwamba sisi Shirika la Bandari wako tayari kesho kama ataandika barua ya kulikiri kwamba yeye anadaiwa kwa niaba ya hao waliokuwa wanaimiliki meli kabla ya yeye, akikubali deni hilo kesho, Ijumaa Jumamosi watakubaliana na ataanza safari zake kwa utaratibu watakaokubaliana kulipana.

Suala la Mheshimiwa Makame Mshimba amezungumzia suala la Ukaguzi. Kiutaratibu unapopeleka maombi ya kukaguliwa chombo chako katika *ZMA* sote tunakumbuka majanga ambayo yametupata na maelekezo ya Serikali kwa ujumla, kwamba vyombo viwili hivi *ZMA* na *SUMATRA* wanapofanya uchunguzi au ukaguzi ni busara zikafanya pamoja, lakini pia *ZMA* tunao upungufu wa baadhi ya wataalamu wa ukaguzi tunalazimika baadhi ya nyakati kuajiri makampuni binafsi kuwa- *engage* kwa ajili ya kuja kufanya kazi hizi za uchunguzi.

Mara nyingine unaweza kupeleka maombi yako leo wao inabidi na wao wachukue maombi kwa ajili ya kumtafuta yule wa kuja kufanya *survey,* ikichukua muda kumpata maana yake na wewe utachelewa kufanyiwa kazi yako, lakini wakimpata haraka maana yake wanafanya ile kazi anatoa ripoti baadae *ZMA* wanaipitia ripoti, ikiwa imekidhi vigezo wanatoa ruhusa vyombo vinaendelea. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi mtu mzima na ndio maana nikatumia busara zangu za utu uzima, sijafika miaka 70 ya pencheni lakini utu uzima tayari, ndio maana nikashauri kutokana na kadhia hii Mawaziri watatu, kwa sababu Mhe. Spika, mtu kukubali kosa ambalo hakufanya yeye sio kitu rahisi, kwa sababu historia ya meli hii Mheshimiwa ilipigwa mnada na mnada wa Mahakama, na katika mnada ule kabla ya kupigwa mnada inakuwa wanaarifiwa wale wanaodai wapeleke madai yao ili katika ule mnada kitakachopatikana kilipwe, kinachobakia ndio akabidhiwe yule aliyeuziwa mali yake.

Katika hao waliokuwa wanadai Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mshimba naye anadai, lakini sikusimama hoja ya kudai haki ya Mwanasheria wangu kwa sababu yeye aliambiwa ilipokuwa mnada unataka kutangazwa katika walioleta maombi yao wanaodai wewe hukuleta ambao ni sawa sawa na Shirika la Bandari, kwa sababu meli imenadiwa, ilikuwepo bandarini lakini hawakupeleka madai yao. Kwa hivyo ina maana yeye alinunua kupitia kwenye mnada, sasa ndiyo maana akalikataa hilo deni akasema mimi hapa sidaiwi, kwa sababu meli ilinadiwa hapa na mimi kilicholipwa waliokuwa wanadai wote walilipwa.

Ndio maana nikasema hapa lazima patumike busara. Mimi naamini ushauri wangu Mawaziri watatu hawa wakikaa tukishirikishwa na sisi tulioleta hii hoja, hili suala litatatuka, kwa sababu kama sasa hivi bandari wanakosa mapato, aliyenunua meli anakula hasara maana yake kanunua kalipa keshaitengeneza meli imekaa inaoza, wananchi wanapata tabu kusafiri ndio maana mimi nikasema kwenye kutumia busara Mawaziri watatu hawa kutakuwa kuna kasoro gani, hebu naomba maelezo ya Waziri mwenyewe.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mheshimiwa huyu bwana kule kukubali kwamba anadaiwa hajakubali tutakaaje Mawaziri watatu? Si kwanza akubali kwamba anadaiwa? Na sisi Meneja wetu wa Bandari amesema akikubali leo kwamba anadaiwa yeye hana tatizo, na mimi naomba kutoa mfano kuna mwengine hivyo hivyo kafanya majaku makubwa sana lakini akasema jamani niangalieni nilivyo tumepata gharama zaidi ya milioni mia nne shirika la Bandari, lakini bado alipokuja kwangu nikawaambia jamani achana naye tutaendelea kupata hasara kwa hilo na huyu na aje hebu aone kama hatutosikilizana. Kwa nini Mawaziri watatu wakati hata kule kukubali kwamba aje tuzungumze hajakubali? Mimi sijaingia huko, ende kwa Meneja wa bandari aseme bwana hili deni mimi nakubali, kwa sababu Mheshimiwa unaponunua kitu unakubali *rights and liabilities* ndio utaratibu wa kununua, na sisi hatujasema kwamba wewe huna matatizo, unayo, lakini njoo ukubali deni naweza kuwaambia mimi msameheni, lakini sasa si kwanza akubali Mhe. Hamza, sasa Mawaziri watatu tukutane mdaiwa hajakubali kwamba anadaiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hamza mimi nadhani hebu tuache utaratibu uende kama ulivyo, na kama itakuwa kuna tatizo zaidi tutatizama uwezekano wa huo ushauri, maana hapa hatuwezi kutoa maamuzi kwa kweli kwa sababu haya mambo kuna Mahakama imo ndani imefanya shughuli zake, kwa hivyo hebu tuache hilo analosema Mhe. Waziri ili tuone tutafikia hatua gani na nini kifanyike baada ya hapo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, mimi ni mdogo sana lakini Mheshimiwa wangu Naibu Waziri kwanza Mhe. Mwenyekiti, nimegundua

hawafuatilii hawa, na ndio maana Mheshimiwa wanatujibu vile wanavyotaka wao wenyewe, ninamuheshimu sana Naibu wangu lakini nataka kumwambia kitu kidogo tu Mheshimiwa.

Mheshimiwa nilitanguliza kumsifu sana Mkurugenzi kuwa yeye akipelekewa barua *faster* kwa mujibu wa sheria anaishusha chini kwa utekelezaji, Mheshimiwa kwenda kuangalia chombo mwezi mmoja. Ndiyo maana nikamuuliza nifanye nini, nifikiri mwanzo au nifikiri mwisho baada ya kwenda kunikagua. Hakunijibu suala hilo, kumbe hajakiona ni Kiswahili kizuri kile.

Sasa kwa maana hiyo inavyotakiwa kuwa yeye yule akishushiwa mtu barua chini ilikuwa aende kwanza halafu baadaye ndiyo afikiri kwa yale aliyoyaona, hilo la kwanza.

Lakini la pili hawafanyi hivyo, *competition* hiyo na wangekuwa wanatoa ofa au mtu kumruhusu atafute Kampuni nyengine mbona tungekwenda vizuri Mhe. Mwenyekiti, wala wasingelalamika wenye vyombo na hiyo ndiyo *right*.

Mimi ninachosema ili niwaachie kuwa hilo suala walirejee kulitamka kuwa sheria hiyo anayoisema Mhe. Naibu kuwa ni ruhusa mtu kuchukua apate mwengine wakala wa nje wa kwenda kukagua vyombo na wakakubali kwa mujibu wa sheria. Naomba atamke rasmi kama wanavyofanya Idara ya Mazingira.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, labda Kiswahili changu kidogo kinamsumbua babu yangu Mhe. Mshimba.

Kwa mujibu wa Sheria ile Mkaguzi ni *ZMA*, sasa *ZMA* kwa sababu ya upungufu wa wataalamu wao, wao ndio wanao-*coordinate* kutafuta huyo mtaalamu. Kwa hivyo wewe ukipata huyo mtaalamu maana yake lazima iwe chini ya usimamizi wa *ZMA*. Maana yake hiyo ripoti lazima aje aisome *ZMA*, wao ndio wanaothibitisha hichi chombo ili kiweze kufanya kazi.

Sasa ukienda kuchukua wewe mwenyewe tu huko, ukaguzi wako, na ripoti usome wewe mwenyewe utajiruhusu wewe mwenyewe, huo sio utaratibu. Lazima mkaguzi wako apitie utaratibu wa *ZMA* ili ripoti ibaki katika *ZMA*, wao ndio wanaokuja kuwapa rai, kama wewe umeruhiwa hakuna tatizo, ama hapana kuna mapungufu haya karekebishe baadaye tutakuruhusu.

Kwa hivyo utaratibu wa kutafuta mkaguzi huyu lazima uthibitishwe na uridhiwe na *ZMA*, kufanya chengine maana yake hata akipasisha hata ukiwa huna tatizo hutoweza kupata ruhusa ya kukiendesha hicho chombo. Kwa sababu chombo kinachosimamia kitakuwa hakijajiridhisha, ndio utaratibu wa sheria Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Utaratibu kwa mujibu wa sheria utumike, nadhani tuendelee. Mhe. Makame Mshimba tunaendelea.

KIFUNGU P02 - PROGRAMU YA MIUNDOMBINU YA BANDARI NA VIWANJA VYA NDEGE

Kifungu S01 Programu Ndogo ya Miundombinu ya Viwanja vya Ndege Shs.151,457,020,000/=
Kifungu S02 Programu Ndogo

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, hapa nitafanana kidogo na suala la kituo cha daladala cha Darajani. Naomba Mhe. Waziri na Naibu Waziri tusikilizane kwa makini kabisa. Forodha Mchanga imeondolewa kuwa meli yoyote isiende. Leo kuna meli pale inaonekana kuwepo ya Kasa siku mbili tatu. Je, Sheria hii kama ile ya Viwanja vya Ndege kwa serikali tu, mnyonge huwa hana haki katika nchi hii. Narudia tena Mhe. Mwenyekiti, kwa lugha nyepesi kabisa ya chini.

Kuna meli ya Kasa inakaa siku tatu, siku nne, Forodha Mchanga, meli nyengine ikienda inakuwa imefanya kosa kwenda pale. Je, sheria hii kwa serikali haina tatizo mwananchi inambinya?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, hoja yake hii anaulizia Bandari ya Forodha Mchanga. Uamuzi wa serikali ukiondoa Bandari ya Forodha Mchanga kwa huduma za kibiashara, jambo hilo limeshafanyiwa maamuzi takriban huu mwaka wa pili Bandari ile haitumiki. Kama kuna meli iwe ya serikali iwe ya mtu binafsi bila shaka atakuwa ameruhusiwa kwa mazingira maalum. Meli anayosema ni meli ya Kasa meli ambayo inamilikiwa na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Utaratibu ni kwamba Mamlaka ya Shirika la Bandari ndio wanaomiliki eneo lile kwa ujumla wake. Kwa hiyo kama kuna maombi maalum ambayo yamepelekwa kwa Shirika la Bandari kuweza kuiruhusu ama kupakia au kushusha huo mzigo basi itakuwa hayo ni mamlaka ya Shirika, na wanaruhusika hivyo kwa mujibu wa Sheria Nam. 1 iliyoanzisha Shirika hili.

Jukumu la Serikali ni kupiga marufuku huduma za kibandari za kibiashara katika eneo la Forodha Mchanga. Namuomba Mhe. Mjumbe aendelee kusimamia maamuzi hayo ya serikali asije akaipeleka meli yake, hatua za serikali zitachukuliwa kama ataipeleka meli yake. Kama kuna tatizo au mahitaji maalum afuate utaratibu, atawasiliana na watu wa Shirika la Bandari kwa mazingira hayo maalum au tabu yake maalum au shida maalum au hiyo haja maalum ambayo itajitokeza kama wengine walivyoruhusiwa na yeye ataruhusiwa kwa mazingira

hayo, lakini ule mfumo maalum wa kiutaratibu ya bandari ya kibiashara katika eneo la Forodha Mchanga limepigwa marufuku na namuomba aendelee kusimamia maamuzi hayo ya serikali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naomba kutumia muongozo wa Sheria Nam. 4 ya mwaka 2007 Kanuni ya 59(3) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

> 59(3) "Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani, atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio ya kubuni au ya kubahatisha tu, na Spika au Mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka Mjumbe hayo anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake unaohusika".

Sasa na atoe uthibitisho Mhe. Naibu Waziri kwa hayo anayoyazungumza. Kwa kuwa meli pale inaruhusiwa ya Kasa ikae siku tatu kama pana dharura ikisha inaondoka. Athibitishe sababu gani inayokwenda pale kila wiki mara mbili mara tatu.

Hii ndio Kanuni Mhe. Spika. Sasa aje na hoja ile ile, anachojua, sitaki kubahatisha kuwapoteza wananchi. Atuone kuwa sisi hatukusoma au hatukufika hivi, humu sote Mhe. Spika, tuko sawa kwa mujibu wa Katiba. Sio anakuja anapopoa tu kama kwipi linapopoa maembe, ajibu hoja anayojua kuisimamia.

Mhe. Mwenyekiti: Hivi, Mhe. Jaku labda sijui kama na mimi sijakufahamu au vipi. Anachosema pale Mhe. Naibu Waziri ni kwamba hii meli ya Kasa ni ya Jeshi na wamepeleka ombi maalum, ndiyo alichokisema pale. Sasa sijui kama hili lina ukakasi ya kwamba labda amesema sivyo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naomba hilo ombi maalum alilete alioneshe kama lipo kweli, kama halitokwenda kutengenezwa sasa hivi. Hilo ombi linakwenda kutengenezwa sasa hivi. Hakuna ombi sisi tumeshafuatilia Mhe. Mwenyekiti.

Mimi kwanza Mhe. Mwenyekiti, nikupe taarifa siwezi kuja nikakurupuka tu hapa, na wala sisimamii hoja nisiyoijua. Nasimamia hoja kwa kujua na uwezo wake sibahatishi. Kitu nisichokijua mimi siwezi kukiuliza humu ndani nitakaa upande. Kukaa kimya si ujinga Mhe. Mwenyekiti. Sasa hizi hoja za kuja kuchukua hivi anavyotaka yeye hatuwezi, tunastahamili mengi. Hichi chombo tupo kwa niaba ya wananchi, tupo kwa mujibu wa kanuni kuihoji serikali kuisaidia. Sasa mwengine aruhusiwe.

Mhe. Spika, nimeona hayo kituo cha daladala jawabu haikutoa serikali. Nilipomwambia ajiuzulu Naibu Waziri wake na mimi Uwakilishi nipo tayari

mbona kashindwa. Tukijenga hoja, tujenge hoja za ukweli Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tuendelee wananchi wameshafahamu huko.

Kifungu Kidogo S02 Programu Ndogo ya Miundombinu ya Bandari na Usimamizi wa Usafiri wa Baharini Shs. 900,000,000/=

Jumla Kifungu P02 **Shs.152,357,020,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

KIFUNGU - P03 PROGRAMU YA HUDUMA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

Kifungu S01 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Miundombinu ya Mawasiliano Shs. 84,646,000/=

Kifungu S02 Programu Ndogo ya Usimamizi wa Huduma za Mawasiliano Shs.177,736,000/=

Jumla ya Kifungu P03 **Shs. 262,382,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

KIFUNGU P04 - PROGRAMU YA MIPANGO NA UTAWALA KATIKA SEKTA YA USAFIRI NA MAWASILIANO

Kifungu S01 Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji Shs. 986,230,000/=

Kifungu S02 Programu Ndogo

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru. Nilipotoa mchango wangu kwenye hotuba hii nilihoji uhalali wa kuwekwa kontena kwenye barabara ya Mlandege kuelekea Malindi. Mhe. Waziri alikiri kwamba kontena ile pale imewekwa kinyume na utaratibu wa Wizara.

Niwakumbushe Wizara kwamba mwaka 2013 walikuja na Sheria hapa ya Uhifadhi wa Barabara, lakini 2013 hiyo wao ndiyo wakaruhusu kontena ile kuwekwa pale tofauti na Sheria ya Hifadhi ya Barabara. Sasa wao wenyewe Sheria ile ya Hifadhi ya Barabara wameivunja kwa kuweka kontena barabarani. Wizara inakiri kwamba kontena ile imewekwa na wanavyosikia kwamba kuna barua ya mkubwa au kuna barua ya maelekezo.

Sasa mimi barua nataka nisiambiwe kwa sababu hata mimi naijua barua inayofuatiliwa, naijua na nimeiona. Lakini hii barua usinambie lakini ni kwa nini Idara yako imeruhusu kuvunja sheria wakati Idara hii ya Mipango na Sera ndiyo

Idara ambayo inatakiwa isimamiwe sheria na mipango ya wizara. Kuwekwa kontena chini ya barabara wakati ni kinyume na utaratibu wa sheria.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nilikiri kwamba kontena lile lilipo si pazuri, na sisi hapo tulipoambiwa kwamba limewekwa lile na sisi tumefuatilia kama yeye alivyofuatilia. Tunachojua kwamba suala lile ni suala la Baraza la Mji. Juzi katika mjadala hapo juu tukamueleza Mkurugenzi wa Baraza la Mji na akatwambia atalishughulikia. Sasa tena ninachotakiwa mimi zaidi nifanye nini na anayehusika nimeshamwambia. Kama ni kontena lile tu basi sasa itabidi tuyavunje yote kwa sababu sio lile tu lilokuwepo kwenye *pigment* itabidi sasa iwe ni *operation* maalum. Lakini vile vile hayo yaliyokuwa yakiwekwa lilikuwa ni suala la Baraza la Mji.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, unajua Sheria ile ya Hifadhi ya Barabara ni Sheria ya Miundombinu, na wao ndio waliotupitishia hapa wakatwambia hasa kwamba mwananchi hatakiwi ajenge chini ya mita 12, kwenye barabara kuu. Kumbe alikuwa akiambiwa mtu wa Kiwani na Muyuni sio watu wenye uwezo mkubwa.

Maana yake mimi ninayekaa Kiwani na Muyuni ukinambia barabara mita 12 nahifadhi na nalinda sheria. Wizara kumbe inajua aliyetoa agizo hili. Sasa aliyepeleka kibali kile ni Baraza la Mji ndiyo aliyetoa kibali kile. Pengine kwa idhini yangu au Mhe. Jaku, lakini sheria imevunjwa. Sasa kama mtu akitoa kibali sheria ifumbiwe macho, basi tuambiwe hapa kwamba Mwakilishi ukitoa kibali basi sheria tutaifumbia macho. Sasa Wizara inajua nani aliyetoa kibali, Manispaa kibali ndio waliotoa mimi nimekiona ile barua,sasa kwa idhini ya nani? Yako wewe Waziri, Katibu Mkuu au Mkurugenzi wa Barabara.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, sijatoa mimi kibali imetoa Baraza la Mji.

Mhe. Mwenyekiti: Labda niseme hivi, kama kuna jambo limevunja sheria, basi iwe sheria hiyo imevunjwa na chombo fulani chenginecho cha serikali.

Mimi nadhani wasimamizi wa sheria na hao waliovunja sheria tukubaliane na mkutane ili tulisawazishe jambo hilo, nadhani hiyo ndiyo itawasaidia. Lakini kusema kwamba msimamizi wa sheria asichukue hatua yule aliyeharibu sheria sasa jambo lile..., nadhani mkubaliane kwa kushauriana kati ya huyu aliyevunja sheria na nyinyi wasimamizi wa sheria hiyo, ili jambo hili liweze kusawazishwa. Tunashukuru, Mhe. Hija.

Mhe. Jaku katika hoja hii?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, niende katika hoja yangu nataka kumwambia Mhe. Naibu Waziri, hivi sasa Kasa ipo tayari imeshakaa kule, akitoka hapa afuatilie hivi sasa na akatafute hicho kibali katoa nani. Hoja ipo katika Mipango ya Sera katika Sekta ya Usafiri na Mawasiliano.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nikuombe sana kabisa, hata wewe nafikiri unapata shida unapopanda boti kwenda Dar-es-Salaam na gari yako yale makalbi yanavyotesa. Wananchi wanachangishwa huku mafuta shilingi 100 na juzi Waziri wa Fedha keshaongeza shilingi 100 nyengine maisha makali dola inapanda, mchele umepanda, sukari imepanda, mkate wa boflo umepanda, viazi zimepanda, mbatata imepanda. Makalbi yale barabara inazidi kuteseka haiwezi kusema tu. Serikali itayaondoa lini?

Mhe. Mwenyekiti, hili nikuombe sana naomba hili uniachie Mwenyekiti, namwambia tu Naibu Waziri Kasa tayari ipo kule akatafutiwa kibali kimetoka wapi?

Mhe. Mwenyekiti: Haya ni makalbi ya kule bandarini siyo?

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwanza samahani sana Mhe. Mwenyekiti, ningemuomba tu Mhe. Mjumbe aendelee kujenga heshima ya chombo hichi. Namna mjadala anavyoupeleka mimi naamini kwamba anakishushia hadhi chombo hichi.

Chombo hichi ni nguzo ya wananchi, na wananchi wangetarajia hapa kuona viongozi wao namna wanavyo-*behave* kwa kujenga taswira ya uongozi na sura wanayoiona wananchi wetu huko mitaani.

Mhe. Mwenyekiti, suala la makalbi hii leo ni mara ya saba kulijibu. Hoja ya msingi imeanzia kwamba makalbi haya yamewekwa baada ya kushauriana na wenzetu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, kipindi ambacho eneo ambalo lipo karibu sana na Wizara ya Katiba na Sheria kulikuwa kuna ujenzi unaendelea.

Maamuzi ya Kamati ya Ulinzi na Usalama wakaonelea kwamba ni busara kuweka mawe haya kwa madhumuni ya kutenganisha barabara mbili. Lakini leo hii Mheshimiwa Mjumbe analijua hilo, kwamba pale Forodhani hasa pembezoni mwa *Mercury* kuna ujenzi mkubwa unaendelea.

Sasa ikiwa wakati huo kulikuwa kunajengwa Shangani serikali ilifikia maamuzi ya kuweka makalbi yale kwa madhumuni haya. Je, leo hii ambapo kuna ujenzi unaendelea chini *Mercury*, serikali itafanyaje maamuzi mengine.

Mimi nimuombe tu kwa *concern* ya kusema kwamba makalbi yale makubwa sisi tunaikubali na ipo haja ya kuweka *pavement* zile maalum, ama mawe yale yanayong'ara au alama maalum kwa ajili ya kutenganisha barabara. Lakini kwa kuwa hilo halijafanyika, serikali ndiyo imeamua kuweka mawe kama njia ya muda ili kuweza kujiandaa kuweka hiyo michoro maalum ama kuna vibati vile maalum kwa ajili ya kugawanya barabara.

Sasa haya mengine atakayoyasema Mheshimiwa Mjumbe mimi nitakuwa simuelewi anamaanisha nini. Msingi wa serikali kuamua kulikuwa kuna ujenzi na ujenzi kama huo sasa hivi unaendelea, tena eneo ambalo lipo karibu zaidi na Bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mimi kwanza nimwambie hichi chombo nakiheshimu sana, lakini tatizo la Naibu Waziri nafikiri Mhe. Mwenyekiti, shahidi yeye mwenyewe anakuja kujibu swali humu Barazani anatokea Mhe. Haji Omar Kheri, kuja kujibu Wizara. Nafikiri yeye ndiye aliyekuwa hakiheshimu chombo hichi.
Juzi tumeshuhudia swali limeulizwa humu hapana Waziri wala Naibu Waziri, Mhe. Haji Omar Kheri, akatokea akaokoa jahazi. Sasa aliyekuwa hakiheshimu mimi au yeye? Haya majibu yake anayozungumza ya uongo ndiyo yanayosababisha tuvunjiane heshima humu na sijamvunjia heshima mimi nimetumia Kanuni, aliyoyazungumza siyo ya kweli.

Mhe. Mwenyekiti, tuendelee mimi haniathiri peke yangu yanawaathiri watu wote pale. Tuendelee tumalize.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana, nakiheshimu kiti chako na nakiheshimu chombo hichi. Kauli ya Mjumbe ya kunambia natoa kauli ya uongo naomba aifute kauli yake. *(Makofi)*

(Mhe. Jaku Hashim Ayoub hapa alitoka nje ya ukumbi)(Vicheko)

Mhe. Mwenyekiti: Tutamtafuta baadaye ili ...

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Hapana Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Maana hayumo hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, naomba iingie katika *record* kwamba kauli yake haikunifurahisha, ni ya

kunidhalilisha na ni ya kunivunjia heshima. Naomba hata kama kesho aje aifute kauli yake.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Kifungu S02 Programu Ndogo ya Mipango na Sera Katika Sekta ya Usafiri na Mawasiliano	Shs. 476,548,000/=
Kifungu S03 Programu Ndogo ya Kuratibu Shughuli za Wizara Pemba	Shs.1,405,852,000/=
Jumla ya Kifungu P04	Shs. 2,868,630,000/=
Jumla Kuu	**Shs. 189,108,700,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko, sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, wale wanaokubaliana na Makadirio hayo wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Najua makofi mengi yale ni kwa sababu kazi haikuwa ndogo. Kwa maana hiyo niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe kwa mashirikiano makubwa ya kuimaliza kazi hii.

Waheshimiwa Wajumbe Waziri anayefuatia amenambia muda uliopo hautoshi kuweza kuwasilisha hotuba yake, labda kama mutamuongezea basi unaweza ukamtosha.

(Wajumbe wamekataa kwa kupiga mayowe)

Mhe. Spika: Kwa sababu hiyo basi tusitishe shughuli zetu kuanzia sasa, na kwa maana hiyo niahirishe kikao hichi haki kesho tarehe 18/06/2015, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:28 jioni Baraza liliahirishwa hadi tarehe 18/06/2015 saa 3:00 asubuhi)